**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA RUVUMA**

# TAARIFA YA MAENDELEO YA MKOA WA RUVUMA ILIYOWASILISHWA KWA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA ZIARA YAKE YA KIKAZI MKOANI RUVUMA TAREHE 23, 2024







**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,**
**Mkoa wa Ruvuma,**
**1Barabara ya Tunduru**
**S.L.P. 74,**
**SONGEA.**
**57180, RUVUMA**

**Simu Na.025-2602256**
**Fax Na. 025-2602144**
**E-mail: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**
**Tovuti: www.ruvuma.go.tz**

**SEPTEMBA, 2024**

# RAMANI YA MKOA WA RUVUMA



**YALIYOMO**

SURA YA KWANZA ........................................................... 1
HALI YA MKOA ............................................................... 1
1.1 Jiografia: ............................................................... 1
1.2 Mwinuko wa Ardhi: ..................................................... 1
1.3 Hali ya hewa: ........................................................... 1
1.4 Eneo la Mkoa: ........................................................... 2
1.6 Utawala: .................................................................. 2
1.7 Uchumi: ................................................................... 3
1.7.1 Mazao ya Chakula ..................................................... 3
1.7.2 Mazao ya Biashara ..................................................... 4
1.8 Pato la mtu kwa mwaka ................................................. 4
1.9 Fursa muhimu za maendeleo zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma ........ 5
1.10 Hali ya ulinzi na usalama .............................................. 6
SURA YA PILI ................................................................ 7
HALI YA MAENDELEO YA MKOA ......................................... 7
2.1 Sekta ya Kilimo ............................................................ 7
2.2 Sekta ya Ushirika ......................................................... 20
2.3 Sekta ya Mifugo ........................................................... 25
2.4 Sekta ya Uvuvi. ........................................................... 30
2.5 Sekta ya Maliasili na Utalii ............................................. 37
2.6. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma .......... 39
2.7 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ............ 47
2.8 Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ...................... 53
2.8.1 Viwanda ................................................................... 53
2.8.2 Biashara .................................................................. 54
2.8.3 Uwekezaji ................................................................ 57
2.9 SIDO ......................................................................... 67
2.10 Sekta ya Madini .......................................................... 73
2.11 Sekta ya Ardhi na Makazi ............................................. 81
2.12 Ujenzi - Barabara -TANROADS ...................................... 89

2.13 Ujenzi - Barabara – TARURA ........................................ 99
2.14 Mawasiliano na Uchukuzi........................................... 106
2.15 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania Bandari.
.......................................................................................... 107
2.16 Usafiri wa anga........................................................... 109
2.17 Sekta ya Nishati ......................................................... 114
2.18 Sekta ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii.................. 126
2.19 Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ........................ 141
2.20 Sekta ya Maji.............................................................. 160
2.20.1 Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira
(RUWASA) ........................................................................ 160
2.20.2 Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea
(SOUWASA)........................................................................ 177
2.21 Maendeleo ya Jamii. .................................................. 185
2.22 Sekta ya Utawala ....................................................... 191
2.22.3 Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya
Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 2023/24. .................. 199
2.22.4 Ujenzi wa Miundombinu Mbalimbali ya Sekretarieti ya
Mkoa.................................................................................... 200
2.22.6 Hitimisho.................................................................... 202

# SURA YA KWANZA
# HALI YA MKOA

## 1.0 Usuli

### 1.1 Jiografia:

Mkoa wa Ruvuma uko kusini mwa Tanzania kati ya latitudo 9°35’ na 11° 45’ Kusini mwa Ikweta na kati ya longitudo 34°38’ na 38°10’ Mashariki mwa mstari wa Meridiani. Upande wa kusini Mkoa huu umepakana na nchi ya Msumbiji, Mashariki unapakana na Mikoa ya Lindi na Mtwara, Kaskazini unapakana na Mkoa wa Morogoro, Kaskazini Magharibi unapakana na Mkoa wa Njombe na upande wa Magharibi Mkoa huu unapakana na nchi ya Malawi.

### 1.2 Mwinuko wa Ardhi:

Sehemu kubwa ya Mkoa wa Ruvuma kwa upande wa Mashariki ni tambarare ambayo ipo kwenye mwinuko wa kati ya mita 300 hadi mita 2000 kutoka usawa wa bahari na kwa upande wa Magharibi ina sehemu kubwa ya milima ambayo ipo kwenye mwinuko wa kuanzia mita 300 hadi mita 2000 kutoka usawa wa bahari.

### 1.3 Hali ya hewa:

Mkoa una joto la wastani wa nyuzi joto 23$^{o}$C. Joto hili huongezeka hasa mwezi Oktoba hadi kufikia nyuzi joto 30$^{o}$C na kupungua wakati wa baridi hasa mwezi Julai kufikia nyuzi joto 13$^{o}$C.

Mkoa huu ni kati ya Mikoa michache nchini yenye bahati ya kupata mvua za kutosha ambazo hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Mei kila mwaka. Wastani wa kiasi cha mvua inayonyesha kwa mwaka ni mm.1100. Kiasi cha juu ni mm.1600 ambacho hupatikana katika

Wilaya ya Mbinga kwenye miinuko ya milima ya Umatengo na kiasi cha chini ni mm 803 ambacho hupatikana katika Wilaya ya Tunduru.

**1.4 Eneo la Mkoa:**

Eneo la Mkoa ni kilometa za mraba 67,372 na kati ya hizi, kilometa za mraba 2,978 (sawa na asilimia nne) zimefunikwa na maji katika ziwa Nyasa, kilometa za mraba 6,958 (sawa na asilimia 11) ni eneo la Hifadhi ya misitu ya Taifa na kilometa za mraba 50,673 ni eneo linalofaa kwa kilimo, (sawa na asilimia 79) ya eneo lote. Aidha, eneo la kilomita za mraba 3,624 ni eneo lisilofaa kwa kilimo, (sawa na asilimia sita) ya eneo lote la Mkoa.

Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Ruvuma una watu 1,848,794 (wanawake 946,496 na wanaume 902,298) ikiwa ni ongezeko la watu 471,903 sawa na asilimia 2.9 ikilinganishwa na idadi ya watu 1,376,891 kwa sensa ya mwaka 2012.

**1.6 Utawala:**

Mkoa una wilaya tano (5) za Kiserikali ambazo ni Tunduru, Songea, Mbinga, Namtumbo na Nyasa. Aidha, Mkoa una Halmashauri nane (8) ambazo ni Halmashauri za wilaya ya Songea, Tunduru, Mbinga, Namtumbo, Nyasa, Madaba, Manispaa ya Songea na Mji Mbinga. Mkoa una Idadi ya Tarafa 24, Kata 173, Vijiji 551 Mitaa 124 na Vitongoji 3,693 kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:-

**Jedwali Na. 1: Takwimu za Mkoa wa Ruvuma zinazoonesha eneo, idadi ya watu na utawala mwaka 2022**

| Halmashauri | Tarafa | Kata | Vijiji | Mitaa | Vitongoji | Kaya | Watu (2022) | Eneo (Km. za Mraba) | Msongamano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** |
| TUNDURU | 7 | 39 | 157 | 0 | 1,179 | 110,208 | 412,054 | 18,778 | 22 |
| MBINGA MJI | 1 | 19 | 49 | 29 | 273 | 39,979 | 158,896 | 1,248 | 127 |
| MBINGA (V) | 5 | 29 | 117 | 0 | 783 | 69,775 | 285,582 | 6,338 | 45 |
| SONGEA | 2 | 16 | 56 | 0 | 443 | 45,198 | 178,201 | 6,664 | 27 |
| MADABA | 1 | 8 | 22 | 0 | 170 | 16,725 | 65,215 | 6,791 | 10 |
| SONGEA MANISPAA | 2 | 21 | 0 | 95 | 0 | 76,927 | 286,285 | 394 | 727 |
| NAMTUMBO | 3 | 21 | 66 | 0 | 424 | 63,274 | 271,368 | 20,370 | 13 |
| NYASA | 3 | 20 | 84 | 0 | 421 | 44,737 | 191,193 | 6,789 | 28 |
| **JUMLA** | **24** | **173** | **551** | **124** | **3,693** | **466,823** | **1,848,794** | **67,372** | **29** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - (2024)*

** Msongamano wa watu (population density) kwa kilometa moja (1) ya mraba.*

## 1.7 Uchumi:

Uchumi wa Mkoa hutegemea kilimo ambapo zaidi ya asilimia 87 ya wakazi wake hupata kipato chao kutokana na shughuli hizo na kuweza kuchangia pato la Taifa na pato la Mkoa. Aidha, shughuli nyingine muhimu za kiuchumi ni pamoja na ufugaji mdogo mdogo, uchimbaji madini, biashara, uvunaji mazao ya misitu na maliasili nyingine mbalimbali.

### 1.7.1 Mazao ya Chakula

Mazao ya chakula yanayolimwa Mkoani Ruvuma hujumuisha Mahindi, Mpunga, Muhogo na Maharage. Mazao mengine ni Mtama, Ulezi, Mbaazi, Viazi Vitamu na Jamii ya Mikunde.

### 1.7.2 Mazao ya Biashara

Mazao makuu ya biashara yanayolimwa Mkoani Ruvuma ni Tumbaku, Kahawa na Korosho. Pia Mkoa wa Ruvuma unalima ufuta, alizeti, karanga, tangawizi, parachichi, ndizi, mpunga, maharage, mbaazi na soya kwa ajili ya biashara. Aidha, kwa upande wa zao la mahindi pamoja na kuwa ni zao la chakula lakini wananchi wanalitumia kama zao la biashara.

## 1.8 Pato la mtu kwa mwaka

Pato la Mkoa wa Ruvuma (*Regional/Gross Domestic Product* - GDP) limeongezeka kutoka **Tshs. 5,108,7492,000,000.00** mwaka 2019 hadi **Tshs. 7,173,946,000,000.00** mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia **40.4**. Aidha, pato la Taifa la mtu (*Per Capital income*) kwa mwaka 2019 lilikuwa **Tshs 3,159,417** na limeongezeka hadi **Tshs. 3,721,073** mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia **17.8.**

Pato la mkoa na mtu kwa mwaka kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka 2023 ni kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na 2.

**Jedwali Na. 2: Pato la Mkoa na mwananchi (*per capital income*) Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | Mwaka | Pato la Mkoa (RGDP) kwa Tshs (Milioni) | Wastani wa pato la mwananchi kwa mwaka (Tshs.) | Nafasi Kitaifa (Pato la mwananchi) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2019 | 5,108,749 | 3,159,417 | 4 |
| 2. | 2020 | 5,506,421 | 3,326,252 | 4 |
| 3. | 2021 | 5,911,176 | 3,487,302 | 4 |
| 4. | 2022 | 6,393,738 | 3,458,329 | 6 |
| 5. | 2023 | 7,173,946 | 3,721,073 | 5 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu - (2024)

**1.9 Fursa muhimu za maendeleo zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma**

Mkoa wa Ruvuma una fursa kadhaa ambazo hutumiwa katika kusukuma mbele maendeleo ya Mkoa. Fursa za msingi ni kama zifuatazo: -

(i) **Eneo kubwa linalofaa kwa kilimo:**

Eneo kubwa la ardhi katika Mkoa wa Ruvuma inafaa kwa kilimo cha mazao yote ya chakula na biashara.

**(ii) Hali nzuri ya hewa:**

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa michache nchini yenye bahati ya kupata mvua za kutosha ambazo hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Mei kila mwaka. Wastani wa kiasi cha mvua inayonyesha kwa mwaka ni mm 1100.

(iii) **Mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji**:

Mkoa una jumla ya eneo la **Ha. 59,943** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

(iv) **Kuwepo kwa mazao ya kudumu ya chakula na biashara katika kila Wilaya:**

Mazao yote makuu ya biashara yanayolimwa mkoani Ruvuma, yanapatikana/yanalimwa katika wilaya zetu zote 5. Mazao hayo ni pamoja na mahindi, mpunga, kahawa, korosho na tumbaku.

(v) **Uwepo wa Maliasili**:

Mkoa wa Ruvuma una maliasili nyingi zikiwemo madini, ziwa nyasa, wanyama pori, misitu ya asili na mito inayotirirsha maji mwaka mzima.

(vi) **Kuwepo kwa nguvukazi ya kutosha**:

Mkoa una wananchi wenye ari kubwa ya kufanya kazi kwa bidii kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka.

(vii) **Uwepo wa miundombinu ya Usafirishaji**

Kufunguka kwa miundombinu ya barabara inayounganisha Makao makuu ya Mkoa na Wilaya pamoja na Mikoa mingine inayotuzunguka kwa kiwango cha lami.

## 1.10 Hali ya ulinzi na usalama

Kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama wa Mkoa ni shwari, ikiwa ni pamoja na mpakani na nchi jirani za Msumbiji na Malawi. Hakuna matukio makubwa ya uvunjifu wa amani yaliyojitokeza, wananchi wameendelea kujishughulisha na shughuli mbalimbali za maendeleo katika hali ya amani na utulivu. Vile vile wananchi wameendelea kuhamasishwa katika ulinzi shirikishi ili kulinda mali zao na usalama wa raia.

# SURA YA PILI

## HALI YA MAENDELEO YA MKOA

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii maelezo yametolewa ili kuelezea hali ya Maendeleo ya sekta mbalimbali Mkoani Ruvuma kwa kuzingatia Vipaumbele kama vilivyoainishwa katika Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Mpango Mkakati wa Mkoa, Halmashauri na Taasisi za Umma, na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa. Aidha, taarifa hii pia imeelezea mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa; changamoto za maendeleo zilizopo na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo.

### 2.1 Sekta ya Kilimo

#### 2.1.1 Hali ya Sekta ya Kilimo

**a) Eneo linalofaa kwa Kilimo**

Mkoa wa Ruvuma una Jumla ya Hekta **4,007,746** zinazofaa kwa kilimo, hadi sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **897,171** sawa na asilimia **22** ya eneo lote**,** na kufanya Mkoa kuwa na ziada ya hekta **3,110,575** sawa na asilimia **78.**

**b) Eneo la Kilimo cha Umwagiliaji**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya hekta **197,108.2** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta 7,388.3 zimeendelezwa,hii ni sawa na asimilia **3.7**. Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa skimu **23** zinafanya kazi na **19** hazifanyi kazi. Skimu **23** zinazofanya

kazi zina ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili, eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji **hekta 5,420** na eneo linalomwagiliwa lenye ukubwa wa **hekta 1,182.**

**c) Mazao ya Chakula**

Mazao ya chakula yanayolimwa Mkoani Ruvuma yanajumuisha Mahindi, Mpunga, Mihogo na Maharage. Mazao mengine ni Mtama, Ulezi, Mbaazi, Viazi Vitamu na Jamii ya Mikunde.

**d) Mazao ya Biashara**

Mazao makuu ya biashara yanayolimwa Mkoani Ruvuma ni Tumbaku, Kahawa na Korosho. Pia Mkoa wa Ruvuma unalima ufuta, alizeti, karanga, tangawizi, parachichi, ndizi, mpunga, maharage, mbaazi na soya kwa ajili ya biashara. Aidha, kwa upande wa mazao ya mahindi na mbaazi pamoja na kuwa ni mazao ya chakula lakini wananchi wanayatumia kama mazao ya biashara.

**e) Maafisa Ugani**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Watumishi Maafisa Kilimo **300** kati ya mahitaji ya Maafisa Kilimo **900** na upungufu wa Maafisa Kilimo **600**. Tunaishukuru serikali kwa kuwa imejiwekea utaratibu wa kuajiri mara kwa mara katika ngazi za Halmashauri. Jedwali Na. 3 linaonesha idadi ya Maafisa Kilimo katika ngazi ya mkoa na Halmashauri.

**Jedwali Na. 3: Idadi ya wataalamu wa kilimo kwa kila Halmashauri**

| Halmashauri/ *RS* | Wanaohitajika | Waliopo | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| **RS** | 3 | 3 | 0 |
| Tunduru DC | 203 | 62 | 141 |
| Namtumbo DC | 94 | 65 | 29 |
| Mbinga DC | 153 | 40 | 113 |
| Nyasa DC | 111 | 20 | 91 |
| Songea DC | 79 | 40 | 39 |
| Madaba DC | 30 | 17 | 13 |
| Songea MC | 123 | 27 | 96 |
| Mbinga TC | 104 | 26 | 78 |
| **Jumla** | **900** | **300** | **600** |

***NB: Kila Kata, Kijiji na Mtaa na Makao Makuu inatakiwa kuwa na Afisa mmoja.***

### 2.1.2 Hali ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

#### a) Malengo na uzalishaji wa mazao;

#### i. Malengo ya Kilimo kwa msimu wa kilimo 2023/2024

Mkoa ulilenga kulima hekta **1,006,325** za mazao ya Chakula, Biashara na mazao ya Bustani zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **2, 168,041** kati ya hekta hizo, hekta **642,906** ni za kilimo cha mazao ya Chakula zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,882,473** na hekta **348,441** ni za kilimo cha mazao ya Biashara zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **100,557.** Mazao ya Bustani jumla ya hekta **14,978** zilitarajiwa kulimwa na matarajio ni kupata mvuno ya tani **185,012.**

#### ii. Utekelezaji wa msimu wa kilimo mwaka 2023/2024

Mkoa umezalisha tani **2,052,449.09 za mazao kati ya hizo tani 1,955,763.76** ni za mazao ya chakula na **tani 96,685.33 n**i za mazao

ya biashara. Makadirio ya mahitaji ya chakula ni tani **470,000** hivyo kuwa na ziada ya tani **1,485,763.76**.

### iii. Malengo ya Kilimo kwa msimu wa kilimo 2024/2025

Mkoa umelenga kulima hekta **1,379,036** za mazao ya Chakula, Biashara na mazao ya Bustani zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **2,158,704** kati ya hekta hizo, hekta **998,745** ni za kilimo cha mazao ya chakula zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,842,503** na hekta **363,055** ni za kilimo cha mazao ya Biashara zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **101,252.** Mazao ya Bustani jumla ya hekta **17,236** zitalimwa na matarajio ni kupata mavuno ya tani **214,949.**

### 2.1.3 Mpango wa kuendeleza Mazao

#### (a) Parachichi

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani **1,768** zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani **37,500** ifikapo mwaka **2025.** Mpango wa kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi unatekelezwa kupitia mkakati wa kuhamasisha wakulima kulima parachichi kupitia vikundi ambapo mpaka sasa jumla ya ekari **600** zimekwishapandwa. Aidha mpango huu unafanywa na Mkoa kwa kushirikiana na Taasisi ya **(SAGCOT).**

#### (b) Kahawa

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani **23,355** hadi kufikia Tani **55,000** za kahawa safi ifikapo mwaka **2025.**

Kwa msimu huu masoko ya kahawa yanaendelea ambapo vyama vya msingi vinaendelea kukusanya kahawa.

**(c) Soya**

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la Soya kufikia **tani 10,000** kwa msimu wa **2023/24** tumezalisha tani **1,208,770.50.** Mkoa na Wizara ya kilimo wanaendelea kusimamia na kuhamasisha wananchi waongeze uzalishaji wa zao hili. Kwa sasa Shirika la Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (**SAGCOT)** linaendelea kutekeleza mradi wa kuendeleza zao la soya katika Halmashauri zinazolima soya unaoitwa **TSSI** - Tanzania Sustainable Soybean Initiatives.

**(d) Korosho**

Mkoa unaendelea na juhudi za kuongeza uzalishaji wa zao la Korosho kwa kuendelea kuhimiza uboreshaji wa miti ya mikorosho, matumizi sahihi ya viuatilifu na kuanzisha mashamba mapya ya miche ya kisasa**.** Masoko ya korosho kwa msimu wa 2024/2025 yanatarajia kuanza mwezi Oktoba.

**(e) Ufuta**

Mkoa ulilenga kuongeza uzalishaji wa zao la Ufuta kutoka **tani 9,649** kwa msimu wa **2022/23** hadi kufikia tani **12,061** kwa msimu wa **2023/24.** Kutokana na juhudi zilizofanyika msimu huu Mkoa umezalisha tani **14,312.**

**2.1.4 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

#### 2.1.4.1 Mbolea za Chumvichumvi

i. **Upatikanaji wa Mbolea Msimu 2023/2024**

Mkoa wa Ruvuma katika Msimu wa kilimo **2023/2024** kuanzia mwezi Julai 2023 hadi kufikia Mwezi **Juni, 2024** zimeingizwa jumla ya tani **113,000** na kusambazwa kwa wakulima mahitaji yalikuwa ni tani **112,692**. Tani **16,854** zimeendelea kutumika kwenye mazao yasiyotegemea msimu wa mvua na maandalizi ya msimu wa mwaka 2024/25. Jedwali Na. 4 linaonesha mchanganuo wa upatikanaji wa mbolea.

**Jedwali Na. 4: Upatikanaji wa Mbolea kutoka msimu 2020/2021 hadi 2023/2024**

| Msimu | Mahitaji (Tani) | Uingizaji (Tani) | Asilimia ya uingizaji |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 50,910 | 43,000 | 84.5 |
| 2021/2022 | 50, 524.50 | 33,501.07 | 66 |
| 2022/2023 | 80,000 | 71,000 | 87.5 |
| 2023/2024 | 112,692 | 129,854 | 115.2 |

ii. **Bei za Mbolea**

Bei za sokoni za mbolea ni kati ya sh.**60,000.00** hadi sh.**132,000.00** na bei za ruzuku za mbolea ni kati ya sh.**50,000.00** hadi sh.**70,000.00** Tunaipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea ambayo imempunguzia mzigo wa gharama za uzalishaji mkulima.

iii. **Usajili wa Wakulima**

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilizindua rasmi mfumo wa mbolea za Ruzuku Agosti, 2022 ambapo zoezi la usajili kwa wakulima lilianza

tarehe 01 Agosti, 2022. Kwa msimu wa mwaka **2023/2024** Mkoa wa Ruvuma umesajili jumla ya wakulima **389,446** kati ya lengo la kusajili wakulima **428,288.00** sawa na asilimia **90.9**.

**iv. Idadi ya Vituo vya Kuuza na Kusambaza Mbolea**

Kwa msimu wa mwaka 2023/24 ya vituo **205** vilisajiliwa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa ajili ya kutumika kuuza mbolea ya ruzuku kwa wananchi.

### 2.1.5 Mbegu Bora

**i. Mahitaji ya mbegu**

Mkoa wa Ruvuma una mahitaji ya kutumia mbegu bora za nafaka, mikunde na mazao ya mafuta jumla ya tani **19,530.34** kati ya hizo mahindi tani **10,431.95**, mpunga tani **1,576.05**, Maharage tani **6,360**, Soya tani **536.06**, mbaazi tani **449.85**, ufuta tani **119.8** na alizeti tani **56.63**.

**ii. Upatikanaji wa mbegu mbalimbali za mazao**

**Mbegu ya ufuta;** Mkoa ulipata mgao wa mbegu bora za ufuta zenye ruzuku ya Serikali jumla ya **tani 2** kutoka TARI Naliendele ambazo zimegawiwa bure kwa wakulima wa ufuta kwenye Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma.

**iii. Mbegu za mahindi zinapatikana kupitia soko huru;** ambapo Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imetoa bei elekezi ya mbegu za mahindi ambazo zitapatikana kwa bei ya ruzuku. Lengo la serikali ni kumpunguzia mkulima gharama za kununua mbegu bila kuathiri Wafanyabiashara (Makampuni na Mawakala wa Pembejeo) wanaozalisha/ kusambaza mbegu.

**iv. Miche Bora - Miche ya Kahawa**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Bodi ya kahawa Tanzania, TACRI, Halmashauri na wadau wengine wa kahawa umesambaza jumla ya miche **2,716,801** na zoezi la usambazaji wa miche hiyo kwa msimu 2023/2024 limekamilika.

### 2.1.6 Miradi ya Ujenzi

**i. Ujenzi wa Maghala 28 ya Kuhifadhia Mazao**

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo unaendelea na zoezi la ujenzi wa maghala **28** yatakayotumika kuhifadhi mazao ya wakulima kwenye Vijiji na Miji. Hadi kufikia mwezi Julai, jumla ya maghala **27** yameezekwa na kujengwa kuta za bati ("roofing and cladding") na ghala **1** lipo katika hatua ya kufungwa vyuma ("frames"). Aidha, shughuli za kukamilisha ujenzi (finishing) zinaendelea ambapo maghala **21** yamesakafiwa zege na maghala **23** yamefungwa gata na

feni. Kwa ujumla hatua ya ujenzi na maandalizi ya vifaa umefikia asilimia tisini (**97%**).

**ii. Ujenzi wa nyumba za maafisa ugani**

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imepanga kujenga nyumba 5 za maafisa ugani kwenye Mkoa wa Ruvuma (Tunduru nyumba 1, Songea DC 1, Mbinga DC 1, Mbinga TC 1 na Namtumbo DC 1). Fedha kiasi cha Shilingi **200,000,000.00 zimetolewa mwezi Juni,2024** ambapo kila Halmashauri imepata shilingi **40,000,000.00** za ujenzi na taratibu za ujenzi zinaendelea.

### 2.1.7 Vitendea kazi kwa Maafisa Ugani

Mkoa wa Ruvuma ulipokea pikipiki 281 kati ya pikipiki 7000 zilizotolewa na Mhe.Rais kupitia Wizara ya Kilimo. Hivyo maafisa ugani wote wa Kata na Vijiji waliopo katika Mkoa wa Ruvuma kila mmoja alipata pikipiki moja. Aidha, Serikali imeleta mashine (Soil Scanner) **7** za kupima udongo na kuzigawa kwenye Halmashauri za Mbinga Mji, Songea Vijijini, Mbinga Vijijini, Nyasa, Madaba na Tunduru ambazo zinaendelea kutumika kupima afya ya udongo. Wizara inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na vitendea kazi vya kutosha.

Mwezi Agosti, 2024 Mkoa ulipokea gari moja **(1)** la usimamizi wa mazao ngazi ya Mkoa, sare za kazi **289** kwa ajili ya Maafisa Kilimo wote wa ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na Vijiji. Tunaishukuru sana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendele kutoa vitendea kazi hivi kwani

vinaongeza ari ya kufanya kazi na hatimaye kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima wa Mkoa wetu.

### 2.1.8 Upimani wa Afya ya Udongo kwa Wakulima wadogo

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti cha Uyole chini ya Mradi wa OCP imefanikiwa kupima Afya ya Udongo, imefanya mashamba darasa kwa ajili ya chanjo na mapendekezo ya mbolea kwa Wakulima pamoja na uendelezaji wa tool ya kusaidia kupata takwimu sahihi za uzalishaji kupitia satelaiti

(a) Upimaji wa Afya ya Udongo

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Tari Uyole ilipima Afya ya udongo katika Vijiji 100 ambavyo uteuzi wake ulizingatia maeneo yenye uzalishaji mkubwa, uwakilishi wa aina ya Mazao yanayolimwa na uwakilishi wa udongo, aina ya Mazao yanayolimwa kwenye Halmashauri husika. Matokeo yalionesha maeneo ya madaba,Mbinga na Nyasa yana Asidi nyingi na hivyo yanahitaji kuboreshwa kwa kuweka chokaa, aidha kwa ujumla maeneo mengi yanaupungufu wa Nitrojeni (N), Fosfati(P), na Potasiam(K). Aidha, madini mengine ni pamoja na Kalsiam, Organic Carbon, Boron na Zinc. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo inatarajia kupima Afya ya Udongo kwa Mkoa wote wa Ruvuma na kutengeneza ramani za muongozo wa wa matumizi ya mbolea.

**(b) Kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea**

Yalifanyika mashamba darasa ya Mahindi katika Halmashauri za Madaba, Namtumbo, Songea Vijijini na Songea Manispaa kwa ajili ya kuonesha matokeo ya mbolea mbalimbali za kupandia na kukuzia. Katika kipindi cha mavuno ilionesha kuwa kuna hitaji kubwa la matumizi ya mbolea za kupandia, salfa na Boron ili kutoa matokeo mazuri ya uzalishaji. Pia Wakulima walijionea matokeo ya kutumia chanjo (Inoculant) kwenye mashamba darasa ya Soya ambapo matokeo yalionesha kuwa kwenye eneo ilipotumika chanjo pekee uzalishaji ulikuwa ni mkubwa na pods zilionesha kujaa vizuri ukilinganisha na maeneo ambapo haikutumika.

(c) **Utengenezaji wa Tool ya kutoa uzalishaji kupitia Satelaiti**

Mkoa kwa kushirikiana na Tari Uyole chini ya ufadhili wa Kampuni ya OCP ya Morroco inaendelea kutekeleza mradi wa kukusanya takwimu za hatua mbalimbali ukuaji na za uzalishaji wa Mazao kwa kutumia GIS unaolenga kutengeneza Tool ambayo itawasaidia maafisa Kilimo kupata takwimu sahihi za uzalishaji kupitia satelaiti ambazo zitaonesha hekta zilizolimwa na uzalishaji wake. Tool hii itasaidia kupata takwimu sahihi na kuwezesha Mkoa na Taifa kwa ujumla kufanya maamuzi sahihi yanayohusiana na Biashara za Mazao na Usalama wa Chakula kwa ujumla, ambapo hadi sasa program bado inaendelea.

### 2.1.9 Mafunzo kwa Wakulima na uhamasishaji wa tekinolojia

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo AGRA, AMDT,MCODE, CARITAS Songea, RUATI, RIKOLTO, BRITEN, HRNS na wadau wengine imeendelea kutoa huduma za Ugani, kuendeleza minyororo ya thamani na kuwawezesha Wakulima kupata mitaji ya kuingia shambani. Pia tumeendelea kuhamasisha matumizi ya tekinolojia mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ya matumizi sahihi ya Viuatilifu, Matumizi ya Chokaa Mazao, Mbinu za kuzuia upotevu wa Mazao, kubadilisha fikra za Wakulima kufanya Kilimo Biashara na umuhimu wa kupima Afya ya Udongo.

**2.1.10 Mafanikio ya Sekta ya Kilimo**

(a) Kuwepo kwa mfumo wa ruzuku ya mbolea ya Serikali kumesaidia kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na manufaa mengine kama ifuatavyo;

i. Kupunguza gharama za mbolea kwa mkulima kwa asilimia 50
ii. Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea yanayoashiria kuongeza uzalishaji wa mazao;
iii. Kuongezeka kwa matumizi ya simu katika Sekta ya kilimo, hii ni kutokana na zoezi la usajili wa wakulima.
iv. Wakulima kuongeza ukubwa wa mashamba yao na kuongeza uzalishaji wa mazao.
v. Mfumo umesaidia kutambua idadi ya wakulima

vi. Mfumo umewezesha kuibua mpango wa vyama vya Ushirika kusajiliwa na kufanya kazi ya kusambaza mbolea kwa wakulima wake kama Mawakala, lengo ni kusogeza huduma kwa wakulima wanaowahudumia.

vii. Kupitia mfumo huu Serikali imeweza kusimamia na kudhibiti uchakachuaji (uuzaji wa mbolea zisizokuwa na kiwango / ubora.

viii. Kupitia mfumo huu Serikali imeweza kusimamia bei za mbolea kwa wakulima.

ix. Kupitia mfumo Mkoa na nchi kwa ujumla umeweza kupata Takwimu sahihi za mahitaji na matumizi ya mbolea.

(b) Maafisa ugani kupewa Vitendea kazi hasa pikipiki, mashine za kupima afya ya udongo, makoti ya mvua na Mabuti ambavyo vimeboresha utendaji wa kazi kwenye vituo vyao.

(c) Serikali Kupitia wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA) kuendelea kununua mahindi ya wakulima kwa bei ya juu ya Tsh **700** kwa kilo ikilinganishwa na bei ya sokoni ambayo ilikuwa ni Tsh 380 - 400.

(d) Serikali kuendelea kuboresha mindombinu ya kuhifadhi mazao ya wakulima na kupunguza upotevu wa mazao na kuzuia sumu kuvu katika mazao kwa kujenga maghala **28** ya kisasa ya mpango wa kuhifadhi mazao vijijini na ghala moja mradi moja kupitia mradi wa sumu kuvu.

(e) Serikali kuendelea kuimarisha mifumo ya kidigitali ya masoko ikiwemo mfumo wa stakabadhi za ghala na TMX.

f) Serikali kuendelea kuweka Mazingira ya Uwekezaji katika kilimo; mathalani katika Mkoa wa Ruvuma tumepata mwekezaji wa kuzalisha

sukari ambaye atazalisha miwa katika shamba la zaidi ya ekari **40** na kutengeneza sukari.

g) Serikali kuendelea kuimarisha mifumo ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali kupitia mashamba ya ASA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo; TARI, TOSCI, Vyuo vya kilimo, Makampuni na watu binafsi.

## 2.2 Sekta ya Ushirika

### 2.2.1 Hali ya Ushirika katika Mkoa wa Ruvuma

Mkoa una jumla ya Vyama vya Ushirika **299,** kati ya hivyo AMCOS **227,** Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) **63,** Vyama vingine **6** na Vyama Vikuu (UNION) **3** ambavyo ni TAMCU Ltd, SONAMCU Ltd, na MBIFACU Ltd.

Mchanganuo wa Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa ajili ya Kahawa ni vyama **114**, Korosho **46**, Tumbaku **45**, na mazao mchanganyiko **22**. Vyama vya msingi vya zao la Kahawa na Korosho vinahudumia wakulima wa mazao ya Kahawa, Korosho na mazao ya nafaka katika maeneo yao kwa kufuata Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Vyama vya Msingi vya Zao la Tumbaku vinahudumia wakulima wanaolima mazao ya nafaka yanayouzwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

### 2.2.2 Elimu na Mafunzo

Kamati ya Elimu Mkoa (KAMEURU) inayoongozwa na Mrajisi Msaidizi inaendelea na utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali wa Vyama vya Ushirika. Julai, 2024 Idadi ya Vyama vilivyopata mafunzo ni **114**.

Lengo la mafunzo ni kuvijengea Vyama uwezo ili vifanye kazi kulingana na Sheria na Kanuni zake.

### 2.2.3 Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *Bodi ya* Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Mamlaka ya Udhibiti wa nafaka Mazao Mchanganyiko (COPRA), Soko la bidhaa Tanzania (TMX) na wadau wa mazao ya Ufuta, Soya, Mbaazi, Korosho, Kahawa unaratibu masoko ya mazao ya kipaumbele kwa njia ya minada inayosimamiwa na Vyama Vikuu vya Ushirika (SONAMCU LTD, TAMCU LTD na MBIFACU LTD).

Mfumo wa Stakabadhi ulianza kupitia zao la Korosho msimu wa 2016/2017 na Mazao mchanganyiko (Soya, Ufuta na Mbaazi) ulianza msimu 2018/2019. Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unatekelezwa kwa kuzingatia Mwongozo ulioandaliwa kwa ushirikiano wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Usimamizi wa Maghala.

### 2.2.4 Uendeshaji wa Masoko (Mazao ya Ufuta, Soya na Mbaazi)

Uendeshaji wa masoko ya mazao ya Ufuta, Mbaazi na Soya hufanyika kupitia wakulima kukusanya mazao kupitia Vyama vya Msingi **101** na Vyama Vikuu **2,** kati ya hivyo Namtumbo vyama **45**, Songea **15**, Mbinga **5**, Nyasa **1** na Tunduru **35**.

#### (i) a) Zao la Ufuta

Kwa msimu wa masoko 2024/2025 minada ya Ufuta ilianza katika AMCOS ya Namtumbo tarehe 22/05/2024. Hadi kufikia tarehe 18/08/2024 jumla ya minada 25 imefanyika ambapo Songea na Namtumbo (chini ya SONAMCU) minada **15** na Tunduru (TAMCU) **10**. Jumla ya kilo zilizouzwa ni **14,312,899.60** zenye thamani ya shilingi **48,461,004,105.10. Minada imemalizika**

#### (ii) Zao la Soya

Kwa msimu wa masoko **2024/2025** imefanyika minada **kumi na tatu (13)** ambapo mnada wa kwanza ulianza tarehe 20/06/2024. Hadi kufikia tarehe 17/08/2024 jumla ya kilo **1,208,770.50** zenye thamani ya kiasi cha shilingi **1,621,528,952.00. Minada imemalizika.**

#### (iii) Zao la Mbaazi

Kwa msimu wa masoko 2024/2025 Mnada wa kwanza ulianza tarehe 15/08/2023 wilayani Tunduru. Ambapo mpaka sasa imefanyika minada sita (Songea na Tunduru) na kufanya jumla ya kilo zilizouzwa kuwa **10,445,227.00** zenye thamani ya kiasi cha shilingi **18,767,746,791.00 Minada inaendelea.**

### 2.2.5 Uendeshaji wa Mazao ya Korosho, Kahawa na Tumbaku

#### (i) Zao la Kahawa

Masoko ya kahawa yanaendelea ambapo vyama vya msingi vinaendelea kukusanya kahawa. Baadhi ya Vyama vya msingi vinauza katika masoko ya awali kwa kujaza mikataba na Makampuni

mbalimbali. Kuishia tarehe 14/08/2024 Mikataba ya mauziano kwa vyama 68 imeidhinishwa na Ofisi ya Mrajisi Msaidizi yenye kilo zilizouzwa **3,377,349.30** kwa bei ya wastani ya shilingi **8,050** kwa kahawa ya "***home parchment".***

Mnada wa kwanza wa kahawa ya Arabica kwa msimu 2024/2025 umefanyika Moshi tarehe **15/08/2024** jumla ya kilo **634,747.00** za Vyama vya Mkoa wa Ruvuma ziliuzwa kwenye mnada huo. Mpaka kuishia tarehe 29 Agosti imefanyika minada matatu (3) yenye jumla ya kilo **1,115,183.00.**

**(ii) Zao la Korosho**

Masoko ya korosho kwa msimu wa 2024/2025 yanatarajia kuanza mwezi Oktoba. Kwa sasa bado wakulima wanaendelea kuhudumia mashamba. Chama Kikuu TAMCU kilikuwa na bakaa ya magunia **166,177** na imeshapokea magunia **501,683** kwa ajili ya maandalizi ya masoko yanayotarajiwa kuanza.

**(iii) Uendeshaji wa Zao la Tumbaku**

Kwa msimu **2023/2024** masoko yalifunguliwa tarehe 15 Mei, 2023. Mpaka kuishia tarehe 13/08/2023 jumla ya kilo **1,535,297.92** zenye thamani ya Dola **3,262,199.97.** Tumbaku iliyouzwa ni aina ya mvuke kilo **795,229.92**, Moshi **734,668.55** na hewa kilo **5,399.45. Masoko ya tumbaku yanaendelea**

### 2.2.6 Uendelezaji wa Miradi ya Kiuchumi ya Vyama Vya Ushirika

Serikali kupita vyama vya Ushirika imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi kama ifuatayo:

- Usimamizi wa uendelezaji wa ujenzi wa kiwanda cha vifungashio cha Chama Kikuu SONAMCU Ltd wilayani Namtumbo.
- Ukarabati wa maghala 5 kati ya 7 ya Chama Kikuu cha MBIFACU Ltd
- Ukarabati wa MBICU Hotel
- Usimamizi wa uendelezaji wa Mradi wa kiuchumi wa shamba la kahawa la Chama Kikuu cha MBIFACU Ltd
- Ujenzi wa Mradi wa shule ya Sekondari ya Mahenge AMCOS Ltd
- Ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao ya wakulima la chama cha Msingi Kimuli na Namitili (AMCOS)

**2.2.7. Mafanikio Katika Usimamizi wa Mazao**

i. Wakulima kupata bei nzuri ya mazao hususani mazao yanayouzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
ii. Kuwepo kwa ushirikiano nzuri kwa wadau wa stakabadhi ghalani kwa ngazi zote;
iii. Kuwepo kwa matumizi sahihi ya vipimo/ mizani, ambayo inasaidia mkulima asinyonywe
iv. Uamshaji wa Vyama vya Msingi sinzia ambavyo kwa sasa vinafanya kazi vizuri;

v. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.
vi. Uwekezaji unaofanywa na Vyama vya msingi katika ujenzi wa maghala, ununuzi wa magari ya kubebea mazao na ujenzi wa shule ya Sekondari na ujenzi wa kiwanda cha Vifungashio

### 2.2.8 Changamoto

i. Ukosefu wa mitaji ya ndani kwa vyama vya ushirika na kutegemea mikopo kutoka vyanzo vya nje
ii. Utoroshwaji wa mazao hasa zao la soya
iii. Kuwepo kwa migogoro mbalimbali kwa Vyama vya ushirika
iv. Uzalishaji mdogo wa mazao ya kimkakati

### 2.2.9 Hitimisho

Licha ya changamoto ndogondogo zinazokabili sekta ya Ushirika bado Ushirika umeendelea kuwa ni mkombozi kwa mwananchi, hivyo usimamizi wa sekta hii unaendelea kuimarishwa ili Ushirika uweze kusonga mbele kwa maendeleo ya wanachama wake.

## 2.3 Sekta ya Mifugo

Katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Mifugo Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuboresha huduma za ugani, uzalishaji wa mifugo, uendelezaji wa nyanda za malisho kwa mfumo wa ranchi ndogo, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, uboreshaji wa miundombinu ya mifugo, masoko ya mifugo pamoja na miundombinu ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

### 2.3.1 Hali ya Uzalishaji

Mkoa wa Ruvuma unakadiriwa kuwa mifugo **3,354,927** ikijumuisha ng’ombe **235,128**, Mbuzi **293,361**, Kondoo, Nguruwe **232,710,** Kuku, Bata, Punda, Mbwa na mifugo mingine midogo midogo. Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 uzalishaji wa mazao yatokanayo na Mifugo umefikia tani **2,733.02** za nyama ya ng’ombe, tani **374.31** za nyama ya mbuzi na kondoo, tani **1,905.66** za nyama ya nguruwe na tani **774.26** za nyama ya kuku. Uzalishaji wa maziwa umefikia lita **2,017,452.96** vipande vya ngozi za ng’ombe vilivyozalishwa ni **19.524** vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo ni **12,477.**

Mkoa una  viwanda viwili vya kusindika nyama katika Abbasia ya Peramiho na Chipole Sisters Halmashauri ya Wilaya ya Songea maarufu kwa usindikaji wa ***sausages*** za nyama wastani wa tani **100** za nyama kwa mwaka.

Kwa upande wa usindikaji wa Maziwa Mkoa  una wasindikaji wadogo **6** wanaosindika wastani wa lita **201,600** kwa mwaka. Aidha ,ili kuimarisha lishe kwa jamii wananchi wanaendelea kuhamasishwa kunywa maziwa ili kufikia lengo la unywaji wa lita **200** za maziwa kwa kila mtu kwa mwaka.

### 2.3.2 Utoaji wa Huduma za Mifugo

i. **Udhibiti wa Magonjwa**

Mkoa wa Ruvuma umeendelea na shughuli za udhibiti wa magonjwa ambapo kwa kipindi cha Mwezi Julai 2023 hadi Juni, 2024 magonjwa

yaliyojitokeza zaidi ni Ndigana kali, Ndigana baridi, Homa ya Mapafu kwa ng’ombe na mbuzi, ugonjwa wa Mapele ngozi, Kideri na homa ya matumbo kwa kuku na Ndui.

Mkoa umesimamia utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ili kukabiliana na magonjwa ya Mifugo, ambapo Ng'ombe **8,184** wamepatiwa chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu (CBPP), mbwa **14,351** na paka **45** wamepatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha Mbwa (Rabies), Kuku **365,648** dhidi ya Ugonjwa wa Kideri, ugonjwa wa Ndui na ugonjwa wa Gumboro.

Matokeo ya uogeshaji katika Mkoa wa Ruvuma ni kupungua kwa vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo.

**ii. Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF)**

Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe uliripotiwa Mwezi Juni 2023 katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga, Tunduru, Nyasa, Songea, Madaba, Mbinga Mji, na Manispaa ya Songea. Ugonjwa huu ulisababisha vifo vya Nguruwe zaidi ya **1,700**. Takwimu zinaonesha ugonjwa ulivyoenea kwa kasi na kupelekea madhara makubwa ya kiuchumi kwa wafugaji na wafanyabiashara ya nguruwe mkoani Ruvuma.

Mambo yanayosababisha ueneaji wa ugonjwa kutoka eneo moja hadi jingine ni pamoja na kuhamisha nguruwe hai kutoka eneo moja lililoathirika hadi eneo lingine lisiloathiriwa na ugonjwa, kupeana zawadi za nguruwe au nyama kutoka kwa ndugu wa eneo lilioathirika

na kupeleka eneo lingine lisiloathirika, kusafirisha nyama za nguruwe kutoka kwenye maeneo yaliyoathirika na ugonjwa, kusafirisha samadi ya nguruwe kutoka kwenye maeneo yaliyoathirika na ugonjwa.

Ili kukabiliana na ugonjwa huu hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwemo: -

- Kuitisha vikao vya wadau wa sekta ndogo ya nguruwe ambao ni wafanyabiashara ya nguruwe, wafugaji wa nguruwe, Wasafirishaji wa mabasi, Maafisa mifugo pamoja na viongozi ngazi ya Mkoa na Wilaya.
- Kuimarisha ukaguzi wa nguruwe wote wanaochinjwa kwa kuwakagua kabla ya kuchinja (Antemortem) na baada ya kuchinja (Postmortem) ili kuzuia kusambaza kwa ugonjwa kupitia machinjio.
- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu dalili za ugonjwa na hatua za kuchukua kuzuia kusambaa zaidi.
- Kuzuia usafirishaji wa nguruwe kwenye maeneo yaliyoathirika na kutumia sheria ndogo za Halmashauri kutoza faini kwa wadau wanaokiuka sheria ya magonjwa ya Mifugo hasa utaratibu wa kusafirisha nguruwe.
- Kuelimisha Maafisa Ugani juu ya namna ya kudhibiti ugonjwa pamoja na kuchukuwa tahadhari pale wanapotibu au kuhudumia mifugo pamoja na kuacha kutibu nguruwe wagonjwa.
- Halmashauri kuandaa vifaa (mabomba na dawa aina ya VIRD) na nguvu kazi ya kuangamiza mashamba yote yaliyoathirika kwa kushirikiana na chama cha wadau wa nguruwe.

- Kupulizia dawa aina ya VIRD kwenye mabanda yote yaliyoathirika
- Kufukia na kuchoma nguruwe wote waliopata ugonjwa na waliokufa ili kuzuia ueneaji wa virusi.

Hadi kufikia mwezi Julai, 2024 ugonjwa huu umedhibitiwa na hakuna maeneo yaliyoripoti uwepo wa ugonjwa huu.

### 2.3.3 Mashamba Darasa

**Mashamba Darasa ya Malisho**

Athari za kupungua kwa malisho zimeendelea kujitokeza mara kwa mara kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo, mabadiliko ya tabia ya nchi na mtazamo wa wafugaji kutegemea malisho ya asili tu. Athari hizo zimesababisha mifugo kudhoofika na wakati mwingine kufa kwa kukosa malisho na maji.

Katika jitihada za kukabiliana na athari hizo Wizara ilitoa fedha za kuanzisha mashamba darasa ya malisho **8** yenye jumla ya ukubwa wa ekari **40** katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Songea, Namtumbo na Tunduru. Lengo kuu la mpango huu ni kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha, kutunza na kuhifadhi mbegu na malisho kwa kutumia utaratibu wa mashamba darasa. Wafugaji walishiriki kikamilifu katika mpango huu kuanzia hatua maandalizi ya shamba kulima na kuhudumia mashamba hayo. Mashamba haya yalishavunwa.

### 2.3.4 Fursa Zilizopo

Kutokana na mifugo iliyopo na mazao yake zinafungua fursa zifuatazo za kiuchumi:

- Ufugaji wa ng’ombe wa maziwa na uzalishaji wa mitamba;
- Usindikaji wa mazao ya mifugo;
- Ujenzi wa viwanda vya vyakula vya mifugo, na mashamba ya malisho; na
- Uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa nyama na mayai.

### 2.3.5 Changamoto

- Kukosekana kwa mitamba bora ya ng’ombe wa maziwa;
- Ukosefu wa malisho na viwanda vya kusindika mazao;
- Changamoto ya magonjwa ya mifugo.

### 2.3.6 Mapendekezo/Mikakati ya Utatuzi wa Changamoto

- Kuhimiza matumizi ya kinga zaidi kuliko tiba kwa mifugo;
- Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo;
- Kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wenye tija; na
- Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya mifugo.

## 2.4 Sekta ya Uvuvi.

### 2.4.1 Utangulizi

Katika sekta ya uvuvi, Mkoa unategemea kupata mazao ya uvuvi kutoka ziwa Nyasa, mito na mabwawa ya kufugia samaki. Hata hivyo tija itokanayo na vyanzo hivyo vya samaki haitoshelezi mahitaji ya Mkoa ambayo ni zaidi ya tani**18, 000** kwa mwaka hivyo kupata samaki kutoka nje ya Mkoa kwa wastani wa Tani **55** kwa mwezi. Uzalishaji wa samaki wa kufuga ni wastani wa tani **121.20** kwa mwaka. Watalaam wanaendelea kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ili kukidhi mahitaji ya walaji. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka **2019** hadi Septemba **2023** jumla ya wavuvi **7,635** walisajiliwa ikiwa ni pamoja na vikundi **38** vya wavuvi na vikundi **4** vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi **(BMUs**) vilivyopo mwambao wa Ziwa Nyasa. Uzalishaji wa samaki katika Ziwa Nyasa na mito ni wastani wa tani **480** kwa mwaka zenye thamani ya **Tshs. 2,400,000,000.00**. Aina ya samaki wanaovuliwa katika Ziwa Nyasa na Mito ni pamoja na Mbufu, Mbelele, Mbasa, Kambale, Vitui, Perege, Ningu, Mchali pamoja na Dagaa.

### 2.4.2 Idadi ya Maafisa Uvuvi.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Watalaam wa uvuvi **17** ambapo katika ngazi ya Mkoa ni mmoja (**1**) na kumi na sita (**16**) wako katika ngazi za Halmashauri.

**Jedwali Na. 5: Wataalam wa Sekta Uvuvi Mkoa wa Ruvuma**

| | Wanaohitajika | Waliopo | Mapungufu | Waliopo kwenye mpango wa kuajiriwa 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|
| RS | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Tunduru DC | 12 | 2 | 10 | 4 |
| Namtumbo DC | 21 | 2 | 19 | 8 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mbinga DC | 31 | 3 | 28 | 6 |
| Nyasa DC | 22 | 4 | 18 | 10 |
| Songea DC | 18 | 0 | 18 | 14 |
| Madaba DC | 9 | 3 | 6 | 2 |
| Songea MC | 5 | 2 | 3 | 3 |
| Mbinga TC | 14 | 0 | 14 | 2 |
| **Jumla** | **133** | **17** | **116** | **49** |

### 2.4.3 Uzalishaji wa Samaki Katika Mabwawa.

Mkoa una wafugaji wa samaki **4,159** wenye jumla ya mabwawa **6,582** **y**enye wastani wa uzalishaji wa tani **121.20** kwa mwaka. Ufugaji wa samaki ni shughuli ambayo wananchi wengi wamekuwa wakiifanya katika kuongeza kipato na lishe katika jamii inayowazunguka.

Kutokana na kutotosheleza kwa vyanzo vya samaki vilivyopo kwenye Mkoa, wananchi kuhamasishwa kufuga samaki kwa tija katika mabwawa ili kuweza kukidhi mahitaji hayo kwa ajili ya chakula na kwa biashara pia. Ndani ya Mkoa kuna kituo kimoja **(1)** cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki chenye uwezo wa kuzalisha vifaranga **3,000,000** kwa Mwaka,kituo hicho kipo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Ruhila (**RADC)** kilichopo Manispaa ya Songea.

### 2.4.4 Fursa zilizopo katika ufugaji wa samaki.

- Mwamko wa wananchi wa Mkoa kuhamasika na ufugaji wa samaki;
- Uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo,mito, chemchem na mabwawa ya Asili/Malambo zaidi ya kumi na nne (**14**) katika Mkoa yenye fursa ya ufugaji kwa kupandikiza au kufuga kwa njia ya vizimba (Cage culture);

- Uwepo wa ziwa Nyasa linalofaa kwa ufugaji wa njia ya vizimba (cage culture);
- Uwepo wa mahitaji makubwa ya samaki katika Mkoa na soko la uhakika.
- Uwepo wa wafugaji wa samaki zaidi ya **4,159** na mabwawa ya samaki zaidi ya **6,582;** na
- Upatikaniji wa uhakika wa malighafi za kutengenezea chakula cha samaki.

**Jedwali Na. 6: Idadi ya mabwawa, wafugaji na wastani wa hali ya uzalishaji wa samaki katika mabwawa kwa mwaka.**

| Halmashauri | Idadi ya wafugaji | Idadi ya mabwawa | Uzalishaji (tani) |
|---|---|---|---|
| Tunduru DC | 315 | 463 | 3.90 |
| Namtumbo DC | 200 | 71 | 1.3 |
| Songea MC | 955 | 937 | 7.1 |
| Mbinga DC | 951 | 1,293 | 8.4 |
| Songea DC | 1,327 | 3,227 | 96.8 |
| Nyasa DC | 168 | 225 | 1.4 |
| Mbinga TC | 215 | 310 | 1.2 |
| Madaba DC | 28 | 56 | 1.1 |
| **JUMLA** | **4,159** | **6,582** | **121.20** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa.***

### 2.4.5 Matumizi ya zana bora za uvuvi.

Katika matumizi ya zana bora za uvuvi, jitihada zimewekwa ili kujenga uwezo wa wananchi kutambua madhara yatokanayo na matumizi ya zana haramu za uvuvi , utoaji wa elimu juu ya matumizi bora ya zana za kisasa za uvuvi zinazokubalika kisheria, kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuhamasisha ufugaji bora wa kisasa na wenye tija. Pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi wa

rasilimali za uvuvi (**Beach Management Units -** BMUs) doria mbalimbali hufanyika hasa katika mwambao wa ziwa Nyasa na Mto Ruvuma kwa kushirikiana na vikundi vya **BMUs** ili rasilimali za uvuvi zitunzwe, zilindwe na ziwe endelevu,na mpaka kufikia Juni **2024** wavuvi **5,488** walisajiliwa na leseni **2,670** za Uvuvi zilitolewa.

### 2.4.6 Hali ya Miundombinu ya Uvuvi.

Ujenzi wa karakana ya kuunda boti za uvuvi za kisasa katika kituo cha Mbamba bay umefikia hatua za mwisho za kuweka mashine, pia soko la samaki la Mbamba bay bado halijaanza kutumika kutokana na kutokukamilika kwa miundombinu ya maji na choo ingawa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia **98.** Aidha, ujenzi wa Mwalo wa kisasa wa Kijiji cha Ng'ombo umeanza mwaka wa fedha **2023/2024.** Mwaka **2019** Halmashauri ya Nyasa ilipata fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 200** kwa ajili ya mradi wa utengenezaji wa boti za uvuvi za kisasa, na mpaka kufikia Juni **2024** boti **2** zimeshakamilika na zinafanya kazi, boti **4** bado hazijakamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha **2023/2024** Halmashauri ya Nyasa imepokea fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 300** kwa ajili ya utengenezaji wa Boti ya doria ya kisasa. Katika mwaka wa fedha wa **2022/2023** Halmashauri Songea ilipokea fedha kiasi cha **Tshs.Milioni 123** kwa ajili ya ujenzi wa shamba darasa moja la ufugaji bora wa Samaki. Kituo hiki kimekamilika na kinafanya kazi.

### 2.4.7 Mikakati ya kuendeleza sekta ya uvuvi.

- Kuhimiza matumizi ya zana bora za uvuvi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ambapo hadi kufikia Disemba **2023** zaidi ya wavuvi

**5,488,** wafugaji **4,159** na wadau **470** wamefundishwa njia bora za uvuvi,ufugaji bora wa samaki na utunzaji wa mazingira.

- Kuendeleza/kuboresha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi hasa mialo(**Land stations**), na katika mwaka huu wa fedha **2023/2024** Wizara ya Mifugo na Uvuvi(sekta ya uvuvi) ina mpango wa kujenga mualo **1** katika kijiji cha Ng'ombo**.**
- Kutoa elimu endelevu ya uanzishaji wa vikundi vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi(**BMUs**) katika mwambao wa ziwa Nyasa.
- Kuhimiza uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki, ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba (***cage*)** katika ziwa na mabwawa ya asili ili kupata mavuno mengi ya samaki yatakayofaa kwa ajili ya viwanda.
- Kukijengea uwezo kituo cha maendeleo ya ufugaji samaki Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga bora na vya kutosha, kwa sasa kituo kina uwezo wa kuzalisha vifaranga **3,000,000** kwa mwaka ukilinganisha na mahitaji ya vifaranga **5,000,000** kwa mwaka kwa Mkoa mzima.
- Kila Halmashauri kuwa na kituo cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki ambapo vituo hivyo vitatumika pia kama mashamba darasa.
- Kuendeleza doria za mara kwa mara ili kuzuia utumiaji na uingizaji wa zana haramu za uvuvi katika ziwa na mito pamoja na kuvikagua vyombo vyote na kuvisajili kisheria.

- Ujenzi wa soko la samaki lililopo Mbamba bay upo katika hatua za mwisho ili liweze kutumika.

### 2.4.8 Changamoto.

- Uvuvi wa kutumia miti yenye sumu **(Mtupa**) bado ni tatizo katika baadhi ya maeneo ya mito ya Ruhuhu, Ruhekei na Mbawa katika Wilaya ya Nyasa;
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya kufanya doria za mara kwa mara;
- Uhaba wa watumishi wa kada ya uvuvi katika Mkoa wa Ruvuma hususani mwambao wa ziwa Nyasa, hali hiyo inadhoofisha shughuli za Uvuvi na hasa Ukusanyaji wa Takwimu na maduhuli ya Serikali
- Kusuasua kwa uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika Halmashauri za wilaya.
- Uchache wa vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (**BMUs**), mpaka sasa kuna BMUs **4** tu kati ya **24** zinazohitajika kwa mwambao mzima.
- Ushiriki mdogo wa ulinzi shirikishi wa rasilimali za Uvuvi kwa wadau mbalimbali;
- Katika kipindi cha mwaka **2020** hadi **2023,** zana haramu za Uvuvi aina ya timba (***monofilament***) pamoja na makokolo zenye urefu wa zaidi ya mita **8,000** na thamani ya zaidi ya shilingi **57,000,000/=**zilikamatwa na kikosi cha kulinda rasilimali za Uvuvi (**FRP)** kwa kushirikiana na Halmashauri.

### 2.4.9 Mapendekezo ya kutatua changamoto.

i. Mkoa unaendelea kuomba kuajiri watumishi wapya hususani Halmashauri ya Nyasa ambayo ina mahitaji makubwa ya watumishi wa kada ya uvuvi;
ii. Kuwahusisha wadau wote katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi hasa jamii ya wavuvi wenyewe ili rasilimali za uvuvi ziwe endelevu kwa kizazi kijacho;
iii. Mkoa unaendelea kufanya doria za mara kwa mara katika mito ili kukomesha uvuvi haramu wa kutumia miti ya sumu;
iv. Kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika kila Halmashauri ya wilaya ili kukidhi mahitaji ya wafugaji; na
v. Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki (**floating pellets)** ili viweze kuwasaidia wafugaji wa samaki kwenye vizimba.

## 2.5 Sekta ya Maliasili na Utalii

### 2.5.1 Misitu

Mkoa umekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii juu ya upandaji miti na utunzaji mazingira. Uhamasishaji huu huenda sambamba na utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti ambao hufanyika kila mwaka kwenye Halmashauri zote.

Mkoa wa Ruvuma una lengo la kupanda miti kibiashara ekari 100,000 kwa muda wa miaka kumi (10) toka 2015 – 2025.Mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya Serikali, vyuo na shule.

Kwa msimu wa mwaka 2023/24 Mkoa wa Ruvuma umepanda jumla ya miche ya miti **4,099,014** ambapo imepandwa katika Halmashauri zote, miti hii ni kwa ajili ya mbao, vyanzo vya maji na matunda. Jedwali namba **13** hapo chini linaonyesha uzalishaji wa miche ya miti iliyopandwa kwa msimu huu wa mvua 2023/24.

**Jedwali Na. 7: Idadi ya miche ya miti Mkoa wa Ruvuma Mwaka - 2024**

| | | IDADI YA MICHE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Bustani (nursery)** | **Mbao** | **Vyanzo vya maji** | **Matunda** | **Jumla** |
| Songea | Matogoro TFS | 120,000 | 5,000 | 10,000 | 135,000 |
| | Mahenge | 100,000 | 20,000 | 35,000 | 155,000 |
| | AVIV FARM | | 31,000 | | 31;000 |
| | Bombambili | 70,000 | 10,000 | 200 | 80,200 |
| Namtumbo | | 57964 | 14400 | 3572 | 75,936 |
| Mbinga DC | | 177,673 | 38,180 | 620 | 216,473 |
| Mbinga Mji | | 1,081,969 | 16,100 | 162,130 | 1,260,199 |
| Nyasa | | 152,500 | 1,060 | 9,846 | 163,406 |
| Madaba | | 100,000 | 30,000 | 300 | 130,300 |
| Wino TFS | | 1,000,000 | | | 1,000,000 |
| Tunduru | | 150,000 | 2000 | 700,000 | 852,000 |
| **Jumla** | | **3,009,606** | **167,740** | **921,668** | **4,099,014** |

### 2.5.2 Hali ya ufugaji Nyuki kimkoa

Hadi sasa Mkoa una jumla ya mizinga **16,378** ambapo mizinga ya kisasa ni **10,883** na mizinga ya kienyeji ni **5,495**.

**Jedwali Na. 8: Idadi ya mizinga ya nyuki**

| S/N | WILAYA | IDADI YA MIZINGA | | | UZALISHAJI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KISASA | KIENYEJI | JUMLA | ASALI - kg | NTA |
| 1 | Nyasa | 1473 | 361 | 1,834 | 1986 | 65 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Mbinga | 3712 | 1231 | 4,943 | 7850 | 0 |
| 3 | Songea | 3492 | 523 | 4,015 | 8100 | 0 |
| 4 | Namtumbo | 1387 | 2675 | 4,062 | 209 | 0 |
| 5 | Tunduru | 819 | 705 | 1,524 | 3300 | 92 |
| | **Jumla** | **10,883** | **5,495** | **16378** | **21,445** | **157** |

Uzalishaji wa asali katika Mkoa wa Ruvuma unakumbwa na baadhi ya changamoto hadi kupelekea kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki. Changamoto hizo ni kama zifuatazo;

i. Wafugaji nyuki wengi hawana utaalamu wa ufugaji nyuki wa kibiashara.
ii. Moto wa msituni ambao hutokea mara kwa mara hasa hasa kwenye miombo
iii. Ukosefu wa masoko ya uhakika unapelekea wafugaji nyuki kutothamini ufugaji nyuki.

## 2.6. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma

### 2.6.1 Utangulizi

Mkoa wa Ruvuma unakadiriwa kuwa na jumla ya hekta 197,108.2 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kati hizo hekta 7,388.3 zimeendelezwa, hii ni sawa na asimilia **3.7**. Pia Mkoa wa Ruvuma una fursa ya kupata mvua nyingi zinazowezesha upatikanaji wa maji ya kutosha wakati wote, ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo na inayokubali kuzalisha mazao aina zote. Katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma una jumla ya skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa, uzalishaji wake unakadiriwa kuwa kati ya tani 2.8 - 5 za mpunga kwa ekari.

### 2.6.2 Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi

#### i. Usajili wa Skimu

Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kusajili jumla ya skimu 63 kati ya skimu 102, kati ya hizo skimu 10 zimesajiliwa kipindi cha mwaka 2023/2024 ili kuendana na sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4, 2013 na kanuni ya mwaka 2015 iliyopitishwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa katika mwaka 2024/2025 imejipanga kukamilisha zoezi la usajili wa skimu 49 zilizobaki ili serikali iweze kuendelea na zoezi la kuelekeza fedha katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa skimu zilizoathiriwa na mafuriko katika vipindi vya miaka mitatu mfululizo 2019-2021. Lifuatalo ni jedwali linaloonesha skimu zinazofanya kazi.

**Jedwali Na. 9: Skimu zinazofanya kazi.**

| S/N | HALMASHAURI | JINA LA SKIMU | ENEO LINALOFAA KWA UMWAGILIAJI(HA) | ENEO LINALOMWAGILIWA(HA) |
|---|---|---|---|---|
| i. | Tunduru | Kitanda | 600 | 100 |
| | | Lekindo | 150 | 25 |
| | | Madaba | 200 | 100 |
| | | Legezamwendo | 220 | 200 |
| | | Misyaje | 200 | 175 |
| | | Naikula | 250 | 200 |
| | | Madaba | 600 | 350 |
| ii. | Nyasa | Kimbande | 260 | 237 |
| | | Ngindo | 250 | 141 |
| | | Ngingangama | 40 | 10 |
| | | Nyomboka | 520 | 160 |
| | | Kwambe | 200 | 100 |
| | | Nkalachi | 150 | 100 |
| | | Kimbande | 200 | 150 |
| iii. | Songea DC | Namatuhi | 220 | 100 |
| | | Mpitimbi B | 200 | 88 |
| | | Njoka | 120 | 33 |
| | | Muhukuru | 48 | 48 |
| | | Nakahuga | 270 | 96 |
| | | Ndongosi | 200 | 135 |
| iv. | Mbinga DC | Litumbandyosi | 250 | 82 |
| | | Sangamabuni | 300 | 70 |
| | | SangaLuhagara | 150 | 65 |
| v. | Namtumbo | Msanjesi | 100 | 45 |
| | | Amani | 90 | 70 |
| | | Njomlole | 120 | 62 |
| | | Namahoka | 150 | 30 |
| | | Kitanda | 100 | 60 |
| | | Mchomoro | 60 | 60 |
| | | Luhimbalilo | 50 | 20 |
| | | Nambecha | 40 | 20 |
| | | Mtakuja | 300 | 300 |
| | | Mwangaza | 250 | 250 |
| | | Nambecha | 40 | 40 |
| | | Liyuni | 140 | 100 |
| | | Likuyuseka | 44 | 25 |

| S/N | HALMASHAURI | JINA LA SKIMU | ENEO LINALOFAA KWA UMWAGILIAJI(HA) | ENEO LINALOMWAGILIWA(HA) |
|---|---|---|---|---|
| | | Mtonya | 75 | 75 |
| vi. | Madaba | Hangangadinda | 400 | 55 |
| | | Mbangamawe | 250 | 50 |
| | | Luhimba | 55 | 25 |
| **JUMLA ya skimu** | | **42** | | |

### ii. Skimu zilizohuishwa utendaji kazi

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma ikishirikiana na wilaya imefanikiwa kuhuisha skimu mbalimbali za umwagiliaji zilizokuwa hazifanyi kazi mfano ni:

- Nyomboka iliyopo wilaya ya Nyasa
- Mpitimbi B wilaya ya Songea
- Muhukuru Wilaya ya Songea
- Ndongosi Wilaya ya Songea

### iii. Ada ya huduma ya umwagiliaji na tozo ya urejeshaji wa gharama za uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji.

Katika kila skimu ya umwagiliaji kila mkulima anayemiliki eneo ndani ya skimu anawajibika kutoa ada ya huduma za umwagiliaji ambayo ni asilimia tano (5%) ya wastani wa uzalishaji kwa ekari kwa msimu.

Aidha, wamwagiliaji wana wajibu wa kurejesha gharama za uwekezaji wa ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ambayo serikali imewekeza ili kuendelea kupanua eneo la umwagiliaji katika maeneo

mengine yenye uhitaji. Hivyo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutoa elimu kwa wakulima wa mwagiliaji.

**iv. Ukusanyaji, Usimamizi na Matumizi ya Fedha za Ada na Tozo**

Ofisi ya umwagiliaji Mkoa ikishirikiana na ofisi za umwagiliaji Wilaya zimefanikiwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyama na wakulima katika skimu zaidi ya 63 kuhusu Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, ukusanyaji wa ada mbalimbali, usimamizi na matumizi ya fedha za ada hizo, zoezi hili bado ni endelevu, ili kupata matokeo chanya unahitajika ushirikiano kwa Maafisa kilimo wa Wilaya na wale waliopo katika maeneo ambayo skimu za umwagiliaji zipo na zinaendelea kuboreshwa.

Kwa mujibu wa aya ya 84 (3) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), na kanuni ya marekebisho ya Kanuni ya mwaka 2021, Ada ya 5% ya Huduma ya Umwagiliaji zitalipwa na wakulima pia zitahifadhiwa katika akaunti maalumu ya skimu. Kuanzia Juni 2023 mpaka Juni 2024. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanikiwa kukusanya ada ya huduma ya umwagiliaji na ada ya mwaka kwa skimu 17, ada hizi zitaongeza nguvu kwenye kazi ya ukarabati wa skimu nne zenye changamoto (Subira, Msanjesi, Nyomboka na Misyaje) pia.

**v. Taarifa ya miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kwa bajeti 2023/24.**

**Jedwali Na. 10: Skimu ya umwagiliaji inayoendelea na ukarabati kwa mwaka 2023/24**

| Wilaya | Jina la skimu | Eneo (Ha) | Hatua za Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| Songea | Muhukuru | 48 | • Thamani ya Mradi: **722,496,890/=**<br>• Mkandarasi: MS MUUNGANO GENERAL INTERPRISES JV MS SAMA CONSTRUCTION<br>• Kazi imefikia 74% |

**Jedwali Na. 11: Miradi iliyokamilika kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ipo kwenye hatua za kimamunuzi**

| Wilaya | Jina la Skimu | Eneo (Ha) |
|---|---|---|
| Nyasa | Kimbande | 750 |
| | Lundo | 1160 |
| | Chiulu | 570 |
| | Kwambe | 200 |
| Tunduru | Nambalapi(Mkandarasi ameshapatikana) | 600 |
| | Mkotamo | 200 |
| Mbinga | Mkungwe | 130 |

**Jedwali Na. 12: Miradi ya ukarabati iliyopo katika hatua za manunuzi**

| Wilaya | Jina la Skimu | Eneo (Ha) |
|---|---|---|
| Songea | Subira | 300 |
| Namtumbo | Msanjesi | 150 |
| Nyasa | Nyomboka | 520 |
| Tunduru | Misyaje | 980 |

**Mabonde ya kimkakati yanayoendelea upembuzi yakinifu na usanifu**

Mkoa wa Ruvuma una mabonde matatu ya kimkakati ambayo yameingia katika hatua ya utekelezaji kutokana na bajeti ya mwaka

2023-2024 ambayo ni Ruvuma, Lityumbandyosi na Ruhuhu ambapo kazi inayoendelea ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**Jedwali Na. 13: Mabonde ya kimkakati yanayoendelea na upembuzi yakinifu na usanifu**

| Mkoa | Jina la Bonde | Skimu zilizotembelewa | Tarehe walizoripoti | Hatua za Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| Ruvuma | Litumbandyosi-Mbinga DC | 1.Sanga mabuni<br>2.Litumbandyosi<br>3.Sanga luhagara | 18/10/2023 | 1. Mshauri Elekezi: **Saba Engineering PLC**<br><br>2. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la Litumbandyosi, umekamilika ripoti imeshatumwa makao makuu. |
| Ruvuma | Bonde la mto Ruvuma | 1.Subira<br>2.Kihekwa<br>3.Seed farm (Luhila-kuchile)<br>4.Luwawasi<br>5.Nambendo<br>6.Nasya<br>7.Mkotamo | 13/05/2024 | 1.Mshauri Elekezi:**Continental JV Multtech JV Netwas**<br><br>2. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la mto Ruvuma unaendelea, kazi zilizofanyika mpaka sasa ni kutembelea maeneo kukusanya taarifa za awali na darft inception ripoti ya kwanza imeshatoka kwa ajili ya mapitio. |
| Ruvuma | Bonde la mto Ruhuhu | | | Kazi haijaanza tunamsuburi Mshauru elekezi wa kazi hii. |

### Vi. Uchimbaji wa Visima

Kazi ya kutambua maeneo ya kuchimba visima ilifanyika na halmashauri za wilaya kwa kufuatia maelezo kutoka makao makuu ya

Tume. Zoezi la kukusanya taarifa za awali/coordinates lilianza rasmi tarehe 07/05/2024 kazi hii inatekelezwa na wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji waliopo Mkoani na wilayani. Zoezi hili limeshafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Manispaa ya Songea, Madaba na Mbinga. Zoezi la kuchukua coordinate linaendelea katika wilaya ya Namtumbo na Tunduru. Maeneo ambayo tayari zoezi la kuchukua coordinates limefanyika yameoneshwa katika jedwali Na. 20.

**Jedwali Na. 14: Maeneo Ambayo Tayari Zoezi la Kuchukua Coordinates Limefanyika**

| S/N | Wilaya | Kijiji |
|---|---|---|
| 1 | Songea MC | Mletele |
| | | Tanga |
| | | Kihekwa |
| | | Lizaboni |
| | | Mwanamonga |
| 2 | Songea DC | Mdunduhalo |
| | | Matimira |
| | | Namatuhi |
| | | Liganga |
| 3 | Mbinga DC | Sanga mabuni |
| | | Sanga Luhagara |
| | | Amani makolo |
| | | Kiwombi |
| | | Mkako |
| 4 | Mbinga Mjini | Utiri |
| | | Kitanda |
| | | Mkwaya |
| 5 | Madaba | Matetereka |
| | | Mahanje |
| | | Kipingo |
| | | Ndelenyuma |
| | | Mtyangimbole |

### 2.6.3 Changamoto

**Ulipaji wa ada ya huduma ya umwagiliaji**

Katika zoezi la ukusanyaji wa ada za mwaka na ada ya huduma ya umwagiliaji Tume inakutana na changamoto ya wananchi kuwa na ari ndogo na wengine kukataa kabisa kulipa ada hizi. Licha ya kwamba vyama hivyo kusajiliwa kwa mujibu wa sheria na vingine kujengewa miundombinu na kupewa elimu kuhusu ada za huduma za umwagiliaji na ada za mwaka.

### 2.6.4 Utatuzi

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa ada hizo kwa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji na uboreshaji wa miundombinu.

### 2.6.5 Hitimisho

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na wadau wengine wa maendeleo ili kuleta tija kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sababu ndio kilimo chenye uhakika.

## 2.7 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)

### 2.7.1 Utangulizi

Kanda ya Songea ni miongoni mwa Kanda nane (8) za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa inayotegemewa kwa kilimo na uzalishaji wa zao la mahindi. Kanda hii inahudumia mkoa mmoja tu wa Ruvuma. Pale uhitaji wa chakula unapokuwa mkubwa katika maeneo mengine ya

nchi, Afisa Mtendaji Mkuu anaweza kuelekeza chakula kilichohifadhiwa katika maghala yaliyopo Songea kupelekwa kwenye maeneo mengine nje ya mkoa wa Ruvuma ili kuweza kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo.

Katika mazoezi ya ununuzi, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), hutumia njia mbalimbali za ununuzi ambazo ni pamoja na:

i. Kutumia vituo vya ununuzi ambavyo vipo katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya
ii. Kutumia vikundi vya Wakulima/SACCOS na
iii. Kutumia mawakala/Wafanyabiashara ambao NFRA huingia nao mikataba

### 2.7.2 Utekelezaji wa kazi mbalimbali zilizopangwa kwa mwaka wa Fedha 2023/2024

#### i) Ununuzi wa tani 36,405 za mahindi

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, kanda ya Songea ilikuwa imepangiwa kununua jumla ya tani 28,000 za mahindi. Aidha, kutokana na upatikanaji mkubwa wa nafaka ya mahindi na kuhuishwa kwa mpango wa biashara wa Wakala (NFRA), Kanda ya Songea iliongezewa mgao wa ununuzi na kufikia tani 36,405 za mahindi.

Pamoja na kufikia lengo lililowekwa bado ilionekana kuna nafaka ya kutosha kwa wanachi wa mkoa wa Ruvuma, NFRA imeendesha zoezi la ununuzi kwa awamu mbili tofauti ambazo ni kuanzia Julai hadi septemba na Disemba hadi Mei, 2024. Ununuzi wa awamu ya pili katika mwaka wa fedha 2023/2024 ulifanyika baada ya ununuzi wa

awamu ya kwanza kusimama mnamo tarehe 08/09/2023 kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha za kuendelea kuwalipa wananchi waliokuwa wameshauza nafaka yao kwa NFRA.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024, Kanda ya Songea ilikuwa imeshanunua jumla ya tani **79,054.142** sawa na asilimia **217.2** ya lengo la kununua tani 36,405. Kiasi hiki cha mahindi kilichokwishanunuliwa kinakadiriwa kuwa na thamani ya shilingi **60,677,444,100/=**.

**Jedwali Na. 15: Mchanganuo wa kiasi kilichonunuliwa kwa kila kituo kilichotumika hadi tarehe 30 Disemba, 2023**

| NA | Jina la Kituo | Kiasi Kilichonunuliwa (Tani) |
|---|---|---|
| 1 | Mgazini | 3,831.317 |
| 2 | Ruhuwiko | 2,925.041 |
| 3 | Ruhuwiko (Wakala) | 39,816.174 |
| 4 | Namabengo | 1,739.330 |
| 5 | Tingi | 10.590 |
| 6 | Mpitimbi | 2,574.283 |
| 7 | Magagura | 5,971.346 |
| 8 | Muungano zomba | 1,537.746 |
| 9 | Kizuka | 2,774.888 |
| 10 | Nakahuga | 821.466 |
| 11 | Madaba | 1,046.707 |
| 12 | Mtyangimbole | 1,865.350 |
| 13 | Mwanamonga | 1,220.325 |
| 14 | Kindimba juu/chini | 334.222 |
| 15 | Mpepai | 207.210 |
| 16 | Mbinga mjini | 649.722 |
| 17 | Matiri | 577.453 |
| 18 | Kigonsera | 5867.335 |
| 19 | Namtumbo | 1,250.803 |
| 20 | Kitanda | 857.180 |
| 21 | Hanga | 1,415.506 |
| 22 | Vikundi vya wakulima / SACCOS | 965.504 |
| 23 | Changarawe | 794.702 |
| **JUMLA** | | **79,054.142** |

- Nafaka hizi zote zilinunuliwa kwa bei tofauti za kati ya shilingi 540/= Kwa kilo na shilingi 840/= kwa kilo.
- Mabadiliko ya bei yalifanyika katika nyakati tofauti tofauti kwa kuzingatia upatikanaji wa nafaka na mwitikio wa wakulima na wafanyabiashara katika vituo mbalimbali vya ununuzi.

**ii) Uhifadhi wa Chakula**

Kama ilivyoelezwa awali, jukumu kuu la NFRA ni kuhakikisha usalama wa Chakula nchini unakuwepo. Hivyo, kwa mwaka mzima wa fedha, NFRA Kanda ya Songea imefanikiwa kuhifadhi jumla ya tani **79,539.532** na kuendelea kuwa moja ya Kanda ambazo zina hifadhi kubwa ya chakula kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali yasiyotabirika ya chakula.

**iii) Kuhamisha tani 5000 za mahindi kwenda Kanda ya Arusha**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, moja ya kazi ambazo kanda ya Songea ilikuwa imepangiwa ilikuwa ni kuhamisha tani **5000** za nafaka ya mahindi kwenda Kanda ya Arusha. Aidha, kutokana na gharama kubwa za uhamishaji na upatikanaji wa raslimali fedha, kazi hii haikuweza kutekelezwa.

### 2.7.3 Mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa kanda ya Songea

Mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi Chakula kwa Kanda ya Songea unalenga kuongeza uwezo kwa tani **55,000**. Mradi huu unahusisha ujenzi wa vihenge 12 na maghala 2.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, mradi huu ulikuwa umefikia wastani wa asilimia **54.07** ya utekelezaji, ambapo kwa upande wa vihenge mradi ulikuwa umefikia asilimia **86.22**.

Aidha, mradi huu una zaidi ya miaka miwili ukiwa umesimama kutokana na Mkandarasi kuondoka kwenye eneo la mradi toka kipindi cha mlipuko wa COVID 19.

Kusimama kwa mradi huu kumeifanya kanda ya Songea kutofikia kwa wakati lengo lake la kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kama ilivyopangwa.

### 2.7.4 Changamoto

i. Baadhi ya wakulima/ wafanyabiashara kuleta vituoni nafaka ambazo hazikidhi viwango vya ubora.
ii. Baadhi ya wakulima kutokuwa na elimu ya teknolojia bora za uvunaji.
iii. Ufinyu wa bajeti ya fedha za kununulia nafaka iliyosababisha baadhi ya malipo kuchelewa kufanyika
iv. Uchache wa miundombinu ya kuhifadhia nafaka katika mkoa wa Ruvuma ambayo NFRA inaweza kukodi na kuitumia kuhifadhia nafaka inayonunuliwa ukilinganisha na ziada ya chakula katika mkoa wa Ruvuma.
v. Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi wa wakala (NFRA) ambako kumesababisha Kanda kuendelea kukosa miundombinu ya hifadhi ya kisasa yenye uwezo wa tani 55,000 zilizopangwa kuongezwa katika mradi wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi.

### 2.7.5 Mikakati ya kutatua Changamoto

i. Kanda imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu teknolojia bora za uvunaji kwa kupitia redio
ii. NFRA imeendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha kama mikopo kutoka benki za biashara ili kuwezesha kupata fedha za kununulia nafaka kutoka kwa wadau mbalimbali.
iii. NFRA imeendelea kuhamasisha wananchi wenye uwezo wa kujenga miundombinu ya kuhifadhia kujenga kwa ajili ya matumizi ya wadau mbalimbali wa hifadhi ya nafaka
iv. Wakala umepata Mkandarasi mwingine wa kumalizia kazi zilizobaki na tayari ameshapita kwenye eneo la mradi kwa ajili ya ukaguzi wa kazi zilizokwishafanyika na zilizobaki kabla ya kuanza kukamilisha kazi.

## 2.8 Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

### 2.8.1 Viwanda

Mkoa wa Ruvuma una viwanda vikubwa 6 ambavyo vitatu (3) ni vya kukoboa kahawa (Coffee Curing) katika Wilaya ya Mbinga, kiwanda kimoja (1) kipo katika Wilaya ya Tunduru cha kubangua korosho, Kimoja (1) kipo Wilaya ya Songea cha Kufua Umeme na kimoja (1) kipo Wilaya ya Songea cha Kusindika Sembe. Mkoa pia una viwanda vya kati ishirini na tano (25) vinavyojishughulisha na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo kama unga wa sembe, mchele, Mikate na Maziwa.

Aidha Mkoa wa Ruvuma una Viwanda vidogo 190 na viwanda vidogo sana vipo 3,264 ambavyo ni viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka mbalimbali, kukamua mafuta ya alizeti, usindikaji wa Mihogo, Chereheni, usindikaji wa nyama (sausages), sembe, juice, useremala na bidhaa nyingine za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili na huchangia ajira kwa wakazi wengi wa Mkoa wa Ruvuma. Bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo huuzwa ndani ya Mkoa na kiwango kingine huuzwa mikoa ya jirani kama vile Mbeya, Lindi, Mtwara, Njombe, Dar es Salaam na Mikoa mengine katika nchi yetu na nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

### 2.8.2 Biashara

#### 2.8.2.1 Utoaji wa Leseni za Biashara

Mkoa unaendelea na zoezi la kurasimisha Biashara na kutoa Leseni kwa kuzingatia Sheria na kanuni za utoaji wa Leseni za Biashara kama Serikali ilivyoagiza. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 jumla ya Leseni **8,370** zilitolewa na jumla ya **TShs. 783,926,622.00** zilikusanywa ikiwa ni mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa Leseni za Biashara katika Mkoa wa Ruvuma.

**Jedwali Na. 16: Muhtasari wa malengo ya utekelezaji wa Utoaji wa Leseni za Biashara kwa kipindi cha Julai, 2023 – Juni, 2024**

| Na | Jina la Halmashauri | Lengo kwa mwaka 2023/2024 | | Utekelezaji kwa kipindi cha Julai - Juni 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Leseni (idadi) | Mkusanyo (Tshs.) | Leseni (idadi) | Mkusanyo (Tshs.) |
| 1 | NAMTUMBO DC | 1,000 | 59,570,000.00 | 817 | 58,280,000.00 |
| 2 | MADABA DC | 1,600 | 34,000,000 | 351 | 26,500,000.00 |
| 3 | TUNDURU DC | 2200 | 130,000,000 | 1,173 | 98,110,000.00 |
| 4 | MBINGA TC | 1,500 | 208,000,000 | 1408 | 164,896,500.00 |
| 5 | MBINGA DC | 640 | 44,440,000 | 152 | 14,949,000.00 |
| 6 | NYASA DC | 980 | 52,000,000 | 872 | 41,025,000.00 |
| 7 | SONGEA MC | 3092 | 384,170,000 | 3138 | 380,113,500.00 |
| 8 | SONGEA DC | 400 | 31,000,000 | 459 | 52,622,00.00 |
| **Jumla** | | **10,182** | **915,680,000.00** | **8,370** | **783,926,622.00** |

**Jedwali Na. 17: Idadi ya Wafanyabiashara Wakubwa, wa kati na wadogo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Wafanyabiashara | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wakubwa | Wakati | Wadogo |
| 1 | Namtumbo DC | 6 | 890 | 641 |
| 2 | Madaba DC | 2 | 66 | 90 |
| 3 | Tunduru DC | 0 | 5 | 1,750 |
| 4 | Mbinga TC | 20 | 411 | 1,219 |
| 5 | Mbinga DC | 0 | 2 | 105 |
| 6 | Nyasa DC | 10 | 18 | 62 |
| 7 | Songea MC | 3 | 16 | 600 |
| 8 | Songea DC | 10 | 100 | 850 |
| **JUMLA** | | **51** | **1,508** | **5,317** |

#### 2.8.2.2 Usajili wa Machinga

Mkoa uliunda uongozi wa Shirikisho la Machinga ngazi ya Mkoa tangu 6 Oktoba, 2021 na kwa sasa uongozi wa Machinga ngazi ya Mkoa wanashirikiana vyema na uongozi wa machinga ngazi ya Halmshauri katika kutekeleza majukumu mbalimbali, Mkoa wa Ruvuma unaendelea na usajili wa kundi la Machinga kupitia Mfumo Jumuishi wa Kidigitali wa Usajili na kuratibu Wafanyabiashara ndogondogo maarufu kwa Jina la Machinga, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 Mkoa ulikuwa umesajili Wanachama **697** kati ya hao Wanawake ni **441** na Wanaume ni **256**, na Jumla ya malipo kiasi cha shilingi **5,760,000** (**Milioni tano laki saba sitini elfu)** ikiwa ni ada ya usajili wa Mfanyabiashara mdogomdogo kupitia mfumo wa Usajili.

**Jedwali Na. 18: Idadi ya masoko rasmi na yasiyo rasmi katika Mkoa**

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Masoko | |
|---|---|---|---|
| | | Rasmi | Yasiyo Rasmi |
| 1 | Namtumbo dc | 4 | 21 |
| 2 | Madaba dc | 1 | 6 |
| 3 | Tunduru dc | 2 | 4 |
| 4 | Mbinga tc | 3 | 19 |
| 5 | Mbinga dc | 3 | 15 |
| 6 | Nyasa dc | 16 | 0 |
| 7 | Songea mc | 9 | 0 |
| 8 | Songea dc | 6 | 1 |
| **JUMLA** | | **43** | **67** |

#### 2.8.2.3 Hali ya majukwaa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi

Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuunda Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake kiuchumi, hii ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi tarehe 6 Juni, 2016.

Majukwaa haya yameundwa rasmi tangu tarehe 21 Februari, 2023 kuanzia ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata, Mtaa na Vijiji. Halmashauri na Mkoa, ambapo hadi sasa jumla ya Majukwaa **173** yameundwa katika ngazi za Kata, Majukwaa **124** katika ngazi ya Mitaa katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Halmashauri ya Mji Mbinga na Majukwaa **8** yameundwa katika ngazi za Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma na Jukwaa 1 katika ngazi ya Mkoa na tarehe 8 Machi, 2023 ulifanyika uzinduzi rasmi wa Jukwaa la Mkoa kupitia sherehe za siku ya Wanawake duniani iliyoadhimishwa Kimkoa katika Wilaya ya Nyasa. Na hadi sasa majukwaa haya yapo hai.

### 2.8.3 Uwekezaji

#### 2.8.3.1 Vichocheo vya uwekezaji Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma una fursa kadhaa ambazo hutumiwa katika kusukuma mbele maendeleo ya Mkoa. Fursa za msingi zilizopo ni kama zifuatazo: -

(i) Eneo kubwa linalofaa kwa kilimo kwa mazao yote ya chakula na biashara;

(ii) Hali nzuri ya hewa; Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa michache nchini yenye bahati ya kupata mvua za kutosha ambazo hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Mei kila mwaka. Wastani wa kiasi cha mvua inayonyesha kwa mwaka ni mm.1100;

(iii) Mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Mkoa wa Ruvuma una jumla ya hekta **197,108.2** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta **7,388.3** zimeendelezwa.

(iv) Maeneo yenye jumla ya ukubwa wa ekari **57,743.35** yametambuliwa kwa ajili ya kilimo cha pamoja katika halmashauri 8 za Mkoa wa Ruvuma.

(v) Kuwepo kwa mazao ya chakula na biashara katika kila Wilaya. Mazao hayo ni pamoja na mahindi, mpunga, kahawa, korosho na tumbaku;

(vi) Uwepo wa Maliasili. Mkoa wa Ruvuma una maliasili nyingi zikiwemo madini, wanyama pori na misitu ya asili;

(vii) Kuwepo kwa nguvukazi ya kutosha. Mkoa una wananchi wenye ari kubwa ya kufanya kazi kwa bidii kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka; na

(viii) Kufunguka kwa miundombinu ya barabara, Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma zimeunganishwa na mtandao wa barabara za lami. Pia Mikoa mingine inayotuzunguka imeunganishwa na barabara ya kiwango cha lami.

(ix) Uwepo bandari ya Mbamba bay kwenye ziwa Nyasa inayowezesha usafirishaji wa Mizigo na Abiria kwa njia ya maji kwenye nchi jirani ya Malawi na maeneo mengine yanayofikiwa na ziwa Nyasa.

### 2.8.3.2 Maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za Uwekezaji.

Mkoa wa Ruvuma kupitia Halmashauri imetenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uwekezaji na ujenzi wa viwanda kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatavyo:

**Jedwali Na. 19: Maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za uwekezaji**

| S/N | Jina La Halimashauri | Eneo Lililotengwa | Ukubwa wa Eneo (Hekari) |
|---|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Songea | Mletele | 3619.17 |
| | | Mwanamonga | 3581.68 |
| | | Lilambo | 953.70 |
| | | Tanga | 1659.00 |
| | | Mwangemshindo (EPZA) | 5000.00 |
| | | Ruhuwiko | 117.33 |
| 2 | Mbinga Mji | Lusaka- Mwembe | 186.61 |
| | | Lusaka Maumba | |
| | | Tanki la maji | |
| | | Luponda | |
| | | Utemi | |
| 3 | Namtumbo DC | kituo kikuu cha Mabasi | 89.68 |
| | | Hospitali ya wilaya | |
| | | Mchafu kuoga | |
| | | Minazini | |
| | | Mageuzi | |
| | | VETA Saruti | |
| 4 | Tunduru DC | Nakayaya | 140.12 |
| | | Nakayaya Magharibi | |
| | | Ngalinje | |
| | | EPZ | |
| 5 | Nyasa DC | Kilosa | 41 |
| 6 | Madaba DC | Ifungwa | 400 |

### 2.8.3.3 Uwekezaji katika Sekta ya Maliasili.

**a) Misitu.**

Vipo viwanda 4 vikubwa vya kuchakata mazao ya misitu, kati ya hivyo 2 ni vya watu binafsi ambavyo vipo katika maeneo ya Madaba na Mbinga, kiwanda 1 kinachotembea (Mobile saw mill) kinamilikiwa na vijiji katika Wilaya ya Tunduru, na kiwanda 1 kinahudumia na kumilikiwa na vijiji vya Wilaya ya Namtumbo na Songea. Viwanda hivi vinafanya uvunaji na uchakataji wa mbao kwenye misitu ya vijiji na vimefadhiliwa na WWF (World Wide Fund - for nature) pamoja na mradi wa FORVAC.

**b) Wanyamapori**

Katika sekta ya wanyamapori kuna wawekezaji wawili katika vitalu vya uwindaji wa kitalii. Wawekezaji hao ni Wembere Hunting Safari aliye katika kitalu cha Mwantis B katika Kijiji cha Ifinga Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na The Best Luxury Safari aliyepo katika vitalu vilivyopo katika Hifadhi za jamii WMA za Mbarang'andu iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na Nalika iliyopo Halmashauri ya wilaya ya Tunduru.

**Jedwali Na. 20: Maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya shughuli za utalii**

| Halmashauri | Eneo pendekezwa | Umiliki wa Eneo | Ukubwa wa Eneo | Shughuli Zinazoweza Kufanyika |
|---|---|---|---|---|
| Nyasa | Hifadhi ya Mbambabay | Halmashauri | 597 ha | Utalii wa fukwe, visiwa, samaki wa mapambo, michezo ya majini (Beach resorts) |
| | Hifadhi ya Luikei | TFS | 2,100 | |
| | Hifadhi ya Ndengele | TFS | 2,466 ha | |
| | Fukwe za Liuli | Halmashauri ya kijiji | 20 ha | Jiwe la Pomonda, Beach camp, Samaki wa mapambo, historia ya Kanisa la Anglikana, michezo ya majini, ngoma za asili |
| | Fukwe za Lundu | Halmashauri ya kijiji | 10 ha | Jiwe la Chingata, fukwe, Samaki wa mapambo, majengo ya historia, michezo ya majini, ngoma za asili |
| | Hifadhi ya Misitu ya asili Lilengalenga | Halmashauri ya kijiji | 23,046 ha | |
| | Hifadhi ya Liparamba | TAWA | 57,099 ha | Utalii wa picha, utafiti wa mimea, utalii wa uwindaji |
| Mbinga | Lugari Zoo | Binafsi | 24 ha | Jiwe la Mbuji, kilimo cha ngoro Tuliladam |
| | Hifadhi ya Tuliladam | Chipole Sisters | 8,434 ha | |
| | Hifadhi ya Litumbandyosi | TAWA | 494 km$^2$ | Utalii wa picha, utafiti wa malikale, utafiti wa kuwinda (Bush camps) mapango ya Amani Makoro |
| | Amani Makoro | Halmashauri ya kijiji | | |
| Namtumbo | Pori la Selous | TAWA | 48,000 km$^2$ | Mbarang'andu uwindaji wa kitalii na picha |
| | Mbarang'andu | Jumuiya | 3,183 km$^2$ | |
| | Kisungule WMA | Jumuiya | 1,345 km$^2$ | Utalii wa kuwinda na picha |
| | Kimbanda WMA | Jumuiya | 2,146.5 km$^2$ | Utalii wa kuwinda na picha |

| Halmashauri | Eneo pendekezwa | Umiliki wa Eneo | Ukubwa wa Eneo | Shughuli Zinazoweza Kufanyika |
|---|---|---|---|---|
| | NE. Undendeule | Jumuiya | 305,495 $km^2$ | Utalii wa kuwinda na picha |
| Songea | Hifadhi ya Gesimasowa | TAWA | 764 KM2 | Utalii wa picha na utafiti |
| | Luhira Zoo, Makumbusho ya Majimaji | TAWA | 311.2 ha | Utalii wa picha na utafiti, utalii wa kitamaduni na makumbusho ya vita vya majimaji |
| | Matogoro | TFS | 7,457.24 ha | Utalii wa picha, mimea, vipepeo, chanzo cha mto Ruvuma |
| | Luhira | TAWA | 311.2 ha | Utalii wa picha na kutembea |
| Tunduru | Mwambesi Nature Reserve | TFS | 104,052 ha | Utalii wa picha na utafiti, utalii wa uwindaji, njia ya kusafirisha watumwa (Mbatamila – Masonya – Kilwa) |
| | Chingole WMA | Jumuiya | 901 $km^2$ | |
| | Nalika WMA | Jumuiya | 1,391 $km^2$ | |

### 2.8.3.4 Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo.

Mkoa wa Ruvuma una fursa ya kupata mvua nyingi, ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo na inayokubali kuzalisha takribani mazao aina zote. Hekta **4, 007,746** zinafaa kwa kilimo, hadi sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **583,279** sawa na asilimia **15** ya eneo lote**,** na kufanya Mkoa kuwa na ziada ya hekta **3, 424,467** sawa na asilimia **85.** Mbali na mazao ya chakula na biashara yanayolimwa Mkoani Ruvuma, ipo pia fursa ya kulima mazao ya bustani ni pamoja na Parachichi, Embe, Machungwa, Matikiti, Ndizi, Papai na Mbogamboga.

Mkoa wa Ruvuma una wawekezaji wakubwa wawili waliowekeza katika Sekta ya Kilimo ndani ya Mkoa ambao ni

Shamba la Kahawa la AVIV lililopo Kijiji cha Lipokela Wilaya ya Songea linalomilikiwa na kampuni ya OLAM na shamba kubwa la "**Ndolela Farm"** lililopo katika Halmashauri ya Madaba.

Hivi karibuni amejitokeza muwekezaji mwingine Mkubwa kutoka nchini Uganda Kampuni ya **Madhvan Group Ltd** ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kilimo cha Miwa na Kiwanda cha Sukari katika kijiji cha Magwamila Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

**Jedwali Na. 21: Maeneo ya kilimo cha pamoja yaliyotengwa katika Halmashauri za Wilaya**

| Na | Halmashauri | Kijiji | Eneo (Ekari) | Zao |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tunduru | Lukumbule | 6,000 | Ufuta |
| | | | 4,000 | Alizeti |
| | | | 500 | Korosho |
| | | Misechela | 3,000 | Alizeti |
| | | Ngapa | 4,000 | Soya |
| | | Matemanga | 2,000 | Soya |
| | | Marumba | 2,000 | Soya |
| | | Namasakata | 1,000 | Michikichi |
| | | | **22,500** | |
| | | | | |
| 2 | Mbinga Dc | Litumbandyosi | 500 | Mpunga |
| | | Sangamabuni | 400 | Mpunga |
| | | Nambalapala | 1000 | Mpunga |
| | | | **1,900** | |
| | | | | |
| 3 | Namtumbo | Kitanda | 278 | Ufuta |
| | | Limamu | 469 | Ufuta |
| | | Likuyusekamaganga | 312 | Alizeti |
| | | Matepwende - Lisimonji | 1,245 | Ufuta |
| | | Namali | 301 | Ufuta |
| | | NAFCO (ekari15,000) | 6,000 | Mahindi |

| Na | Halmashauri | Kijiji | Eneo (Ekari) | Zao |
|---|---|---|---|---|
| | | | 2500 | Alizeti |
| | | | 4,000 | Soya |
| | | | 1000 | ufuta |
| | | | **16,105** | |
| | | | | |
| 4 | Songea DC | Magwamila | 5,000 | Korosho |
| | | Nambendo | 5,000 | Korosho |
| | | Matimira | 150 | Alizeti |
| | | Parangu | 100 | soya |
| | | | 200 | Alizeti |
| | | | **10,450** | |
| | | | | |
| 5 | Mbinga TC | Mkwaya magereza | 1000 | Alizeti |
| | | | | |
| 6 | Songea MC | Lilambo | 122 | Soya |
| | | Mletele | 30 | Alizeti |
| | | Tanga | 40 | Alizeti |
| | | | **192** | |
| 7 | Madaba | Ndelenyuma | 400 | Korosho |
| | | Mkongotema | 1000 | kahawa |
| | | | **1,400** | |
| **JUMLA KUU** | | | **53,547.00** | |

### 2.8.3.5 Uwekezaji katika Sekta ya Madini

Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na madini aina mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 28. Wawekezaji mbalimbali wapo katika Mkoa wa Ruvuma wakijishughulisha na Shughuli za uchimbaji wa madini ikiwepo kampuni Kubwa za Ruvuma Coal Ltd, Tancoal, Jitegemee Company Ltd na makampuni mengineyo zaidi ya 16 yanayojishuhulisha na uchimbaji wa makaa ya mawe.

**Jedwali Na. 22: Aina ya madini yanayopatikana katika Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | Aina ya Madini | Mahali yanapopatikana |
|---|---|---|
| 1 | Dhahabu | **Nyasa** (Darpori, Mpepo na Nindi)<br>**Mbinga** (Mhongozi na Lukalasi)<br>**Namtumbo** (Kitanda)<br>**Tunduru** (Mbesa na Mbati) |
| 2 | Shaba | **Nyasa** (Mt. Livingstone)<br>**Mbinga** (Ndongosi)<br>**Tunduru** ( Mbesa na Mbati) |
| 3 | Makaa ya Mawe | **Nyasa** (Liweta na Malini)<br>**Mbinga** (Luanda, Mbuyula na Paradiso)<br>**Songea** (Mhukuru) |
| 4 | Chuma | **Namtumbo** (Mtonya) |
| 5 | Urani | **Namtumbo** (Mtonya) |
| 6 | Madini ya Ujenzi na Viwanda *(Mchanga, Kokoto, Moramu naMawe)* | **Nyasa**<br>**Mbinga**<br>**Namtumbo**<br>**Songea** (Mhukuru na Mtyangimbole) na **Tunduru** |
| 7 | **Madini ya Vito** (*Sapphire, Ruby, Alexandrite, Chrisoberly, Spinel, Ganet, Aquamarine, Tourmaline)* | **Tunduru (**Ngapa, Muhuwesi, Majimaji, Mbuyula na Lukala)<br>**Nyasa** (Maeneo ya Mwambao wa Ziwa)<br>**Mbinga** (Maeneo ya Mkako, Masuguru, Ngembambili, Amani Makolo na Kuhagala)<br>**Namtumbo**(Mputa,Lusewa,Suluti,Mtwarapachani,Mkongo na Kiburungutu) |

**Mikakati ya uendelezaji wa sekta ya uwekezaji katika Mkoa wa Ruvuma.**

i. **Kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma**

Fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma zinatangazwa kupitia mwongozo wa fursa za uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma zimeainishwa na kupitia maonesho hayo Mkoa umeweza kupokea wageni mbalimbali walionesha nia ya kuwekeza katika Mkoa wetu.

ii. **Kutenga na kupima maeneo maalum ya viwanda.**

Halmashauri zimeagizwa kutenga maeneo maalum, kwa ajili ya wawekezaji ambayo yamepimwa na yasiyohitaji fidia kwa mwekezaji na yenye huduma muhimu kama vile maji, umeme, barabara n.k, jambo hili litasaidia kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

iii. **Uanzishwaji na Uimarishaji wa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na Mkoa.**

Uendelezaji wa sekta ya viwanda unategemea uwepo wa Mabaraza ya Biashara katika ngazi za Wilaya na Mkoa. Mabaraza ya Biashara ni sehemu nzuri ya kujadili fursa na kuweka mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na taarifa za Vikao vya Mabaraza zinatakiwa kuwasilishwa katika vikao vya DCC na RCC ili maeneo yenye changamoto yaweze kutatuliwa na vikao vya ngazi hizo.

iv. **Uanzishwaji wa kongano (clusters).**

Kila Halmashauri imeagizwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuhakikisha kuwa inandaa maeneo kulingana na kongano za shughuli za viwanda ili kuweza kuanzisha industrial parks.

v. **Kusimamia na kuendeleza shughuli za kijasiriamali.**

Halmashauri zimetakiwa kuwajibika kikamilifu katika kuzitambua na kuziendeleza shughuli za kijasiriamali na kuhakikisha zinatenga fedha kwa ajili ya kukuza shughuli

hizo. Katika kuboresha mazingira ya wajasiriamali ya kufanyia biashara, wajasiriamali 3769 wamepangwa katika maeneo 59 yaliyotengwa katika Halmashauri zote za Mkoa.

## 2.9 SIDO

### A. Utekelezaji wa Kazi za Shirika kwa Kipindi cha Julai 2023 Hadi Juni 2024

Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) lina huduma kuu nne (4) ambazo ni:-

**1.** Huduma ya Uendelezaji wa Teknolojia
**2.** Huduma ya Mafunzo na ushauri wa biashara
**3.** Huduma ya Masoko na Uwekezaji
**4.** Huduma za Mikopo kwa Wajasiriamali

#### a) Huduma ya uendelezaji wa Teknoloja

SIDO inahamasisha uanzishwaji na uwekezaji katika Viwanda vidogo ili kuongeza uchakataji wa rasilimali zilizopo nchini ikiwemo mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini. Aidha kumekuwa na mwamko mkubwa kwa wananchi katika kushiriki shughuli za uanzishaji miradi ya uzalishaji hivyo kupelekea ongezeko la uhitaji wa Teknolojia wezeshi kwa maendeleo ya viwanda vidogo endelevu.

Shirika limekuwa likitengeneza mashine kupitia Vituo vyake saba vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) na kushirikisha sekta

binafsi katika kuhakikisha teknolojia zinazohitajika na sahihi zinawafikia wananchi. Uwepo wa mazao yanayohitaji teknolojia za uchakataji rahisi na rafiki, mkakati wa kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo takriban asilimia 30 ya mazao yanaharibika. Lengo ni kuhakikisha kunakuwa na teknolojia mbalimbali ambazo zinapatikana hapa mkoani na nje ya mkoa kwa wajasiriamali ili waweze kuanzisha viwanda vidogo na kuongeza uzalishaji na ufanisi. Kuwezesha kuboresha bidhaa wanazozalisha, kuboresha maeneo ya uzalishaji na pia kuleta mwamko katika kuwekeza zaidi katika teknolojia ambayo itawasaidia kuongeza tija.

I. Viwanda vidogo **47** vya kuongeza thamani mazao ya kilimo vimeanzishwa baada ya kuunganishwa na kujipatia mashine kutoka SIDO na wazalishaji wengine wa teknolojia.
II. Viwanda vidogo **158** vimetembelewa na vimepewa ushauri wa kiufundi ikiwa ni pamoja na ushauri wa kuboresha bidhaa, mpangilio wa uzalishaji kiwandani, Kuongeza ufanisi viwandani na uboreshaji wa mazingira ya uzalishaji kwa kufuata miongozo iliyopo. Pia uchaguzi wa mashine, vipuri na matengenezo mbalimbali ya mashine yalifanyika kwa kushirikiana na mafundi waliopo mtaa wa Viwanda wa SIDO.

### 2.9.2 Huduma ya mafunzo na ushauri wa biashara

Shirika limekuwa likitoa mafunzo ya ujuzi na uendelezaji biashara kwa wahitaji baada ya kuhitimu na kuingia katika soko la ajira ambapo wengi wao huingia katika sekta binafsi kwa kujiajiri.

Kuongezeka kwa wajasiriamali wazalishaji na biashara zao kuboreshwa na kuwa shindani katika sekta isiyo rasmi na rasmi na umuhimu wa sekta hii yenye kutengeneza ajira nyingi na kuchangia katika uchumi unahitaji ujuzi na ushauri wa kitaalam kwa wakati na ubora.. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia Machi, 2024; -

I. **Wajasiriamali 745 (Wanawake 477 na Wanaume 268)** wamepatiwa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kujipatia ujuzi wa kuanzisha/kuendeleza viwanda vidogo. Mafunzo haya yalikuwa kwenye nyanja za ujasiriamali, usimamizi wa biashara, usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa sabuni za maji na za mche, utengenezaji wa batiki, elimu ya masoko, urasimishaji wa biashara, ufungashaji wa bidhaa na Uwekaji lebo,

II. **Wajasirimali 938** wamepewa ushauri wa biashara ambao umelenga kuimarisha biashara kwa kuzirasimisha, kuongeza uzalishaji na ufanisi, usimamizi wa fedha za mikopo, kuongeza mitaji, kuongeza faida na kujiimarisha zaidi.

### 2.9.3 Huduma ya masoko na uwekezaji

Bidhaa za viwanda vidogo zinazalishwa kwa wingi na kwa kiwango kikubwa na zinahitaji kuyafikia masoko ya ndani na nje. Wazalishaji wa bidhaa hizi wanahitaji taarifa sahihi za mlaji ili kuweza kukidhi na kuwavutia kununua bidhaa. Uhitaji wa taarifa za masoko, vifungashio na ufungashaji ni endelevu. Aidha bidhaa nyingi zinazalishwa na zimekuwa zikiongezeka hivyo, ili kuhimili ushindani na kuwa endelevu taarifa za masoko zinahitajika kuwafikia wajasiriamali. Shirika limeendelea kutumia tovuti, mitandao ya jamii na maonesho ambapo fursa na taarifa za masoko zimekuwa zikiwafikia. Sekta ya viwanda vidogo ukuaji wake unaendana na uzalishaji bidhaa zenye kukidhi mahitaji ya soko kwa wakati husika. Hivyo taarifa za soko na ushawishi wa mlaji kutumia bidhaa za viwanda vidogo kupitia matangazo, kongamano za kibiashara na maonesho hufanyika.

i. **Wajasiriamali 84** wamewezeshwa kupata fursa na taarifa za kimasoko
ii. **Wajasiriamali 17** kutoka Mkoa wa Ruvuma wameshiriki **maonesho ya SIDO Taifa** yaliyofanyika Mkoani Njombe kuanzia **tarehe 21 hadi 31 Oktoba, 2023**. Kupitia maonesho hayo waliweza kuuza bidhaa zao, kupata oda, kujifunza kutoka kwa wenzao na kupata elimu kutoka kwenye taasisi mbalimbali zilizoshiriki kwa ajili ya kuendeleza biashara zao.

iii. **Wajasiriamali 41** wameunganishwa na kituo cha usambazaji wa vifungashio-SIDO Dar es salaam na pia wasambazaji wa vifungashio hapa mkoani Ruvuma. Pia **Wajasiriamali 16** waliwezeshwa kutengeneza lebo zenye mvuto kwa bidhaa zao.
iv. SIDO Ruvuma ina fremu za **maduka 21** ambazo zimepangishwa kwa wajasiriamali kwa ajili ya kuuzia bidhaa na huduma mbalimbali.
v. Mtaa wa Viwanda wa SIDO Ruvuma una **majengo 29** yanayotumika kufanyia shughuli za wajasiriamali kuzalisha bidhaa mbalimbali na kutoa huduma katika mtaa wa viwanda uliopo SIDO.

### 2.9.4 Huduma ya mikopo kwa wajasiriamali

SIDO imeendelea kuwezesha sekta ya viwanda vidogo kwa kuwapatia mikopo yenye riba ndogo na kuwaunganisha na Taasisi za fedha. Huduma ya mikopo inayotolewa na SIDO kupitia mfuko wa kuendeleza wajasiriamali inazingatia uzalishaji katika sekta mbalimbali kama vile sekta ya viwanda, biashara, ufugaji, kilimo, uvuvi, madini na mifugo. Mfuko wa kuendeleza wajasiriamali wananchi (National Entrepreneurship Development Fund-NEDF) ulianzishwa mwaka-1994 kwa azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya mfuko huu ni kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kujipatia mitaji ili kuondoa umaskini kwa kuendeleza miradi yao.

Kwa kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi kufikia Juni 2024 Jumla ya mikopo **224** yenye thamani ya shillingi **891,100,000.00** ilitolewa kwa Wajasiriamali.

**Jedwali Na. 23: Mchanganuo wa mikopo kijinsia**

| Wanawake | | Wanaume | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi | Thamani ya mikopo (Sh.) | Idadi | Thamani ya mikopo (Sh.) | Idadi | Thamani (sh.) |
| 105 | 396,900,000/= | 119 | 494,200,000/= | 224 | 891,100,000/= |

### 2.9.5 Ukusanyaji wa maduhuli ya serikali

**Jedwali Na. 24: Mchanganuo wa ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali.**

| Makisio 2023/24 | Makusanyo halisi | Asilimia ya ukusanyaji |
|---|---|---|
| 256,500,000 | 266,809,870 | 104% |

### 2.9.6 Changamoto za utekelezaji

i. Ufinyu wa bajeti unasababisha kutofikisha shughuli zetu maeneo ya vijijini pamoja na kuwa mahitaji ni makubwa.
ii. Uchakavu wa miundombinu ya mtaa wa Viwanda wa SIDO Songea
iii. Upungufu wa wafanyakazi ambao unaathiri utoaji wa huduma
iv. Mfuko wa kukopesha wajasiriamali wananchi (NEDF) una fungu dogo ukilinganisha na maombi ya mikopo yanayopokelewa kutoka kwa Wajasiriamali.

### 2.9.6 Mikakati ya kutatua changamoto

i. Kuwa na Miradi ya ubia ya kimkakati ya kimaendeleo ili kuongeza mapato ya Shirika ikiwemo ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mitaa ya Viwanda ya SIDO na kutumia sehemu ya mapato yake kuongeza wigo wa kuwafikia watu wengi.

ii. Kuendelea kuomba kuongezewa fedha za mikopo kupitia mfuko wa kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF) na kupatiwa wafanyakazi ili kujiimarisha na kuwezesha Viwanda vidogo vingi.

iii. Mafunzo ya kupitia mfumo wa kidigitali ili kufikia kundi kubwa likiwemo la vijana.

**D. Hitimisho**

Uwezeshwaji wa SIDO unahitajika sambamba na mikakati yake iliyopo ili kuwezesha sekta ya Viwanda vidogo kuendelea. Shirika linatakiwa kupatiwa fedha ili miradi yake ya kimkakati iweze kufanyika hatimaye kuongeza wigo na kufikia wahitaji kwa kiwango kikubwa.

## 2.10 Sekta ya Madini

**A. Utangulizi**

Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma inahudumia Mkoa wa Ruvuma wenye Wilaya tano. Aidha, Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma ina ofisi ndogo za madini katika maeneo ya Ngaka na Tunduru.

Kazi zilizotekelezwa na ofisi hii ni pamoja na;

i. Utoaji wa leseni za madini na vibali mbalimbali;
ii. Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;
iii. Usimamizi wa masoko ya madini;
iv. Usimamizi wa uzalishaji na mauzo ya Makaa ya Mawe; na
v. Utoaji wa elimu kuhusu Sheria ya Madini na kanuni zake kwa wachimbaji

## 1.0 Madini yapatikanayo mkoani Ruvuma

**Jedwali Na. 25:** Aina ya madini na mahali yanapopatikana Mkoani Ruvuma

| Na | Aina ya madini | Kijiji | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 1 | Dhahabu | Darpori | Nyasa |
| | | Mpepo | |
| | | Liparamba | |
| | | Mipotopoto | |
| | | Nindi | |
| | | Lukarasi | Mbinga |
| | | Mhongozi | |
| | | Kitanda | Namtumbo |
| 2 | Urani (Uranium) | Likuyuseka–Maganga | Namtumbo |
| 3 | Shaba | Mbesa | Tunduru |
| | | Mbati | |
| | | Lukarasi | Mbinga |
| | | Mhongozi | |
| 4 | Makaa ya Mawe (Coal) | Ruanda | Mbinga |
| | | Mbuyula | |
| | | Ntunduwalo | |
| | | Paradiso | |
| | | Liweta | Nyasa |
| | | Malini | |
| | | Mhukuru, Mtyangimbole | Songea |
| | | Mhepai | |
| | | Ndunduwalo | |
| | | Mtyangimbole | |
| | | Maposeni | |
| 5 | Chokaa (Limestone) | Maposeni | Songea |
| | | Mtyangimbole | |
| 6 | Chuma | Mtonya | Namtumbo |

| Na | Aina ya madini | Kijiji | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 7 | Quartz | Mtyangimbole, | Songea |
| 8 | Tantalite | Kiburungutu | Namtumbo |
| 9 | Gemstones (Sapphire, Amethyst, Alexandrite, Tourmaline, Garnets, Aquamarine, Spinel, Ruby, | Ngapa, Muhuwesi, Mtetesi, Ngatala, Ligunga, Majimaji, Matepwende, Nakapanya, Mkako, Amani Makolo, Suluti, Mkeke na Lumesule | Tunduru , Mbinga & Namtumbo |
| 10 | Ulanga | Kiburungutu | Namtumbo |
| 11 | Madini Ujenzi | Maeneo Mbalimbali | Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma |

### 2.10.2 Taarifa ya leseni za uchimbaji madini na biashara

Ofisi imekuwa ikitoa leseni za Uchimbaji madini mdogo (PML) pamoja na leseni za Biashara ya madini (Dealers, Brokers) kwa mujibu wa Sheria ya Madini **Sura 123** na Kanuni zake. Kwa mwaka wa fedha **2023/2024** kati ya mwezi Julai 2023 hadi **Juni, 2024** idadi ya leseni zilizotolewa ni kama zilivyoainishwa katika Jedwali Na 32. hapo chini.

**Jedwali Na. 26: Leseni za Uchimbaji Madini na Biashara ya Madini Mkoani Ruvuma kati ya Julai, 2023 hadi Juni, 2024**

| Na. | Aina ya Leseni | Lengo | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Leseni (PML) | 375 | 422 | 113 |
| 2. | Dealers | 90 | 111 | 123 |
| 3. | Brokers | 30 | 39 | 130 |
| | **Jumla** | **495** | **572** | |

Aidha, hadi sasa Mkoa wa Ruvuma una jumla ya leseni 34 za Utafutaji Madini (Prospecting Licence-PL), leseni Tisa (9) za uchimbaji wa kati (Mining Licence-ML) na leseni Moja (1) ya uchimbaji mkubwa (Special Mining Licence-SML) na leseni

mbili (2) za Uchenjuaji/Uchakataji Madini (Processing Licence-PCL).

### 2.10.3 Ukusanyaji wa maduhuli ya serikali

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Afisa Madini Mkazi ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 41,000,000,000.00**. Baada ya mapitio ya tathimini kwa makusanyo ya nusu ya mwaka lengo likapunguzwa na kuwa **Shilingi Bilioni 38,000,000,000.00** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Kuanzia Mwezi Julai hadi Juni 2023/2024, Ofisi imekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 28.96** sawa na **asilimia 76%** ya lengo la makusanyo kwa kipindi husika. Jedwali hapo chini linaonesha makusanyo ya kila mwezi kwa kipindi hicho.

**Jedwali Na. 27: Mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha Mwezi Julai 2023 hadi Juni 2024**

| Mwezi | Makisio kwa Mwezi Mwaka2023/2024 | Makusanyo Halisi Mwaka 2023/2024 | % ya Makusanyo |
|---|---|---|---|
| | (TZS) | (TZS) | |
| Julai | 3,166,666,666.67 | 1,339,909,329 | 42% |
| Agosti | 3,166,666,666.67 | 2,989,675,356 | 94% |
| Septemba | 3,166,666,666.67 | 2,069,806,377 | 65% |
| Oktoba | 3,166,666,666.67 | 2,794,188,161 | 88% |
| Novemba | 3,166,666,666.67 | 2,341,463,902 | 74% |
| Disemba | 3,166,666,666.67 | 1,587,259,934 | 50% |
| Januari | 3,166,666,666.67 | 2,200,166,201 | 69% |
| Februari | 3,166,666,666.67 | 1,989,561,425 | 63% |
| Machi | 3,166,666,666.67 | 2,534,403,912 | 80% |
| April | 3,166,666,666.67 | 1,691,400,793 | 53% |
| Mei | 3,166,666,666.67 | 4,049,544,748 | 139% |
| Juni | 3,166,666,666.67 | 3,013,722,758 | 95% |
| **Total** | **38,000,000,000** | **28,961,102,896** | **76%** |

### 2.10.4 Usimamizi wa masoko ya madini

Ofisi ya Madini Ruvuma inasimamia masoko mawili ya madini. Soko la Madini ya dhahabu na Vito lililopo Songea pamoja na Soko la Madini ya vito katika Wilaya ya Tunduru. Masoko haya yote yanasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni za Masoko ya Madini za Mwaka 2019.

**Jedwali Na. 28: Madini yaliyouzwa katika Masoko ya Madini mkoani Ruvuma katika kipindi cha mwezi Julai hadi Juni Mwaka wa Fedha 2023/2024.**

| Aina ya Madini | Uzito (Kg) | Thamani (Tzs) | Mrabaha (Tzs) | Ada ya Ukaguzi (Tzs) | Kodi ya Huduma (Tzs) |
|---|---|---|---|---|---|
| Vito vya Thamani | 357,961.09 | 6,633,254,569.10 | 473,724,698.90 | 67,472,545.69 | 19,899,763.71 |
| Dhahabu | 52.64 | 8,021,997,759.64 | 481,319,865.20 | 80,219,977.87 | 24,065,993.28 |
| **Jumla** | | **14,655,252,328.74** | **955,044,564.10** | **47,692,523.56** | **43,965,756.99** |

### 2.10.5 Uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe

Uchimbaji na uuzaji wa makaa ya Mawe Mkoani Ruvuma ulianza mwaka 2011 kupitia Kampuni ya *Tancoal Energy Ltd*. Aidha shughuli za uchimbaji makaa ya mawe zilianza kuongezeka Mwaka 2019/2020 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nishati Ulimwenguni na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi. Makampuni yaliyojitokeza kushiriki katika biashara hiyo ni pamoja na Ruvuma Coal Ltd, Jitegemee Holdings Co. Ltd, Mbuyula Coal Ltd, Rutanza Coal Ltd, Njuga Mining Ltd na mengineyo katika uchimbaji mdogo. Makaa haya huuzwa ndani

na nje ya nchi hususani nchi zinazotuzunguka, barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es Salaam.

Uzalishaji na uuzaji wa Makaa ya Mawe umetoa mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya madini na uchumi wa mkoa wa Ruvuma. Kwa Mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 Mwaka wa Fedha 2023/2024 kiasi cha **Tani 2,561,286.33** kiliuzwa kikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani (**USD) 309,182,024.08** na kuwezesha Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Ruvuma kukusanya maduhuli ya Serikali jumla ya Dola za Kimarekani **(USD) 9,419,174.60** kupitia Mrabaha na Ada ya ukaguzi.

**Jedwali Na. 29: Mauzo ya Makaa ya Mawe katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 katika Mkoa wa Ruvuma.**

| MWEZI | UZITO(T) | THAMANI (USD) | MRABAHA (USD) | ADA YA UKAGUZI (USD) |
|---|---|---|---|---|
| Jul-23 | 114,095.48 | 16,008,532.03 | 348,903.95 | 160,085.32 |
| Aug-23 | 220,147.40 | 28,998,022.54 | 702,118.10 | 163,725.59 |
| Sep-23 | 305,815.87 | 38,175,155.73 | 972,415.28 | 164,434.75 |
| Oct-23 | 271,484.86 | 31,526,300.61 | 765,929.38 | 169,349.31 |
| Nov-23 | 275,365.33 | 30,041,364.43 | 743,550.79 | 138,041.69 |
| Dec-23 | 169,340.90 | 21,888,537.71 | 518,331.25 | 156,335.94 |
| Jan-24 | 175,864.67 | 20,589,118.00 | 503,819.02 | 143,410.67 |
| Feb-24 | 205,443.31 | 24,277,431.00 | 613,345.87 | 148,997.85 |
| Mar-24 | 219,447.04 | 24,501,743.51 | 648,810.25 | 128,455.14 |
| Apr-24 | 132,240.84 | 18,526,310.38 | 433,564.69 | 123,625.55 |
| Mei-24 | 230,121.44 | 24,285,543.74 | 635,825.81 | 111,224.14 |
| Juni-24 | 241,919.19 | 30,363,964.40 | 751,083.01 | 173,791.25 |
| **JUMLA** | **2,561,286.33** | **309,182,024.08** | **7,637,697.40** | **1,781,477.20** |

### 2.10.6 Mchango wa sekta ya madini Mkoa wa Ruvuma

Sekta ya madini katika mkoa wa Ruvuma imekua ikichangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Kupitia sekta ya madini Mkoa wa Ruvuma umeweza kuwa kivutio kikubwa na kupata wawekezaji wengi kwenye shughuli zinazohusiana na madini kama Uchimbaji wa Madini, Ununuzi wa Madini, Usafirishaji wa Madini na Uchenjuaji wa Madini. Yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya madini Mkoani Ruvuma:

i. Ongezeko la ajira rasmi na zisizo rasmi na hivyo kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi;

ii. Kuongeza mchango wa fedha za kigeni nchini kutokana na mauzo ya madini nje ya nchi; na

iii. Kuongezeka kwa vyanzo mapato vya Halmashauri mbalimbali yatokanayo na ushuru wa huduma unaotozwa kwenye madini yanayochimbwa.

### 2.10.7 Changamoto za sekta ya madini katika mkoa wa ruvuma

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya madini mkoani Ruvuma, kumekuwepo na changamoto zifuatazo:

i. Ubovu wa barabara za maeneo ya migodini na hivyo kupelekea kutofikiwa ipasavyo kwa malengo ya uzalishaji, kuongezeka kwa gharama za matengenezo ya magari na gharama za uendeshaji migodi. Maeneo yenye changamoto kubwa zaidi ni pamoja na barabara ya Amani Makoro-Ruanda hadi Lituhi (80km), Peramiho-Mhepai (65km), Nakapanya-Ngapa (30km) Nyoni-Darpori (80km)

Nalasi-Matepwende (90km) na Likuyufusi-Mkenda (100km);

ii. Hitajio la kuongeza ubora wa makaa ya mawe kwa kutumia teknolojia ya kisasa kama (*Wash Plants)* ili kuweza kushindana na soko la Dunia;

iii. Ukosefu wa mitaji kwa wachimbaji wadogo hivyo kupelekea kusuasua kwa shughuli zao za uchimbaji wa madini; na

iv. Hitajio la taarifa za kijiolojia ili kubainisha kiasi na aina za mashapo ya madini.

**2.10.8 Mikakati ya kupambana na changamoto**

i. Ofisi tayari imewasilisha tarifa ya changamoto ya barabara kwa mamlaka husika kwa hatua zaidi;

ii. Kuendelea kuhamasisha wachimbaji wa makaa ya mawe pamoja na wawekezaji wengine kuleta mitambo ya kisasa ili kuongeza ubora ikiwemo matumizi ya *(Wash Plant)* ambapo hadi sasa *(Wash Plant)* zinatumiwa na migodi ya Ruvuma Coal (2) na Bharya Engineering and Contracting Co. Ltd (1);

iii. Wizara ya Madini imeendelea kuhamasisha Taasisi za kifedha kuwawezesha wachimbaji wadogo kimitaji; na

iv. Wizara kupitia Dira 2030 (Madini ni Maisha na Utajiri) inaendelea na programu za ukusanyaji tarifa za kijiolojia katika maeneo mbalimbali nchini.

## 2.11 Sekta ya Ardhi na Makazi

### A. Utangulizi

Ofisi ya ardhi Mkoa inasimamia masuala ya ardhi katika Halmashauri 8 za mkoa huu. Uanzishwaji wa ofisi hii ni moja ya mikakati ya Serikali kusogeza huduma karibu na wananchi ili kukabiliana na changamoto za Sekta hii na kukidhi mahitaji ya huduma za ardhi za Kupanga miji na vijiji, Uthamini, Upimaji, Umilikishaji na Usajili wa Hati na Nyaraka mbalimbali. Awali huduma hizi zilikuwa zinatolewa katika Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kusini ambayo ilikuwa Mtwara hivyo, wananchi walilazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita mia sita kufuata huduma hizi ambazo kwa sasa zinatolewa na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.

### 2.11.1 Kazi zilizofanyika kwa kwa kipindi cha Julai 2023 – Juni, 2024

Ofisi ya Ardhi Mkoa inaendelea kusimamia na kutekeleza Ilani ya chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 katika Ibara ya 72 – 76. Kazi zilizoelekezwa katika ibara hizo ni pamoja na upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na nyaraka mbalimbali, utatuzi wa migogoro ya Ardhi pamoja na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali. Utekelezaji wa masuala haya yameainishwa hapo chini.

### 2.11.2 Upimaji wa viwanja ,mashamba na mipaka ya vijiji.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024, jumla ya viwanja **7,059** na mashamba **15** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine. Aidha, jumla ya vijiji 45 vimepimwa upya baada ya kuhakiki mipaka yake. Jedwali Na.36 hapo chini linaonyesha taarifa upimaji wa viwanja, mashamba na mipaka ya vijiji:

**Jedwali Na. 30: Kuonyesha viwanja, mashamba na vijiji vilivyopimwa kwa kila Halmashauri**

| NA | HALMASHAURI | VIWANJA | | MASHAMBA | | MIPAKA YA VIJIJI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA |
| 1 | Songea Manispaa | 3202 | 320,200,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2 | Songea DC | 125 | 12,500,000 | 1 | 645,000.00 | 0 | 0 |
| 3 | Mbinga Mji | 1994 | 199,400,000 | 7 | 4,515,000.00 | 0 | 0 |
| 4 | Mbinga DC | 337 | 33,700,000 | 0 | 0 | 16 | 64,000,000 |
| 5 | Tunduru | 248 | 24,800,000 | 4 | 1,935,000.00 | 29 | 116,000,000 |
| 6 | Madaba | 613 | 61,300,000 | 3 | 2,580,000.00 | 0 | 0 |
| 7 | Nyasa | 277 | 27,700,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 8 | Namtumbo | 263 | 26,300,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | **7059** | **705,900,000** | **15** | **9,675,000** | **45** | **180,000,000** |

### 2.11.3 Mipango Miji Na Vijiji

Katika kipindi cha kuanzia Julai,2023 hadi Juni, 2024, jumla ya michoro **40** ya Mipangomiji yenye jumla ya viwanja **14,658** vya matumizi mbalimbali kutoka Mamlaka za upangaji ilipokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa. Aidha jumla ya viwanja **3,365** vimerasimishwa katika Halmashauri mbalimbali

za Mkoa wa Ruvuma kama inavyoonekana hapa chini kwenye jedwali Na.31

**Jedwali Na. 31: Kuonyesha idadi ya michoro ya mipangomiji kwa kila Halmashauri**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Michoro ya Mipango Miji | Idadi yaviwanja vilivyopangwa | Viwanja vilivyorasimishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga DC | 4 | 447 | 0 |
| 2 | Mbinga TC | 14 | 4,856 | 1934 |
| 3 | Namtumbo DC | 2 | 470 | 0 |
| 4 | Nyasa DC | 5 | 1,723 | 625 |
| 5 | Madaba DC | 7 | 3,431 | 0 |
| 6 | Songea DC | 0 | 0 | 0 |
| 7 | Songea MC | 4 | 2,104 | 417 |
| 8 | Tunduru DC | 4 | 1,627 | 389 |
| | **JUMLA** | **40** | **14,658** | **3,365** |

### 2.11.4 Umilikishwaji ardhi na usajili wa hati na nyaraka

kwa kipindi cha kuanzia Julai,2023 hadi Juni,2024, ofisi ya Ardhi Mkoa, imepokea na kusajili jumla ya miamala **1190** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki. Aidha, jumla ya Hati Milki **1,674** zimeandaliwa na kusajiliwa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 32: Kuonyesha idadi ya hati zilizoandaliwa na kusajiliwa kwa kila Halmashauri**

| NA | HALMASHAURI | IDADI YA HATI |
|---|---|---|
| 1 | Mbinga DC | 167 |
| 2 | MbingaTC | 290 |
| 3 | Songea MC | 650 |
| 4 | Namtumbo DC | 48 |
| 5 | Madaba DC | 56 |
| 6 | Songea DC | 224 |
| 7 | Nyasa DC | 52 |
| 8 | Tunduru DC | 187 |
| | **JUMLA** | **1674** |

#### 2.11.5 Uthamini

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya majedwali ya fidia **1,258** yameidhinishwa. Aidha jumla ya taarifa za uthamini **266** kwa ajili ya madhumuni mbalimbali ikiwemo uhamisho wa miliki, rehani na fidia zimeidhinishwa.

#### 2.11.6 Migogoro ya ardhi

Ofisi ya Ardhi Mkoa imepokea na kushughulikia migogoro ya Ardhi mbalimbali inayohusu mipaka ya Kijiji na Kijiji, mipaka ya Vijiji na maeneo ya Uhifadhi, migogoro ya mirathi, migogoro ya mtu na mtu n.k. kama iliivyoelezewa hapo chini.

i. **Migogoro ya Vijiji 975 iliyotolewa maamuzi na Baraza la Mawaziri**

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa iliyokuwa na migogoro ya vijiji 975 ambayo imefanyiwa kazi na Baraza la Mawaziri 8 wa kisekta. Kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma, kulikuwa na jumla ya migogoro 38 ambayo ilikuwa inahusu wananchi na maeneo ya hifadhi, migogoro ya fidia pamoja na uvamizi wa shamba la Serikali lililopo Namtumbo (NAFCO).

Baraza la Mawaziri lilifika Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kushughulikia migogoro husika na kutoa maamuzi juu ya migogoro hiyo. Kwa ujumla migogoro yote 38 imetatuliwa na kutolewa maelekezo. Maelekezo hayo yanaendelea kutekelezwa. Baadhi ya utekelezaji huo ni kuainisha mipaka ya hifadhi na vijiji, kumega eneo la msitu wa hifadhi na kurejesha kwa wananchi, kulipa fidia kwa wananchi zaidi ya

800 katika eneo la EPZA katika Halmashauri ya Manispa ya Songea, kupima upya vijiji na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Aidha, zoezi la kuwaondoa wananchi katika eneo la ushoroba katika kijiji cha Likusanguse Wilaya ya Namtumbo linaendelea kushughulikiwa.

**ii. Migogoro mingine ya ardhi inayoendelewa kushughulikiwa.**

Mkoa wa Ruvuma pia umekuwa na migogoro ya ardhi ya kawaida ikiwemo migogoro ya mirathi, migogoro baina ya mtu na mtu, migogoro ya milki ya ardhi. Ofisi ya Ardhi ya Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri zote imekuwa ikiendesha mazoezi ya kliniki za ardhi kwa ajili ya kushughulikia na kutatua migogoro ya ardhi mbapo jumla ya migogoro ya ardhi 86 imetatuliwa.

Katika kuhakikisha migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Ruvuma inaisha, Mhe. Mkuu wa Mkoa aliunda Timu maalumu ya kushughulikia migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Ruvuma, timu hiyo ilizinduliwa tarehe 18 Novemba, 2023 ambapo hadi sasa jumla ya migogoro 76 imeshughulikiwa.

### 2.11.7 Makusanyo ya maduhuli ya serikali

Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Ruvuma imeendelea kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya **Tshs. 1,180,729,876.94/=**

ziimekusanywa. Mikakati ya kuongeza makusanyo ya kodi ya Ardhi pamoja na maduhuli mengine yatokanayo na Ardhi ikiwemo kutoa elimu ya ulipaji kodi, kuandaa na kusambaza ankara za umilikishaji na kutoa Hati za madai ya kodi inaendelea katika Halmashauri zote kama ilivyoelekezwa na Wizara.

**2.11.8 Mradi wa uboreshaji wa milki salama Tanzania (Land Tenure Improvement Project - LTIP)**

Mkoa wa Ruvuma umebahatika kuwa miongoni mwa mikoa iliyofaidika na mradi wa uboreshaji milki salama nchini unaoendeshwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mradi huu unafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Mbinga.

**2.11.9 Mradi wa uboreshaji wa milki salama katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga**

Lengo la mradi huu ni kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa wananchi waliopo katika vijiji 103 vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Mradi huu unatarajia kufanikisha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 103 na kutoa Hati milki za kimila 44,000 kwa wananchi wa Halmashauri hiyo.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2024 mradi umeshafanya utekelezaji katika maeneo muhimu yafuatayo;

i. Kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi wa Wilaya ya

Mbinga (District Land Use Framework Project - DLUFP).

ii. Kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 58
iii. Migogoro ya mipaka ya vijiji 51 imetatuliwa
iv. Mipaka ya vijiji 52 imehuishwa na kupimwa upya
v. Vipande vya ardhi 55,939 vimetambuliwa na kupandishwa kwenye mfumo wa ILMIS
vi. Jumla ya Hatimiliki za kimila 3,266 zimesajiliwa katika mfumo wa ILMIS
vii. Mipango kina ya vitovu ya vijiji nane (08) imefanyika
viii. Elimu ya sheria za ardhi, Mazingira na Utawala kwa vijiji 58 imetolewa.

**2.11.10 Mradi wa Uboreshaji wa milki salama katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea**

Lengo la mradi huu ni kuongeza usalama wa milki za ardhi katika Kata ya Peramiho kwa vijiji vya Peramiho “A”, Peramiho “B”, Lundusi na Nguvumoja; Kata ya Parangu kwa Kijiji cha Parangu; Kata ya Litisha kwa Kijiji cha Morogoro; na Kata ya Maposeni katika Kijiji cha Maposeni. Zoezi hili linatekelezwa kwa kuzingatia makundi na jinsia zote kupitia urasimishaji wa makazi yasiyopangwa Mijini. Kwa ujumla mradi unatarajia kupanga, kupima na kumilikisha jumla ya viwanja 10,000.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2024 mradi umeshafanya utekelezaji katika maeneo muhimu yafuatayo;

i. Jumla ya wananchi 3,155, vikundi rika 1,687 na wadau 59

wamehamasishwa na kupewa elimu juu ya umuhimu wa ushiriki katika mradi wa Uboreshaji Milki Salama

ii. Jumla ya vipande vya ardhi 9,951 vimetambuliwa na kupandishwa kwenye mfumo wa ILMIS.
iii. Uandaaji wa Michoro ya Mipangomiji unaendelea ambao hadi sasa jumla ya viwanja 18,840 vyenye matumizi mbalimbali vimeshapangwa
iv. Jumla ya viwanja vilivyopimwa kwa kuwekewa alama ardhini ni 9,470 na
v. Jumla ya migogoro ya ardhi 110 imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

**2.11.11 Changamoto na mikakati ya kutatua changamoto**

Pamoja na jitihada ambazo zimekuwa zikiendelea kufanyika ili kuboresha huduma mbalimbali za ardhi kwa wananchi, bado kuna changamoto mbalimmbali ambazo Ofisi imekuwa ikikumbana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo pamoja na mikakati ya kutatua changamoto hizo ni kama ifuatavyo;-

i. Kutokuwepo kwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika Wilaya ya Nyasa na Namtumbo.

   Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa sasa ipo katika maandalizi ya uanzishwaji wa baraza la Ardhi katika Wilaya ya Namtumbo ambapo wajumbe wa mabaraza hayo wameshateuliwa, aidha Baraza la Wilaya

ya Nyasa wajumbe wake wapo katika hatua ya kutangazwa.

ii. Upungufu wa watalaam wa fani mbalimbali katika Halmashauri zilizopo Mkoa wa Ruvuma.

    Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma zina upungufu wa wataalam wa fani mbalimbali na kupelekea changamoto katika utekelezaji wa kazi mbalimbali. Katika kutatua changamoto hiyo, Ofisi imekuwa ikiunda timu maalumu ambazo zimekuwa zikizunguka katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi.

iii. Migogoro ya ardhi kufikishwa katika vyombo vya mahakama.

    Baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwasilisha malalamiko ya ardhi ambayo yapo mahakamani au yameshatolewa maamuzi na vyombo vya mahakama. Aidha, wananachi hawa wamekuwa wakishauriwa kuendelea na hatua za kukata rufaa au kuendelea kusikiliza mashauri yaliyopo mahakamani.

## 2.12 Ujenzi - Barabara -TANROADS

### A. Utangulizi

Serikali kupitia Wakala ya Barabara (TANROADS) inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa miundombinu ya Barabara na Madaraja mkoani Ruvuma inaimarishwa ili kurahisisha shughuli

za usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kuinua Uchumi na kupunguza Umaskini.

TANROADS mkoa wa Ruvuma ina jukumu la kusimamia matengenezo ya mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 2,166.62. Kati ya hizo barabara kuu zikiwa na Kilomita 920.98 ambapo kilomita 702.60 ni za kiwango cha lami na 218.34 ni za kiwango cha changarawe. Urefu unaobaki wa Kilomita 1,245.64 ni wa barabara za mkoa ambapo Kilomita 31.34 ni za lami na 1,214.21 ni za changarawe.

### 2.12.1 Muhtasari wa bajeti iliyoidhdinishwa kwa mwaka 2023/24

Katika kutimiza majukumu yake Wakala inatekeleza miradi ya aina ifuatayo:

(i.) Miradi mikubwa ya Maendeleo,
(ii.) Miradi midogo ya Maendeleo na
(iii.) Miradi ya matengenezo ya Barabara na Madaraja.

Miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo ile inayofadhiliwa na Serikali au Wadau wa Maendeleo inatekelezwa kwa bajeti inayosimamiwa kupitia Makao Makuu ya Wakala.

**Jedwali Na. 33: Miradi midogo ya Maendeleo na ya Matengenezo inatekelezwa kupitia Ofisi ya Meneja kwa mwaka wa Fedha 2023/24**

| Aina ya Miradi | Idadi ya Mikataba | Bajeti (TShs. Billioni) | Fedha zilizopokelewa (TShs. Billioni) |
|---|---|---|---|
| Miradi midogo ya Maendeleo | 6 | 4.112 | 2.545 |
| Miradi ya Matengenezo ya barabara na Madaraja | 47 | 17.964 | 9.372 |
| **Jumla** | **53** | **22.076** | **11.917** |

### 2.12.2 Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi

Shughuli za taasisi zilizotekelezwa na mafanikio yaliyopatikana

Hadi kufikia mwezi Julai 2024 Wakala ya Barabara Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kukamilisha Miradi mikubwa ya Maendeleo kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 34: Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi na mafanikio**

| Na. | Mradi Husika | Mafanikio |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Barabara ya Mbinga – Mbamba bay | Wakala imefanikiwa kukamilisha Ujenzi wa Barabara hii yenye urefu wa Km 66 kwa kiwango cha lami |
| 2. | Ujenzi wa Daraja la Ruhuhu | Wakala imefanikiwa kukamilisha Ujenzi wa Daraja la hili |
| 3. | Ukarabati na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Songea | Wakala imefanikiwa kukamilisha Ukarabati huu. |
| 4. | Ujenzi wa Barabara ya Kitai -Lituhi - Ndumbi | Wakala imefanikiwa kukamilisha Ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango Cha lami kwa Km 5 (Kitai – Amani Makoro) |
| 5. | Ujenzi wa Barabara ya Mbamba bay – Lituhi | Wakala imefanikiwa kukamilisha Usanifu wa Kina wa Barabara hii yenye Urefu wa Km 112.4 na Ujenzi wa Km 10 (Lituhi – Ndumbi Port) uko katika hatua ya Utekelezaji |
| 6. | Ujenzi wa barabara ya Mtwarapachani – Nalasi – Tunduru | Wakala imefanikiwa kukamilisha Usanifu wa Kina wa Barabara hii yenye Urefu wa Km 300. Serikali inaendelea na Juhudi za kutafua fedha ili kutekeleza ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami |
| 7. | Ujenzi wa Barabara ya Madaba – Mundindi (Liganga) – Mkiu | Wakala imefanikiwa kukamilisha Usanifu wa Kina wa Barabara hii yenye Urefu wa Km 46. Serikali inaendelea na Juhudi za kutafua fedha ili kutekeleza ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami |
| 8. | Ujenzi wa Barabara ya Unyoni – Maguu – Kipapa | Wakala imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Kilomita 4.2 kwa kiwango cha |

| Na. | Mradi Husika | Mafanikio |
|---|---|---|
| | | lami kwa kutumia fedha za miradi ya maendeleo. Serikali inaendelea na Juhudi za kutafua fedha ili kutekeleza Usanifu wa Barabara hii. |
| 9. | Matengenezo ya Barabara na Madaraja kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 | Pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Ofisi ya Meneja Wakala ya Barabara Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kuendelea kufanya Matengenezo ya Barabara na Madaraja kila Mwaka.<br>Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Jumla ya TZS 17.964 Bilioni zimetumika kwa ajili ya kufanya Matengenezo ya kawaida, Muda maalumu, Sehemu Korofi na Madaraja ili kuhakikisha Barabara zote zinapitika kipindi chote cha mwaka. Hivyo kuwezesha shughuli za Kijamii na za Maendeleo kufanyika bila bikwazo. |

## Jedwali Na. 35: Miradi ya maendeleo inayoendelea

| Na | Jina la Mradi | Mradi husika kwa kifupi | Hatua ya utekelezaji | Maelekezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Amani Makoro - Ruanda (km 35) | Mradi huu ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara ya Kitai -Lituhi - Kipingu. Ujenzi huu unatekelezwa kwa kujenga Kilomita 35 kwa kiwango cha lami kipande cha Amani Makoro - Ruanda. Mradi ulianza tarehe 15 Juni 2022 na ulitegemewa kukamilika mnamo Aprili 2024, Mkandarasi ni kampuni ya China Railway Seventh Group, gharama ya mradi ni TZS TZS 60.481 Bilioni. Mhandisi mshauri wa mradi ni kampuni ya LEA Associates South Asia Pvt Ltd. | Utekelezaji wa mradi kwa hivi sasa umefikia 28%. | Mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa mradi huu.<br>Aidha mradi haujakamilika kutokana na uzembe wa Mkandarasi. Hivi sasa TANROADS inapitia maombi ya Mkandarasi ya kuongezewa muda baada ya muda wa nyongeza wa awali wa mwezi Agosti kukaribia kuisha. |

| Na | Jina la Mradi | Mradi husika kwa kifupi | Hatua ya utekelezaji | Maelekezo |
|---|---|---|---|---|
| **2.** | Ujenzi Kiwango cha Lami Barabara ya Ruanda – Lituhi – Ndumbi (Km 50) | Barabara hii itaanzia eneo la Ruanda hadi bandari ya Ndumbi. Yenye urefu wa Kilomita 50. Tarehe 13 Machi 2024 Serikali kupitia Wakala ya Barabara Tanzania iliingia mkataba na mkandarasi kampuni ya *China First Highway Engineering Group Co. Ltd*. Mradi utatekelezwa kwa gharama ya TShs. 95,756,992,529.58 kwa muda wa miezi 28 hivyo kutarajiwa kumalizika mwezi Juni 2026 endapo hakutokuwa na mabadiliko yoyote. | Hivi sasa mkandarasi yupo katika maandalizi ya awali ya kimkataba kwa ajili ya kuanza kazi. | Taarifa ya Uthamini wa Fidia kwa waathiriwa na mali zao ya kiasi cha takribani TSh. 2.9 Billioni imeshawekwa wazi kwa waathiriwa na sasa inaandaliwa kuwasilishwa makao makuu ya TANROADS kwa ajili ya mchakato wa kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua zaidi za upatikanaji wa fedha. |
| **3.** | Ujenzi wa barabara ya Likuyufusi hadi Mkenda | Barabara hii ina urefu wa Kilomita 124. Usanifu wake kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ulifanyika mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na muda mrefu kupita usanifu huo ulifanyiwa marejeo na TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU) kwa gharama ya Tsh 178 Milioni na kazi hiyo kukamilika Desemba 2020. | Tathmini ya zabuni za wakandarasi ilikamilika na Serikali hivi karibuni kupitia Waziri mwenye dhamana Mhe. Innocent Bashungwa imetoa kibali cha utekelezaji wa mradi huu.<br>Kwa sasa mkandarasi wa kutekeleza mradi huu ameshapatikana na Wakala ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba. | Taarifa ya Uthamini wa Fidia kwa waathiriwa na mali zao ya kiasi cha TSh. 5,198,353,724.16 imeshawasilishwa makao makuu ya TANROADS kwa ajili ya mchakato wa kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua zaidi za upatikanaji wa fedha. |
| **4.** | Ujenzi wa Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa | Mradi huu ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Malinyi Kilosa | Serikali tayari imewekeana saini na mkandarasi China | Hivi sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya |

| Na | Jina la Mradi | Mradi husika kwa kifupi | Hatua ya utekelezaji | Maelekezo |
|---|---|---|---|---|
| | kwa Mpepo – Londo – Kitanda - Lumecha | kwa Mpepo – Londo – Lumecha yenye jumla ya Kilomita 512 ambayo inaunganisha mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Serikali imeshaanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mkoa wa Morogoro kuanzia Kidatu – Ifakara (66.9Km) kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya. | Civil Engineering Construction Corporation Ltd (CCECC) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea Kilomita 512 kwa ajili ya kuijenga kwa kutumia mfumo wa EPC+F. Mradi huu utakuwa wa muda wa miezi 66. Katika ujenzi huu Kilomita 123.93 kuanzia Londo (mpaka na Mkoa wa Morogoro) – Lumecha zipo mkoa wa Ruvuma. | kukamilisha upatikanaji wa dhamana za benki kabla ya kukabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya utekelezaji. |
| **5.** | Ujenzi wa Barabara ya Songea – Lutukira | Mradi huu ni wa Kilomita 116 ambapo utahusisha kipande cha Songea – Lutukira Kilomita 100 pamoja na kipande cha Songea *bypass* Kilomita 16. Upembuzi yakinifu, na usanifu wa kina wa awali ulifanywa na Mhandisi Mshauri BEOMAN Engineering and Architect Co. Ltd na kukamilika mwaka 2014. | Serikali imefanikiwa kupata ufadhili wa benki ya dunia kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi huu. Kutokana na muda mrefu kupita Serikali ilitangaza manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya Usanifu wa Kina pamoja na kusimamia utekelezaji wa | Sambamba na hilo hivi sasa Wizara ya Fedha ipo katika hatua ya kutafuta Fidia kwa waathiriwa yenye thamani ya kiasi cha TSh. 646,964,536.20 kwa upande wa barabara ya Songea – Lutukira na TSh. 4,005,567,798.36 kwa upande wa Songea *Bypass*. |

| Na | Jina la Mradi | Mradi husika kwa kifupi | Hatua ya utekelezaji | Maelekezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | ujenzi wa mradi tarehe 17 Februari 2023 na hivi sasa mchakato upo katika hatua za mwisho. Hali kadhalika Serikali ilitangaza zabuni ya kutafuta mkandarasi tarehe 30 Novemba 2023 na kufunguliwa 28 Februari 2024. Hivi sasa hatua za kupitia zabuni zinaendelea. | |
| **6.** | Ujenzi wa Daraja la Mitomoni | Daraja hili litawezesha magari kuvuka Mto Mitomoni na hivyo kuunganisha wilaya za Nyasa na Songea (Vijijini). Daraja hili lilishafanyiwa usanifu na kampuni ya Advanced Engineering Solutions na kukamilishwa tarehe 3 Machi 2020. Daraja hili limesanifiwa kuwa na urefu wa mita 47.7, njia mbili za magari na njia za waenda kwa miguu kila upande zenye upana wa mita 1.9 kila moja. | Zabuni ya ujenzi wa daraja hili ilitangazwa tarehe 15 Desemba 2022 na kufunguliwa tarehe 17 Januari 2023. Hata hivyo, kutokana na kujitokeza kwa mzabuni mmoja pekee na ambaye zabuni yake ilikuwa juu ya makadirio Ofisi ya Meneja baada ya kushauriana na TANROADS Makao Makuu ilishauriwa kuitangaza upya zabuni hii, kwa sasa kazi hii ipo katika hatua za manunuzi. | Ujenzi wa Daraja hili utafanyika katika eneo ambalo ni la hifadhi ya barabara na hivyo halitohusisha wananchi kuathiriwa na kupoteza mali zao. |
| **7.** | Ujenzi wa Daraja la | Daraja hili linaunganisha nchi ya Tanzania | Zabuni ya ujenzi wa daraja | Ujenzi wa Daraja hili utafanyika |

| Na | Jina la Mradi | Mradi husika kwa kifupi | Hatua ya utekelezaji | Maelekezo |
|---|---|---|---|---|
| | Mkenda | na Msumbiji katika mto Ruvuma. Daraja hili lilishafanyiwa usanifu na kampuni ya Advanced Engineering Solutions na kukamilishwa tarehe 3 Machi 2020. Daraja hili litakuwa na urefu wa mita 144, njia ya magari kuelekea kila upande na njia za waenda kwa miguu. | hili ilitangazwa tarehe 15 Desemba 2022 na kufunguliwa tarehe 17 Januari 2023.Hata hivyo, kutokana na kujitokeza kwa mzabuni mmoja pekee na ambaye zabuni yake ilikuwa juu ya makadirio Ofisi ya Meneja baada ya kushauriana na TANROADS Makao Makuu ilishauriwa kuitangaza upya zabuni hii, kwa sasa kazi hii ipo katika hatua za manunuzi. | katika eneo ambalo ni la hifadhi ya barabara na hivyo halitohusisha wananchi kuathiriwa na kupoteza mali zao |
| **8.** | Usanifu wa Barabara ya (Nangombo – Chiwindi, Mbinga – Litembo na Chiwindi - Lumesule) | Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unafanywa na mhandisi mshauri M/s Crowntech kwa Barabara za Nangombo – Chiwindi na Mbinga – Litembo na Chiwindi – Lumesule. | Mhandis mshauri ameshasaini mkataba na yuko katika hatua za utekelezaji | Mhandisi Mshauri ameshaanza utekelezaji. |

### 2.12.3 Changamoto

Katika kutekeleza miradi hiyo pia pana changamoto mbalimbali ambazo Wakala inakabiliana nazo kama zinavyoainishwa hapa chini.

**Jedwali Na. 36: Changamoto katika utekelezaji wa Miradi ya Barabara na utatuzi wake**

| | Changamoto | Utatuzi |
|---|---|---|
| **A.** | **Miradi ya Kitaifa** | |
| 1. | Kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi wanaotekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya kitaifa. Jambo linalosababisha utekelezaji wa baadhi ya miradi kusuasua au hata kusimama kabisa.<br>Mfano: *mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani – Makoro.* | Serikali kuwalipa makandarasi kwa wakati ili kuwezesha kutekelezwa miradi kwa wakati na pia kuepuka kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mradi. |
| 2. | Kuchelewa kutekelezwa kwa miradi iliyopewa kibali cha kufanyiwa Usanifu na taarifa zake kukamilika.<br>*Mfano:*<br>• *Ujenzi wa barabara ya Mtwarapachani – Nalasi – Tunduru*<br>• *Ujenzi wa barabara ya Mbambabay - Lituhi* | Serikali kuandaa vyema mpango kazi wake wa utekelezaji wa miradi ya kitaifa. |
| 3. | Mlolongo mrefu unaohusisha taasisi mbalimbali wa ufanyaji wa zoezi la uthamini hadi ulipwaji wa fidia kwa wananchi. Jambo linalosababisha manung’uniko kwa wananchi na hata wakati mwingine kusababisha zoezi la uthamini kurudiwa. | Serikali kupitia utaratibu wa uthamini ili ufanyike baada ya kupatikana kwa uthibitisho wa uwepo wa fungu na si baada ya ripoti ya uthamini kuandaliwa. |
| **B.** | **Miradi ya Matengenezo ya Mkoa** | |

| | Changamoto | Utatuzi |
|---|---|---|
| 4. | Fedha pungufu inayotolewa ikilinganishwa na Gharama/ mahitaji halisi ya fedha za matengenezo na ukarabati zinazohitajika. | Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya matengenezo.<br>Kutoa vipaumbele kwa maeneo yenye uhitaji zaidi. |
| 5. | Hujuma za alama za barabarani, vyuma vya madaraja/ makalvati, na utupaji ovyo wa taka unaosababisha uchafuzi wa mazingira ikiwemo na kuziba kwa mitaro na makalavati. | Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa barabara juu ya utunzaji wa rasilimali za barabara ili kusaidia kutunza miundombinu ya barabara na mazingira kwa ujumla. |
| 6. | Uvamizi wa hifadhi ya barabara | Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya hifadhi ya barabara ili kukabiliana na tatizo hilo.<br>Wakala hivi sasa imeunda kikosi katika ofisi za mikoa mahsusi kwa ajili ya kusimamia maeneo ya hifadhi ya barabara ili kuendesha ukaguzi wa kudumu wa hifadhi ya barabara na kubaini mapema wavamizi na kuchukua hatua stahiki.<br>Ofisi ya meneja pia inaendelea na kuweka vigingi vinavyoonesha mwisho wa hifadhi ya barabara katika barabara zote zilizopo katika mtandao wake kadiri ya upatikanaji wa fungu. |
| 7. | Uwepo wa magari mazito kupita kiasi kwenye barabara jambo linalosababisha kuharibika mapema kwa barabara | Kuwepo kwa mizani za kudumu, kumefanikisha udhibiti wa mizigo mikubwa katika barabara zetu. Aidha, elimu kwa watumiaji wa barabara na utekelezaji wa sheria kumeongeza ufahamu wa mizigo inayostahili kwenye barabara zetu. |
| 8. | Umwagaji makaa ya mawe kwenye hifadhi ya barabara | Kuelimisha wasafirishaji juu ya usafirishaji wa makaa unaotunza mazingira ya barabara na mengine kwa ujumla.<br>Ukaguzi wa barabara mara kwa mara kuweza kubaini wasafirishaji wanaomwaga makaa katika hifadhi. |

| | Changamoto | Utatuzi |
|---|---|---|
| **C.** | **Miradi ya Maendeleo ya Mkoa** | |
| 9. | Kucheleweshwa kutolewa kwa mafungu yake jambo linalosababisha kusuasua kwa utekelezaji wake pamoja na kudhoofisha wakandarasi wa ndani wanaofanya kazi hizo.<br>Kufifisha mwitikio wa wakandarasi katika kazi hizi kutokana na mwenendo usioridhisha wa malipo yake. | |

**Hitimisho**

Wakala ya Barabara mkoa wa Ruvuma itaendelea na juhudi za kuhakikisha malengo ya Serikali katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi yanafikiwa kadiri ya mipango ya Serikali.

## 2.13 Ujenzi - Barabara – TARURA

### A. Utangulizi

Wakala wa Barabaraza Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma una mtandao wa barabara wa jumla ya kilometa **7146.21** kati ya hizo kilometa **2312.83** ni za Mjazio (Feeder Roads) ambazo ni sawa na asilimia **32.36%, 3873.85** ni za Mkusanyo (Collector Roads) ambazo ni sawa na asilimia 54.21%, na Kilometa 959.52 ni za Jamii/Kijiji (Community Roads) ambazo ni sawa na asilimia 13.43% ya mtandao mzima.

TARURA Mkoa wa Ruvuma inahudumia Halmashauri nane (8) ambazo ni Songea Manispaa ambayo ina mtandao wa barabara wa kilometa **513.65**, wilaya ya Songea Vijijini ina mtandao wa

barabara wa kilometa **1,057.24**, Halmashauri ya Madaba ina mtandao wa barabara wa kilometa **629.69**, Wilaya ya Namtumbo ina mtandao wa barabara wa kilometa **975.25**, wilaya ya Mbinga Mji ina mtandao wa barabara wa kilometa **1063.51**.

Wilaya ya Mbinga Vijijini ina mtandao wa barabara wa kilometa **973.340**, wilaya ya Nyasa ina mtandao wa barabara wa kilometa 729.91 na wilaya ya Tunduru ambayo ina mtandao wa barabara wa kilometa 1203.61 katika hali ya kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya barabara na madaraja.

**B. Hali ya Mtandao wa Barabara**

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma una jumla ya km **124.53** za kiwango cha Lami sawa na asilimia 1.74% ya mtandao mzima, Changarawe km 1478.382 ambayo ni sawa na asilimia 20.69%. Barabara za udongo km 5543.287 sawa na asilimia 77.57% ya mtandao mzima wa Barabara, madaraja 306, Makalvati 531, Madrifti 14, mifreji mita 6912. Aidha imefunguliwa barabara mpya kilomita 392.7. Taa za barabarani 383. Mpaka sasa mtandao wa barabara hizi unapitikwa kwa zaidi ya asilimia 64.4%.

**C. Utekelezaji wa miradi ya kazi za ujenzi, matengenezo ya barabara na madaraja kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

### i. Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024

Kwa mwaka wa fedha **2023/ 2024**, Mkoa wa Ruvuma katika bajeti ya miundombinu ya barabara uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 22,616,712,196** ambapo Mfuko wa Barabara ni **Shilingi. 7,917,264,689.00** Mfuko wa Barabara (Maendeleo) **Shilingi. 200,000,000** Mfuko Mkuu wa Serikali (kila Jimbo) **Shilingi**. **4,500,000,000** na fedha tozo ya mafuta Shilingi 100 kwa lita **Shilingi. 9,999,447,506.00**; kwa mantiki hiyo fedha za nyongeza ya bajeti ni **Shilingi. 14,499,447,506.41** kama inavyojieleza katika jedwali Na.37.

**Jedwali Na. 37: Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24**

| S/N | Halmashauri | Bajeti ya Matengenezo | Bajeti ya Maendeleo. | Bajeti Nyongeza |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea MC | 1,207,143,478 | | 1,500,000,000 |
| 2 | Songea DC | 970,670,784 | | 2,000,000,000 |
| 3 | Madaba DC | 675,641,684 | | 1,500,000,000 |
| 4 | Mbinga DC | 831,543,784 | 200,000,000,00 | 1,849,447,506 |
| 5 | Mbinga TC | 879,905,527 | | 1,500,000,000 |
| 6 | Namtumbo DC | 1,116,513,478 | | 1,500,000,000 |
| 7 | Nyasa DC | 937,373,478 | | 1,500,000,000 |
| 8 | Tunduru DC | 1,116,783,784 | | 3,000,000,000 |
| | **Jumla** | **7,735,575,997.00** | **200,000,000.00** | **14,349,447,506.00** |

### ii. Mapokezi ya Fedha

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Juni 2024, Wakala wa barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma umepokea jumla ya fedha kiasi cha **Tshs**. **10,530,821,430.80**

ambayo ni asilimia **46.56** ya bajeti nzima ya matengenezo ya barabara na fedha za Maendeleo.

**iii. Hali ya utekelezaji wa miradi ya Barabara kupitia fedha za mfuko wa Barabara (Road Fund)**

Hadi kufikia Juni, 2024 ya mwaka wa fedha 2023/2024, TARURA Mkoa wa Ruvuma umefanya Matengenezo ya barabara ya Kawaida yenye urefu wa kilometa 366.1 sawa na asilimia **73.8**, Matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa Kilometa 125.20 sawa na asilimia **98** ya utekelezaji, Matengenezo ya Muda Maalum yenye urefu wa Kilometa 111.49 sawa na asilimia **75.4** ya utekelezaji. Madaraja na Makalvati yamejengwa sawa na asilimia 65 ya utekelezaji.

**iv. Hali ya utekelezaji wa miradi ya Barabara kupitia fedha za Maendeleo (Fedha za Jimbo na Tozo)**

Hadi kufikia Juni, 2024 ya mwaka wa fedha 2023/24, TARURA Mkoa wa Ruvuma kupitia fedha za mfuko wa maendeleo unaendelea kufanya kazi za matengenezo ya barabara kilomita **7.54** zinajengwa kwa kiwango cha lami; matengenezo ya barabara kwa kiwango cha changarawe kilomita **267.60** ambazo utekelezaji wake umefikia asilimia **75.5** na madaraja **18** yamejengwa utekelezaji wake umefikia asilimia **80**. Jedwali Na 38 linaonesha mchanganuo wa kilometa zilizotengenezwa kwa ujumla kwa kila Halmashauri.

**Jedwali Na. 38: Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Mwaka wa Fedha 2023-2024 kwa Kila Halmashauri kwa Vyanzo Mbalimbali Mkoa wa Ruvuma**

| S/N | Halmashauri | Barabara ya rami | | Matengenezo ya mara kwa mara | | Matengenezo ya sehemu korofi | | Matengezo ya kipindi maalum | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mpango (km) | Utekelezaji (km) | Mpango (km) | Utekelezaji (km) | Mpango (km) | Utekelezaji (km) | Mpango (km) | Utekelezaji (km) |
| 1 | Madaba Dc | 1.10 | 1.10 | 3.00 | 3.00 | 2.20 | 0.50 | 59.89 | 46.80 |
| 2 | Mbinga Dc | 1.00 | 1.00 | 40.66 | 32.50 | 5.00 | 5.00 | 23.30 | 18.30 |
| 3 | Mbinga Tc | 1.70 | 1.70 | 8.38 | 5.00 | 10.10 | 6.10 | 66.24 | 51.90 |
| 4 | Namtumbo Dc | 1.00 | 1.00 | 103.49 | 93.50 | 0 | 0 | 72.49 | 35.70 |
| 5 | Nyasa Dc | 0.80 | 0.80 | 34.05 | 21.00 | 17.47 | 13.77 | 52.90 | 14.00 |
| 6 | Songea Dc | 2.00 | 2.00 | 74.10 | 54.00 | 15.00 | 15.00 | 47.02 | 41.09 |
| 7 | Songea Mc | 2.00 | 2.00 | 199.33 | 135.00 | 38.23 | 15.00 | 16.50 | 3.00 |
| 8 | Tunduru Dc | 2.14 | 0 | 33.21 | 22.10 | 39.57 | 22.60 | 152.40 | 117.40 |
| | **Total (km)** | **11.74** | **9.60** | **496.22** | **366.10** | **127.57** | **77.97** | **490.74** | **328.19** |

**D. Changamoto zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa miradi**

- Mvua nyingi zilizonyesha kwenye mkoa wetu na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara.
- Upungufu wa watumishi
- Upungufu wa vitendea kazi hususani Magari
- Uharibifu wa miundombinu ya Barabara na Madaraja uliotokana na mvua za El nino ambapo hadi sasa uharibifu huo unakadiriwa kufikia jumla ya **Tsh 2,565,798,500** ukihusisha vivuko, Madaraja na maungio ya Madaraja yaliyozolewa na mvua.

**E. Mikakati Iliyopangwa kuendelea kuboresha hali nzuri za miundombinu kwa kutatua changamoto/kero za wananchi**

TARURA Mkoa wa Ruvuma umejiwekea mikakati ya kuendelea kuboresha hali ya miundombinu ya barabara kwa lengo la kutatua changamoto au kero wanazokumbana nazo wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, mikakati hiyo ni kama ifuatayo: -

- Kuondoa vikwazo vya barabara (bottle necks) hasa ujenzi wa madaraja na makalavati yaliyoharibiwa na mvua nyingi zilizonyesha.
- Kuendelea kuwasilisha kwa Mtendaji mkuu maombi ya kuongezewa watumishi pamoja na vitendea kazi hususani magari.
- Kuhakikisha bajeti iliyopitishwa na serikali inatekelezwa na kukamilika ndani ya muda uliopangwa

- Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami katika miji na makao makuu ya kila wilaya
- Kufungua barabara mpya kupitia fedha za Tozo katika maeneo ya uwekezaji mkubwa wa sekta ya Kilimo na uchimbaji wa makaa ya mawe;
- Kuendeleza barabara za mitaa kwa kiwango cha changarawe;
- Kuweka taa katika mitaa mbalimbali kwenye maeneo ya miji;

**F. Hitimisho**

Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma tunampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza kwa mafanikio hasa katika sekta ya Miundombinu na kuondoa vikwazo vya usafiri na usafirishaji wa mazao vijijini na kwa kipekee kwa kuongeza fedha kupitia Mfuko wa Majimbo na fedha za Tozo za mafuta ya petrol na dizeli kwa kufanya hivyo kumetuongezea ufanisi zaidi kwenye utekelezaji wa miradi na pia kusaidia kuinua uchumi kwa wananchi wa kawaida hasa wakulima kwa kuweza kusafirisha mazao yao kwa urahisi kuyafikia masoko na hatimaye kukidhi mahitaji yao kwa urahisi. Tunaomba TARURA iendelee kuwezeshwa ili tuweze kutimiza kauli mbiu yetu isemayo

"***Tunakufungulia Barabara kufika kusiko fikika***"

## 2.14 Mawasiliano na Uchukuzi

Mawasiliano na uchukuzi kama ilivyo barabara, ni muhimu katika kipindi hiki cha ushindani wa kibiashara kwa lengo la kukuza uchumi. Huduma ya mawasiliano hutolewa na shirika la Posta na makampuni binafsi katika usafirishaji wa barua, vifurushi na fedha kwa njia ya kawaida na haraka.

Sambamba na huduma zitolewazo na kampuni ya simu hapa Mkoani, yapo makampuni binafsi yanayotoa huduma ya simu za mkononi. Makampuni hayo ni Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel na Halotel. Huduma za simu zimeboresha hali ya mawasiliano ya wananchi walio wengi ndani ya Mkoa.

Aidha, huduma za simu zinatumika pia kwenye masuala ya kifedha na benk hali ambayo imesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa usumbufu kwa wananchi hasa wa vijijini katika kutuma na kupokea fedha kwa haraka.

Mkoa pia una vituo vya Redio, Kimoja kikiwa mali ya Serikali (TBC) na vituo vya binafsi ni Redio Maria ya Kanisa Katoliki, Redio Free Africa (RFA), Redio Jogoo FM, KEY fm, Ruvuma fm. Mkoa unaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuleta mapinduzi ya upashanaji habari.

## 2.15 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania Bandari.

### A. Utangulizi

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inasimamia Bandari 15 katika Bandari za ziwa Nyasa na Bandari ya Itungi ni makao makuu ya bandari zote za ziwa Nyasa upande wa Tanzania. Bandari hizo 15 zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Mkoani Mbeya katika Wilaya ya Kyela kuna Bandari tatu (3) za Itungi, Kiwira na Matema, Mkoani Njombe katika Wilaya ya Ludewa kuna Bandari sita (6) za Lumbila, Ifungu, Nsisi, Makonde, Lupingu na Manda, na Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa kuna Bandari sita (6) za Ndumbi, Lundu, Nkili, Njambe, Liuli na Mbamba Bay.

### 2.15.1 Utekelezaji wa shughuli za Bandari za ziwa Nyasa kuanzia Julai 2023 - Juni 2024.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Juni 2024 kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka imeendelea kutekeleza shughuli za bandari ambazo ni kupakia na kupakua mizigo melini pamoja na kuhudumia abiria kupitia Bandari zote za ziwa Nyasa.

### 2.15.2 Shehena (mizigo na mibiria) Kwa kipindi cha Julai, 2023 - Juni 2024

Shehena (mizigo na abiria) iliyohudumiwa katika Bandari ya ziwa Nyasa ni jumla ya tani 2,491 na kusafirisha abiria 15,017.

### 2.15.3 Changamoto Zilizopo na Mapendekezo ya Kuziondoa

Pamoja na mafanikio kidogo yaliyopatikana kuna changamoto chache ambazo zikiondolewa, kazi ya kuhudumia abiria na mizigo kati ya nchi zetu mbili (Tanzania na Malawi) itakuwa na ufanisi mkubwa. Changamoto zilizopo na mapendekezo ya kuziondoa ni kama inavyoonekana kwenye **bango kitita** linalofuata.

**Jedwali Na. 39: Changamoto zilizopo na mapendekezo ya Kuziondoa**

| Na | Changamoto | Mapendekezo ya Namna ya Kuziondoa |
|---|---|---|
| 1. | Bandari za Malawi hasa bandari ya Nkata Bay kutoridhia meli zetu za Mizigo ziende katika bandari hiyo. Wateja kadhaa tuliopata wanataka kusafirisha mizigo (Gypsum na Makaa ya mawe) kwenda bandari ya Nkata Bay. | i) TPA inaendelea kuwasiliana na mmliki wa Bandari za Malawi ili kupata ufumbuzi wa suala hilo.<br>ii) TPA imekutana na Mheshimiwa Andrew Kumwenda, Balozi wa Malawi nchini Tanzania akiwa Kyela na kufanya naye mazungumzo na kumuomba aongee na Serikali ya Malawi, ambapo Mhe. Balozi amelipokea ombi letu na kuahidi kulifanyia kazi baada ya kufika Dar Es Salaam.<br>iii) Ubalozi wa Tanzania nchini Malawi wanaendelea kuwasiliana na Serikali ya Malawi ili meli zetu ziruhusiwe kwenda kwenye bandari za Malawi. |

### Hitimisho

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania inatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri, na msukumo wake juu ya kuendelea kuboresha Bandari za Tanzania zikiwemo Bandari za Ziwa Nyasa.

Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu kila anapotoa maelekezo juu

ya uboreshaji wa Bandari zetu, mara moja hutoa fedha kwa ajili ya kuyatekeleza maelekezo hayo.

### 2.16 Usafiri wa anga

### 2.16.1 Miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Kiwanja cha ndege cha Songea ni mojawapo ya viwanja vya ndege 58 vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiwanja hiki kilijengwa kati ya mwaka 1974 hadi 1980, kikiwa na barabara ya kutua na kurukia ndege kwa kiwango cha changarawe iliyokuwa na urefu wa mita 1600 na upana wa mita 30. Lengo kuu la ujenzi wa kiwanja hiki ilikuwa ni kuhudumia ndege ndogo na abiria wachache hivyo miundo mbinu yake ililenga kuhudumia abiria wachache.

Mnamo mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ilitenga fedha kwa ajili ya Ukarabati wa jengo lilokuwa likitumika na mkandarasi mshauri ili liweze kutumika kama jengo la abiria (*Remodeling of engineer's office into the terminal building)* mradi ulilenga kazi zifuatazo;

Kukarabati eneo la ukumbi wa kuondokea abiria (Depature lounge) ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 145 kwa wakati mmoja pamoja na kuboresha ukumbi wa kuwasili abiria

(Arrival lounge), kutengeneza maegesho ya magari ya kisasa na kusimika mfumo wa kamera za usalama.

### 2.16.2. Mapato

Kuna aina kuu mbili za vyanzo vya mapato ambayo ni mapato yatokanayo na shughuli za ndege na yale yasiyotegemea shughuli za ndege yaani *Aeronautical Vs Non aeronautical revenues*.

### 2.16.3. Safari za ndege

Kiwanja kinatoa huduma kwa ndege za ratiba na ndege za dharura (Adhoc). Hivi sasa tuna shirika moja tu la ndege la ATCL linalofanya safari za ratiba. Shirika la ndege la ATCL linafanya safari zake mara 3 kwa wiki Jumatatu, Jumatano na Ijumaa.

### 2.16.4. Takwimu za miruko ya ndege na abiria

Takwimu za miruko ya ndege kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita kuanzia Mwaka 2019 hadi 2023 imeongezeka kutoka 304 iliyorekodiwa mwaka 2019 hadi kufikia miruko 468 kwa mwaka 2023. Idadi ya abiria Pia imeongezeka kutoka abiria 2,025 mwaka 2019 hadi kufikia abiria 56,884 Juni mwaka 2024; Kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 40: Takwimu za miruko ya ndege na abiria**

| Mwaka | Idadi ya miruko ya Ndege | Idadi ya Abiria |
|---|---|---|
| 2019/20 | 304 | 2,025 |
| 2020/21 | 276 | 3,971 |
| 2021/22 | 400 | 13,048 |
| 2022/23 | 468 | 18,580 |
| 2023/24 | 397 | 19,260 |
| ***JUMLA*** | **1,845** | **56,884** |

### 2.16.5. Uendeshaji wa shughuli zaTaasisi:

**i. Shughuli za kiwanja cha ndege Songea zilizotekelezwa**

Uendeshaji wa kiwanja unahusisha wadau mbalimbali kutoka taasisi za umma na sekta binafsi kwa kupitia kamati za kudumu za kiwanja ambazo zimeundwa kisheria.

Kamati za uendeshaji wa kiwanja ni kama zifuatazo:

a. Kamati ya ulinzi (*Aviation Security committee*).

b. Kamati ya uwezeshaji (*Airport Facilitation Committee*)

c. Kamati ya dharura na Uokoaji kiwanjani (*Aerodrome Emergency Committee*).

d. Kamati ya usalama katika Eneo la uendeshaji (Airside Safety Committee).

e. Timu ya kuboresha Huduma bora kwa wateja (Customer Service Joint Improvement Team Committee).

f. Kamati ya kudhibiti Wanyama na ndege (Wildlife Management Committee).

g. Timu ya Menejimenti ya kiwanja (Management Team).

- **Taasisi na idara zilizopo katika kiwanja cha ndege cha Songea**

Katika kuimarisha mnyororo wa huduma tunazotoa kwa wateja, kuna Taasisi, Idara mbalimbali zikiwemo za Serikali, Makampuni ya watu binafsi ambazo kwa pamoja tunashirikiana katika utendaji

wa kazi za kila siku kiwanjani. Miongoni mwa Taasisi na Idara hizo ni kama zifuatazo: -

**Jedwali Na. 41: Taasisi na idara zilizopo katika kiwanja cha ndege cha Songea**

| NA | JINA LA TAASISI/KAMPUNI | AINA/MMILIKI |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) | Wakala wa Serikali |
| 2 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) | Wakala wa Serikali |
| 3 | Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) | Wakala wa Serikali |
| 4 | Jeshi la Polisi (Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi) | Serikali |
| 5 | Kampuni binafsi ya Ulinzi ya "M/S 94 Security Services". | Binafsi |
| 6 | Idara ya Usalama wa Taifa | Serikali |
| 7 | Idara ya Uhamiaji | Serikali |
| 8 | Kampuni ya ndege (ATCL) | Serikali |
| 9 | Kampuni ya kuhudumia ndege (KENCAN) | Binafsi |

Jumla ya Watumishi wote wa Umma, Makampuni na Mashirika Binafsi, Waajiriwa wa muda na wale wa mikataba ni 80.

**ii. Miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.**

**Jedwali Na. 42: Mradi wa kurekebisha upya Jengo lilokuwa la mkandarasi mshauri.**

| Na | Jina la Mradi / Program | Shughuli/Miradi husika kwa ufupi | Fedha Pokelewa | Fedha Tumika | Hatua/Hali ya utekelezaji kwa Ujumla | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Ukarabati wa jengo lilokuwa likitumika na mkandarasi mshauri ili liweze kutumika kama jengo la abiria (Remodeling of engineer's office into the terminal building). | -Kukarabati eneo la ukumbi wa kuondokea abiria (Depature lounge) ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 145 kwa wakati mmoja pamoja na kuboresha ukumbi wa kuwasili abiria (Arrival lounge)<br>-kutengeneza maegesho ya magari ya kisasa<br>-kusimika mfumo wa kamera za usalama | 423,836,376.60 | 63,575,456.49 | Mkandarasi ameshindwa kutekeleza mradi ikiwa ni pamoja na kushindwa kutimiza mashariti ya mkataba | Mkandarasi mpya ameshapatikana |

### 2.16.6. Changamoto za Utekelezaji

Katika mradi wa Ukarabati wa jengo lilokuwa likitumika na mkandarasi mshauri ili liweze kutumika kama jengo la abiria (Remodeling of engineer's office into the terminal building) changamoto kuu iliyojitokeza ni mkandarasi aliyekabidhiwa kazi hiyo kushindwa kufikia masharti ya mkataba aliopatiwa na mwajiri wake Mamlaka ya Viwanja vya ndege kupelekea kusitishiwa mkataba.

### 2.16.7. Mikakati ya Kutatua Changamoto

Uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania umeshafanya taratibu za kumpata mkandarasi mpya atakae endeleza ukarabati wa jengo lilokuwa likitumika na mkandarasi mshauri ili liweze kutumika kama jengo la abiria.

### 2.16.8. Hitimisho

Kukamilika kwa mradi wa upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kiwanja, kutasaidia kupunguza changamoto kama ufinyu wa jengo la abiria na ufinyu wa eneo la maegesho ambao umetokana na ongezeko la idadi ya abiria.

## 2.17 Sekta ya Nishati

### A. Utangulizi

Mkoa wa Ruvuma una wilaya tano (5) ambazo makao makuu ya Wilaya zote tayari yamepatiwa umeme, wilaya hizo ni Songea, Namtumbo, Tunduru, Mbinga na Nyasa. Mkoa wa Ruvuma

unapata umeme wa gridi kupitia vituo vikubwa vya kupoza umeme vilivyopo Madaba na Songea.

- **Usambazaji**

Mkoa wa Ruvuma una mtandao mkubwa wa usambazaji wa umeme wenye mashine umba (Transformers) **878** na urefu wa jumla ya kilomita **2,584.16** kwa msongo wa kilovoti 33, kilomita **157.89** kwa msongo wa kilovoti 11 na kilomita **2,333.40** kwa msongo wa kilovoti 0.4/ 0.23 (LT). Pia Mkoa una jumla ya wateja **113,243** mpaka kufikia tarehe 30/06/2024 kwa mchanganuo ufuatao; wateja wa mtumizi ya kundi la chini ni **113,205** wateja wakubwa wa matumizi makubwa ni **38**

- **Madeni**

Mpaka sasa Mkoa una deni linalofikia Shs **295,028,576.68** linalojumuisha tasisi za serikali na watu binafsi mchanganuo wa deni la Mkoa ni kama inavofafanuliwa kwenye jedwali Na.43

**Jedwali Na. 43: Taasisi za Serikali**

| **Madeni ya Tasisi ya Taasisi za Serikali** | | |
|---|---|---|
| **Na** | **Jina la Tasisi** | **Deni** |
| 1 | TPDF Ruvuma | 31,003,496.68 |
| **Jumla la Deni** | | **31,003,496.68** |
| **Madeni ya Tasisi Binafsi** | | |
| **Na** | **Jina la Mdaiwa** | **Deni** |
| 1 | Mr Ramadhani .N.Kayombo | 114,592,837.21 |
| 2 | M/s Andoya Minhydro Electrical | 149,432,243.70 |
| **Jumla la Deni** | | **264,025,080** |

## B. Hali ya Upatikanaji wa Umeme

Hali ya upatikanaji wa umeme kwa mkoa wa Ruvuma kwa sasa ni nzuri na ya kuridhisha baada ya kuunganishwa na Gridi ya Taifa tarehe **15/09/2018** katika wilaya nne (4) za Songea, Namtumbo, Mbinga na Nyasa kupitia ujenzi wa laini ya msongo wa Kilo volti 220 kutoka Makambako na vituo viwili vikubwa vya kupoza na kusambaza umeme vya Songea na Madaba.

Wakati huohuo wilaya ya Tunduru iliunganishwa na gridi ya Taifa tarehe **22/12/2019** na kuzima mitambo ya mafuta. Pia mkoa unapata umeme kutoka kwa wawekezaji binafsi wa kampuni ya **TULILA** na **ANDOYA** ambao wana uwezo wa kufua Megawati **5.5** na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa.

**Jedwali Na. 44: Vituo vya kupoza umeme**

| Na | Maelezo | Madaba | Songea | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uwezo wa kituo(MVA) | 30 | 60 | 90 |
| 2 | Uwezo wa kituo (MW) | 24 | 48 | 72 |
| 3 | Idadi-ya transfoma( vituo vya gridi) | 1 | 2 | 3 |
| 4 | Matumizi ya juu yaliyofikiwa | 1.7 | 17 | |
| 5 | Laini za usambazaji 33kV | 3 | 4 | |

## C. Miradi Mikubwa (Major Projects)

Mkoa wa Ruvuma ni mojawapo ya Mikoa iliyofaidika na Miradi ya Gridi Imara inayotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 Nchi nzima, ikiwa na lengo la kuboresha upatikanaji umeme wenye ubora na kujenga vituo vya kupooza umeme kwenye kila Wilaya.Katika

Mkoa wa Ruvuma mradi unatekelezwa na Mkandarasi Kalpataru Projects International Limited kutoka India.

Gharama za mradi huu ni Shilingi za Kitanzania **150,782,754,376.88.** Mradi huu una urefu wa kilomita 214.5 na ambao utahusisha ujenzi wa kituo cha kupozea umeme katika Wilaya ya Tunduru chenye ukubwa wa **2x60MVA** cha msongo wa kilovolti 220/33. Muda wa utekelezaji wa mradi ni miezi 18, ulisainiwa tarehe 24 Februri, 2023 na ulianza tarehe 10 Machi, 2023 na unatarajiwa kukamilika 10 Septemba, 2024. Maendeleo ya mradi mpaka sasa umefikia asilimia **50.6%** za utekelezaji.

Faida zitakazo patikana katika mradi huu ukikamilika ni kwamba kutakuwa na umeme wa uhakika katika wilaya ya Tunduru na Namtumbo kwani kutakuwa na line hivyo nyingi hatutategemea njia moja kama ilivyo sasa.

**D. Miradi Inayofadhiliwa na TANESCO**

- **Miradi ya kusongeza miundombinu (New extension projects)**

Mkoa wa Ruvuma umetekeleza miradi ya kusambaza umeme maeneo mbalimbali ambayo bado yalikuwa hayajafikiwa na huduma hiyo. Kwa mwaka huu wa fedha wa **2023/24** jumla ya shilingi **Tshs. 2,022, 999,807** zilitengwa kwa kazi hiyo ili kufikisha umeme maeneo **22** Mkoani na Wilayani.

Kwa mwaka wa fedha wa **2022/23**, mkoa ulifanikiwa kujenga laini za msongo wa kati (33&11kV) zenye jumla ya kilomita **47** laini za msongo wa 0.4kV zenye jumla ya kilomita **45.54** na transfoma **33** zilifungwa

- **Miradi ya kuimarisha umeme (Voltage improvements projects)**

Katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla **Tsh 2,705,086,653** zimetengewa kutekeleza miradi **43** ya kuondoa tatizo la umeme hafifu. Utekelezaji wa miradi hii umefanikiwa kuwanufaisha wananchi zaidi ya 500 na viwanda vidogo (mashine za kusaga na kukoboa) hivyo kuongeza tija zaidi katika uzalishaji na matumizi ya umeme.

- **Miradi ya Matengenezo (Repair and Maintenance)**

Miradi ya ukarabati wa miundombinu chakavu inatekelezwa kwa gharama Tsh. **2,860,182,184** yenye idadi ya miradi **27** kwa mwaka wa fedha 2023/2024**.** Miradi hii inahusisha kazi za kubadilisha nguzo, kukata miti inayokaribia laini kwa umbali wa kilomita 2500 na kufanya matengenezo ya vituo vidogo vya kupoozea umeme (substations) **85**. Kwa mwaka 2022/23 tulipata fungu la kutekeleza miradi 21.

Maboresho haya yamesaidia kuboresha hali ya upatikanji wa umeme katika Mkoa wa Ruvuma na kuchangamsha shughuli za uzalishaji mali.

➢ **Kuunganisha wateja**

Kwa mwaka wa fedha wa **2023/2024** mpaka mwezi Desemba 2023, Mkoa umeweza kuwaunganishia umeme wateja **21,141** sawa na **asilimia 140.35%** ya lengo la Mkoa la kuunganisha wateja wapatao **15,063.** Kwa kiasi kikubwa uboreshaji wa mifumo ya kuunganisha wateja umechangia sana ongezeko la wateja.

➢ **Miradi Inayofadhiliwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA)**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vijiji 551 ambapo kufikia Juni 2024 vijiji **541** sawa na asilimia **98.2%** vimepata huduma ya umeme kupitia miradi ya REA ikiwemo REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa kwanza na wa Pili, REA Awamu ya Pili na REA Awamu ya kwanza. Mkoa wa Ruvuma kuna jumla ya vitongoji **3,693,** kati ya hivyo vitongoji **1,836** vina umeme sawa na asilimia **49.7%** na vitongoji **1,857** havina umeme sawa na asilimia **50.3%.** Wakala wa Nishati vijijini umeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Mkoa wa Ruvuma ikiwa na lengo la kuwapatia huduma za Nishati Wananchi wa Vijijini ili kuboresha huduma za jamii.

➢ **Miradi ya REA Inayotekelezwa Mkoa wa Ruvuma**

Wakala wa Nishati Vijijini unatekeleza jumla ya Miradi Minne (4) katika maeneo tofauti ya mkoa wa Ruvuma kama ilivyoanishwa hapa chini:-

a) REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (**REA III Round II**);

b) Mradi wa Kupeleka umeme kwenye Vituo vya Afya na Pampu za Maji (**COVID 19 Project**).

c) Mradi wa kupeleka umeme kwenye migodi midogo na mashamba (**small-scale Mining Project**)

d) Mradi wa ujazilizi (**Densification 2C)**

**ii. REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II)**

Mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme, kwenye Mkoa wa Ruvuma, kuna Jumla ya Vijiji **264** vinavyoendelea kupatiwa Umeme kupitia mradi wa **REA III Round II,** mradi unatekelezwa kwa gharama **Tsh. 91.3 bilioni** ambapo Wakandarasi (2) wanaendelea na utekelezaji wa mradi **(Lot 25 & 26).**

**iii. Hali ya utekelezaji wa mradi**

Mpaka kufikia mwezi Juni 2024 Wakandarasi wa **Lot 25 & 26** wamewasha Vijiji **251** kati ya vijiji **264.**

**E. Mradi wa kupeleka umeme katika vituo vya afya na pampu za maji ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na UVIKO-19.**

Mradi huu unahusu kusambaza umeme kwenye vituo vya afya na visima vya maji kwenye Mkoa wa Ruvuma ambapo inatarajiwa vituo vya afya, hospitali 3 na visima vya maji 16 vitaungwa na huduma ya umeme. Serikali inatekeleza mradi huu ili kuongeza

jitihada za kupambana na magonjwa ya kuambukiza ukiwemo UVIKO-19. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia shilingi **milioni 848.063**. Mradi unatekelezwa na mkandarasi anaitwa **STATE GRID**

Maeneo yatakayonufaika na mradi ni maeneo **19** ambapo pump za maji **16** na vituo vya afya **3** kutoka wilaya za mkoa wa Ruvuma kama zinavyoonekana kwenye **jedwali Na. 45**

**Jedwali Na. 45: Maeneo ya Visima vya maji na vituo vya afya vitakavyonufaika.**

| S/N | Wilaya | Pump za maji | Vituo vya afya |
|---|---|---|---|
| 1 | Songea | 2 | 2 |
| 2 | Namtumbo | 5 | - |
| 3 | Tunduru | 9 | 1 |
| | **TOTAL** | **16** | **3** |

### i. Utekelezaji wa Mradi Kwenye Mkoa wa Ruvuma

Mpaka kufikia mwezi Juni, 2024 mradi umefikia asilimia **84.1%** ya utekelezaji kama unavyoonekana kwenye **jedwali Na.46**

**Jedwali Na. 46: Hali ya utekelezaji wa mradi wa COVID 19**

| Maelezo | Wigo | Zimekamilika | % |
|---|---|---|---|
| Detailed Survey (MV & LV) | 100% | 100% | 100.00% |
| Vituo/pampu ya maji | 13 | 12 | 92.00% |
| Usimamishaji wa Nguzo Msongo wa kati | 9.926 | 8.622 | 86.86% |
| Uvutaji wa waya - Msongo wa kati | 9.926 | 8.508 | 85.71% |
| Usimamishaji wa Nguzo Msongo wa Mdogo | 1.029 | 0.626 | 60.83% |
| Uvutaji wa waya - Msongo Mdogo | 1.029 | 0.816 | 79.31% |
| Mashine Umba | 13 | 12 | 92.00% |
| **Asilimia ya utekelezaji** | | | **84.1%** |

### ii. Mradi wa kupeleka umeme vijijini, katika migodi midogo, maeneo ya viwanda na maeneo ya kilimo.

Mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 5 ya uchimbaji madini hususani wachimbaji wadogo, viwanda vidogo na mashamba ya kilimo katika Mkoa wa Ruvuma, lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa. Mradi utahusisha ujenzi wa 108.3km za mkondo wa kati wa umeme, 27km mkondo mdogo wa umeme na kufunga mashine umba 16 (transformer). Gharama za mradi huu zinakadiriwa kufikia **shilingi Bilioni 4.66.**

**Jedwali Na. 47.** Linaonesha idadi ya maeneo kila wilaya yatakayonufaika

**Jedwali Na. 47: Idadi ya Maeneo ya Migodi, Mashamba na Viwanda yatakayonufaika**

| NA | WILAYA | IDADI YA MAENEO |
|---|---|---|
| 1 | Songea | 4 |
| 2 | Mbinga | 2 |
| 3 | Nyasa | 3 |
| 4 | Tunduru | 6 |
| 5 | Namtumbo | 1 |
| | **Jumla ya maeneo** | **16** |

### iii) Maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa small scale mining

Hatua ya utekelezaji wa mradi huu unaoendelea ni uchimbaji wa mashimo ya nguzo, kusimika nguzo, kuvuta waya, kufunga transfoma na kuwasha umeme kwenye maeneo mbali mbali yaliyopitiwa na mradi huu zikiwemo Wilaya za Tunduru, Namtumbo, Nyasa, Mbinga na Songea kwenye Mkoa wa

Ruvuma.Mpaka kufikia mwezi Juni 2024 mradi umefikia **asilimia 32.1%**

**Jedwali Na. 48: Hali ya utekelezaji wa mradi Migodi, mashamba na viwanda**

| Maelezo | Wigo | Zimekamilika | % |
|---|---|---|---|
| Detailed Survey (MV & LV) | 100% | 100% | 100.00% |
| Vijiji/maeneo | 19 | 0 | 0% |
| Usimamishaji wa Nguzo Msongo wa kati | 108.3 | 24.7 | 22.8% |
| Uvutaji wa waya - Msongo wa kati | 108.3 | 4.375 | 4.04% |
| Mashine Umba | 32 | 1 | 3.125% |
| Wateja | 87 | 0 | 0% |
| **Asilimia za utekelezaji** | | | **32.31%** |

### iv. Mradi wa Ujazilizi (Densification 2C)

Mradi huu una lengo la kufikisha umeme kwenye Vitongoji vya Mkoa wa Ruvuma. Wigo wa mradi huu unahusisha **Vitongoji 272** wenye ujenzi wa Msongo mdogo 664km, Mashine umba **241** na kuunganisha wateja wa awali 13,744. Gharama za mradi huu ni takribani **shilingi Bilioni 33.56**. Mradi huu kwa mkoa wa Ruvuma utatekelezwa katika Loti 2 ambazo ni Lot 11 (Songea, Mbinga na Nyasa-Vitongoji 137) na Lot 12 (Namtumbo na Tunduru-Vitongoji 135).

Mpaka kufikia mwezi Juni 2024 Wakala umepokea detail survey ya Mkandarasi MF kupitia TANESCO kwa loti zote mbili (11 &12) na ipo kwenye mchakato wa kuzipitia kwa kina na kutoa "Approval" ruhusa kwa Mkandarasi kuendelea na utekelezaji.

**Jedwali Na.49:** linaonyesha idadi ya maeneo kila wilaya yatakayonufaika

**Jedwali Na. 49: Vitongoji vitakavyonufaika na umeme mradi wa ujazilizi**

| Na | Wilaya | Idadi ya Vitongoji |
|---|---|---|
| 1. | Songea DC | 50 |
| 2. | Mbinga | 42 |
| 3. | Nyasa | 19 |
| 4. | Namtumbo | 46 |
| 5. | Tunduru | 89 |
| **JUMLA** | | **246** |

## F. Changamoto

Mkoa wa Ruvuma unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Uchomaji wa moto wakati wa uandaaji wa mashamba ambao unaathiri miundombinu ya shirika.

ii. Matukio ya wizi wa waya za shaba kwenye transfoma na vyuma vya kushikilia nguzo isianguke (base plate)

iii. Upungufu wa wafanyakazi katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa ujumla uliosababishwa na baadhi yao kuhamishwa au kustaafu

iv. Urefu wa line za kusambaza umeme 33KV na 11KV kuwa ndefu zaidi. Mfano line ya Mbinga na Namtumbo

v. Kutopatikana kwa vifaa kwa wakati mfano waya,nguzo ,n.k kusababisha miradi mingi kuchelewa na wateja kutokujengewa kwa wakati.

**G. Jinsi ya Kukabiliana na Changamoto**

i. Shirika limeendelea na zoezi la kupalilia visahani kwa kutumia wanavijiji na kuendelea kutoa elimu pamoja na mwaka huu kuanza kutumia nguzo za zege kwa Mkoa wa Ruvuma;

ii. Kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na viongozi wa serikali ili kuwabaini wanaofanya uharibifu huo na kuchukuahatua za kisheria;

iii. Katika kukabiliana na upungufu wa wafanyakazi mahitaji ya watumishi yamewasilishwa makao makuu kitengo cha rasilimali watu. Aidha, tumeendelea kutumia wafungwa na wanakijiji kwa kazi ambazo sio za kiufundi;

iv. Tumeomba ngazi za juu kujengewa kituo cha kupozea umeme Mbinga ili kupunguza urefu wa line na kuongeza njia nyingi badala ya kuwa na njia moja tu inayopeleka umeme Mbinga na Nyasa;

v. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 shirika limejipanga kurudisha manunuzi ngazi za mkoa badala ya nchi nzima kununuliwa sehemu moja (Makao makuu).

## 2.18 Sekta ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii

### A. Huduma za Afya

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vituo **419** vinavyotoa huduma za afya, kati ya hivyo Hospitali ni **15** zikiwemo tisa (**9)** zinazomilikiwa na Serikali (GoV) na nane (**8)** zinamilikiwa na Mashirika ya Dini (FBO).Vituo vya Afya vipo **50**, kati ya hivyo vituo **39** vinamilikiwa Serikalina **11** ni vya Mashirika ya Dini na Binafsi (FBO &Private). Zahanati zipo **352,** kati ya hizo zahanati **293** zinamilikiwa na Serikali**,** na **59** zinamilikiwa na Mashirika ya Dini na Binafsi.

- **Rasilimali Watu Afya Katika Mkoa**

Upatikanaji wa watumishi wa afya katika Mkoa wa Ruvuma kwa sasa ni **2,681 sawa na asilimia 41** katika watumishi wote **6,569** wanaohitajika kwa kujumuisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ruvuma na Halmashauri zote. Uongezekaji wa vituo vipya vya huduma umepelekea kufanya msawazo wa watumishi waliopo, hivyo kushusha asilimia ya upatikaji wa watumishi.

- **Matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali (GoTHOMIS)**

Kufikia mwezi Juni 2024, jumla ya vituo **94** sawa na asilimia **27.6** ya vituo vyote **340** vya kutoa huduma za afya vimesimikwa na vinatumia mfumo wa GoTHOMIS.Mkoa umeweka lengo la kuhakikisha vituo vyote vinasimika mfumo huo ifikapo mwishoni mwa mwezi Desemba, 2024.

- **Hali ya Uwepo wa Bidhaa za Afya na Uchunguzi**

Katika hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya jumla ya **Tsh. 7,950,003.39** zilipokelewa ambapo kati ya hizo **Tsh 3,275,003,560.39** zilipelekwa kama ruzuku ya Serikali kupitia Bohari ya dawa (MSD) na **Tsh 4,700,000** zilipelekwa kwenye Halmashauri kama Ruzuku kwenda ngazi ya vituo vipya vya kutolea huduma kwa ajili ya kununua vifaa na vifaa tiba. Kati ya kiasi cha bidhaa **29,819** zilizoagizwa bidhaa **26,888** (90.1%) zilipatikana.

- **Utekelezaji wa Huduma za Chanjo**

Mafanikio kwa kipindi cha Januari hadi Disemba, 2023 yalionesha kuwa kiwango cha chanjo kilichofikiwa: Chanjo ya kifua kikuu (BCG) asilimia **166,** chanjo ya kuzuia kupooza (Polio) asilimia **135,** chanjo ya Donda koo, Kukakamaa na Kifaduro (DTP3) **135%,** chanjo ya kuzuia homa ya mapafu (Pneumonia) asilimia **135,** chanjo ya kuzuia kuharisha (Rota virus) **127%,** chanjo ya surua (Measles Rubella) **asilimia 152,** chanjo ya Pepopunda (Td) kwa wajawazito asilimia **106%** na chanjo ya kuzuia Saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa wasichana umri wa miaka 14 ni asilimia **126.**

- **Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto**

Mkoa una jumla ya vituo **348** vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na mtoto na asilimia **91.0** ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika

Mkoa Kati ya vituo hivyo, vituo **325** sawa na asilimia **93.3** vinatoa huduma ya chanjo, vituo **313** sawa na asilimia **90.0** vinatoa huduma ya uzazi na kujifungua, vituo 308 sawa na asilimia **89.0** vinatoa huduma ya uzuiaji wa maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Aidha kati ya vituo vya afya 38, vituo **20** sawa na asilimia **51.2** ya vituo vya afya vinatoa huduma kabambe za dharura za mama wajawazito na Watoto wachanga (**CEmONC**).

Kiwango cha akina mama wanaohudhuria kliniki kabla ya wiki 12 za ujauzito kimeongezeka kutoka asilimia **53.0** Desemba 2022 hadi asilimia **54.2** Desemba **2023**. Kiwango cha akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma kimeongezeka kutoka asilimia 83.2 mwaka 2022 hadi asilimia 87.3 mwaka **2023**.

- **Huduma za Kupima na Kutibu Saratani ya Shingo ya Mlango wa Kizazi**

Mkoa una jumla ya vituo 59 vinavyotoa huduma ya upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi sawa na asilimia 16.1 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto. Kati ya vituo Hivyo Vituo 30 sawa na asilimia 50.1 vina mashine za matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi (Cryo/Thermo)

Mwaka 2023, jumla ya wanawake 18,116 walichunguzwa, kati yao wanawake 276 sawa na asilimia 2.0 waligundulika kuwa na VIA positive. Kati yao akinamama 261 sawa na asilimia 94.0

walipatiwa tiba ya Cryotherapy/thermo. Wanawake 79 sawa na asilimia **0.4** walihisiwa kuwa na saratani ya shingo ya kizazi, wanawake 8 sawa na asilimia **0.04** walikuwa na mabadiliko makubwa ya awali, wote walipata rufaa.

- **Huduma za Kinywa na Meno Katika Mkoa**

Upatikananji wa huduma za Kinywa na Meno umeboreshwa kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na kipindi cha miaka mitatu iliyopita, hadi kufikia mwezi Disemba 2023 huduma za Kinywa na Meno zinatolewa katika angalau kituo kimoja cha Serikali (Hospitali au Kituo cha Afya) katika Halmshauri zote nane. Hali hii imetokana na Mkoa kupokea fedha za ununuzi wa vifaa na vifaa tiba vya Kinywa na Meno, Mkoa kupokea Watumishi Wataalam wa Kinywa na Meno, Halmashauri kununua vifaa vya kinywa na Meno kupitia mapato ya ndani na fedha za ruzuku.

- **Huduma za Lishe**

Mkoa unaratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za lishe kwa kuzingatia viashiria vilivyoelekezwa kwenye mpango mkakati jumuishi wa lishe wa Taifa na Mkoa. Kwa mujibu wa tafiti ya lishe na Malaria ya mwaka 2022 hali ya lishe ya Mkoa wa Ruvuma ni duni; udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 ni **35.6%,** ukondefu kwa watoto chini ya miaka 5 ni 2.8.%, watoto wanaozaliwa na uzito pungufu ni 12.2%, na upungufu wa damu

kwa watoto chini ya miaka mitano ni 45% na upungufu wa Damu kwa wajawazito ni asilimia 30 viashiria hivi vipo katika kiwango cha juu kuliko cha kitaifa.

Aidha Mkoa Katika kutekeleza mkakati huo, unatekeleza yafuatayo;

- Kutoa elimu kuhusu lishe (MIYCAN) kwa jamii kupitia vyombo vya habari kama vile radio, siku ya Afya na lishe ya kijiji. Sambamba na hilo elimu inatolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya hasa siku za kliniki. (95.7%).
- Kuanzisha mashamba darasa ya kilimo cha mahindi Lishe na ufugaji mbalimbali kwa ajili ya kuongeza lishe ambapo hadi May, 2024 Mkoa ulikuwa na mashamba darasa ya kilimo katika Halmashauri za Madaba, Songea DC, Namtumbo na Manispa ya Songea.
- Kuongeza na kudhibiti upungufu wa virutubishi kwa kutoa vitamin A kwa watoto ambapo hadi Juni Disemba, 2024 Mkoa ulifanikiwa kutoa vitamin A kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka 5
- Kufanya maadhimisho ya siku ya afya ya kijiji ambayo hutumika katika kutoa mafunzo ya lishe kwa vitendo
- Mkoa unatoa huduma ya matibabu jumuishi ya utapiamlo mkali ambapo jumla ya watoto 253 walipata matibabu ya utapiamlo mkali (IMAM) kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

- Katika utekelezaji wa afua za lishe kwa kipindi cha Julai, 2023 mpaka Juni, 2024, Mkoa umetenga kiasi cha TSh 559,230,268.04 na kutumia 512,818,114.16 sawa na asilimia 91.7 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.50

**Jedwali Na. 50: Mchanganuo wa utekelezaji afua za Lishe kwa kila Halmashauri**

| SN | HALMASHAURI | KIASI CHA FEDHA KILICHOTENGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SONGEA MC | 99,105,086.31 | 97,760,342.96 | 98.6 |
| 2 | NYASA DC | 53,372,850.29 | 51,751,614.57 | 97.0 |
| 3 | MBINGA TC | 35,468,000.00 | 33,752,545.00 | 95.2 |
| 4 | MADABA | 33,824,592.13 | 32,097,655.38 | 94.9 |
| 5 | SONGEA DC | 35,970,629.97 | 33,509,464.00 | 93.2 |
| 6 | MBINGA DC | 102,173,649.62 | 95,205,649.62 | 93.2 |
| 7 | TUNDURU | 115,330,922.72 | 104,591,368.72 | 90.7 |
| 8 | NAMTUMBO | 83,984,537.00 | 64,149,473.91 | 76.4 |
| | MKOA | 559,230,268.04 | 512,818,114.16 | 91.7 |

Mkoa wa Ruvuma kwa sasa una jumla ya wataalam 16 wanaotoa huduma za Lishe katika Halmashauri na Hospitali za Halmashauri.

- **Utekelezaji wa Huduma za Afya Chini ya Miradi Misonge**

**Huduma za Udhibiti UKIMWI Katika Mkoa**

Vituo 334 sawa na asilimia 88 vinatoa huduma za unasihi na upimaji wa VVU (HTS); vituo 304 sawa na asilimia 80 vinatoa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT); vituo 150 sawa na asilimia 39.6 vinatoa huduma za matunzo na tiba za UKIMWI (CTC); Vituo 332 sawa na

asilimia 87.8 vinatoa huduma za uchunguzi na tiba ya magonjwa ya ngono (STI); vituo 115 sawa asilimia 30.4 vinatoa huduma za UKIMWI ngazi ya jamii (CBHS); vituo 45 sawa na asilimia 11.9 vinatoa huduma ya tohara ya kitabibu kwa wanaume (VMMC) na vituo 41 sawa na asilimia 10.8 vinatoa huduma za dawa kinga ya kuzuia maambukizi ya VVU (PrEP).

Kiwango cha maambukizi ya VVU katika Mkoa kimepungua kwa asilimia 0.7 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2016/17 hadi asilimia 4.9 mwaka 2022/23. Mwaka 2023, watu 60,271 sawa na asilimia 3.2 ya wakazi wote wa Mkoa walikuwa wanaishi na maambukizi ya VVU, ikiwa watu wazima zaidi ya miaka 15 ni 57,639 sawa na asilimia 95.6 na watoto ni 2,632 sawa na asilimia 4.4 (*Spectrum 2023*). Katika kutekeleza Malengo ya Kimkakati ya 95-95-95, kufikia mwezi Desemba 2023, WAVIU 65,916 sawa na asilimia 109.4 walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi; WAVIU 64,924 sawa na asilimia 98.5 walikuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs), na WAVIU 60,899 sawa na asilimia 93.8 walikuwa wamefubaza makali ya VVU (*DHIS2*).

- **Huduma za Udhibiti Malaria**

Ugonjwa wa Malaria bado ni tatizo la kiafya kwa wananchi wengi wa Mkoa wa Ruvuma, ugonjwa huu unachangia kwa kiwango kikubwa hali ya kuugua na vifo.Kulingana na matokeo ya Tafiti zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya takwimu (Malaria Indicator

Surveys) zinaonesha kuwa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa Malaria katika Mkoa kimepungua kutoka asilimia **11.8** mwaka 2018 hadi kufikia asilimia **7.9** mwaka 2022. Aidha, kiwango hiki kipo chini ya kiwango cha maambukizi kitaifa cha asilimia **8.1**kwa mwaka 2022**.** Aidha, japokuwa kiwango hiki kimepungua, hali ya maambukizi ya Malaria katika Halmashauri zetu inatofautiana. Halmashauri zenye kiwango kikubwa maambukizi mara mbili zaidi ya wastani wa Kitaifa ni Halmashauri za Wilaya ya Namtumbo asilimia **16** na Tunduru asilimia **15**. Adiha, Halmashauri zenye kiwango cha maambukizi chini ya wastani wa Kitaifa ni Halmashauri ya Mji Mbinga asilimia **5** na Halmashauri ya Manispaa ya Songea asilimia **5.2.**

i. Katika kutekeleza mkakati wa kudumu wa kupambana na ugonjwa wa Malaria, chini ya kauli mbiu isemayo “Ziro Malaria Inaanza na Mimi” Mkoa unaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:- Uhamasishaji wa matumizi sahihi na ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu kwa kupitia kampeni za ugawaji wa vyandarua shuleni (School Net Programme) na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa kwenye clinic za afya ya uzazi na mtoto (Chandarua Clinic). Kwa mwaka wa 2023 Mkoa umegawa Jumla ya Net 338,618, Chandarua Kilinik 142,636 na School net 195,982.

ii. Mkoa umefanikiwa kufanya upuliziaji wa viuadudu kwenye mazalia ya mbu na usimamizi wa usafi wa mazingira kwa

kuondoa mazalia ya mbu kwenye makazi ambapo kwa mwaka 2023 jumla ya viuatilifu lita 1,760 vilinunuliwa na kupuliziwa kwenye mazalia ya mbu kwenye Halmashauri.

- **Huduma za Kifua Kikuu na Ukoma**

Huduma na Kifua Kikuu na Ukoma zinatolewa katika zahanati, vituo vya afya pamoja na Hospitali. Vituo 73 vinafanya uchunguzi wa Kifua Kikuu kwa njia ya hadubini sawa na asilimia 19.3, Vituo 9 sawa na 2.3 vinatoa huduma ya uchunguzi wa Kifua Kikuu kwa njia ya vinasaba, na Vituo 15 sawa na asilimia 3.8 vinafanya uchunguzi kwa njia ya mionzi (X-ray). Aidha, Vituo 304 vinatoa huduma ya matibabu ya Kifua Kikuu na Ukoma sawa na asilimia 80.4.

Mwaka 2023 wagonjwa 2,394 walifanyiwa uchunguzi wa Kifua Kikuu, kati yao 985 sawa na silimia 41 walikuwa na vimelea: watoto walikuwa 397 sawa na asilimia 16; wenye VVU walikuwa 293 sawa na asilimia 12.3. Wagonjwa wenye Kifua Kikuu sugu walikuwa 6.

**B. Huduma za Ustawi wa Jamii**

- **Usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano (U5BR)**

Mkoa wa Ruvuma unasimamia utekelezaji wa mpango wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya

miaka mitano bure katika halmashauri zote za mkoa. Lengo la Mkoa wa Ruvuma ni kusajili na kuwapatia vyeti watoto 242,140, ambapo hadi sasa Mkoa umeandikisha na kusajili vyeti vya watoto **274,992 sawa na asilimia 114.03** kwenye mfumo wa eRITA, ambapo watoto **18,680 (Me 8,662** na **Ke 10,018)** ni kutoka katika familia zenye mazingira magumu.

- **Utambuzi na Huduma kwa Watoto Waishio Kwenye Mazingira Hatarishi (WWKMH)**

Mkoa unasimamia utambuzi na huduma kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na 21 ya mwaka 2009. Hadi sasa mkoa umetambua watoto **80,101 (Me 37,660 na Ke 42,441)** na kuwapatia huduma mbalimbali zikiwemo msaada wa kisaikolojia, afya, elimu, malezi kwenye makao ya watoto yatima na kuimarisha uchumi wa familia**.**

- **Utambuzi na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

Mkoa umewatambua watu wazima 7,893 (Me 3,959 na Ke 3934) wenye ulemavu wa aina mbalimbali na watoto 3,941 wenye umri chini ya miaka mitano. Kati ya watoto waliotambuliwa, wenye ulemavu wa viungo ni 1,720, wasioona 527, ukiziwi 626, changamoto ya ufahamu 922 na wenye ualbino 112. Watoto wenye uwezo wa kujumuishwa kwenye afua za ujifunzaji wameandikishwa shule.

- **Utambuzi na Huduma kwa Wazee**

Katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wazee, hadi kufikia 30 Juni, 2024, Mkoa umetambua Wazee 67, 404 (Me 32,199 na Ke 35,205), ambapo wazee 54,279 (Me 25,516, Ke 28,763) wamepatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata msamaha wa matibabu. Pia, Mkoa umeunda Mabaraza ya Ushauri ya Wazee katika ngazi zote za vijiji, kata, Halmashauri na Mkoa.

- **Utambuzi, Usajili na Utoaji wa Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, Mkoa unafanya utambuzi na uhamasishaji wa usajili wa watoa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa mujibu wa Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Na.23 ya mwaka 2002. Hadi 30 Juni 2024 Waganga **1,476** wametambuliwa, ambapo **814** wamepatiwa usajili na Baraza la Tiba Asili na Tiba na Tiba Mbadala. Aidha, kliniki **16** zimesajiliwa, maduka **27** ya Dawa za Tiba Asili na Tiba Mbadala yamesajiliwa.

- **Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF)**

Mkoa unatekeleza Waraka Na.1 wa Mwaka 2018 wa Maboresho ya Mfuko wa Afya ya Jamii ambao umeleta tija kubwa kwa wananchi katika kupata huduma za afya za uhakika. Hadi kufikia

30 Juni, 2024 jumla ya kaya **31,211** zenye wanufaika **144,160** sawa na asilimia **8.6** zimeandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF) kwa malipo ya **Tshs.30,000** kwa kila kaya, sawa na makusanyo ya **936,330,000.00**.

**C. Hali ya Usafi wa Mazingira na Magonjwa ya Mlipuko**

- **Hali ya usafi na mazingira katika Mkoa**

Hali ya uwepo wa vyoo katika katika kaya kwa Mkoa wa Ruvuma ni asilimia 99.8. Kaya zenye vyoo bora ni asilimia 74.6 na kaya *sisizo na* vyoo ni asilimia 1.8.

Mkoa bado unaendelea na jitihada mbalimbali ili kuimarisha hali ya vyoo bora na usafi wa mazingira katika kaya na taasisi. Jitihada hizo ni pamoja na:- Ukaguzi wa vyoo katika kaya kwa kutumia wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii pamoja na wataalamu ngazi ya Mkoa na Halmashauri, Usimamizi wa sheria zinazo husu Afya na Usafi wa Mazingira na ujenzi wa vyoo katika vituo vya kutolea huduma za Afya kupitia mradi wa Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

- **Hali ya Magonjwa ya mlipuko katika Mkoa**

Aidha, Mkoa unaendelea kufuatilia, na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko pale yanapotokea, kwa mwaka 2023, mkoa ulipata mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza Mkoa

ulipata mlipuko kuanzia tarehe 21 Januari 2023 hadi12 Februari 2023 ambapo kulikuwa na jumla ya wagonjwa 12 na vifo vitatu. Kwa awamu ya pili mlipuko ulitokea mwezi Desemba 2023 ambapo kulikuwa na jumla ya wahisiwa 3 ambapo kati yao ni mgonjwa 1 tu ndiye alithibitika kuwa na ugonjwa wa Kipindupindu, wagonjwa wote walipatiwa huduma na kuruhusiwa.

**D. Huduma za maabara na uchunguzi wa magonjwa ya binadamu na huduma za mionzi.**

- **Vifaa tiba vya maabara na huduma za mionzi.**

Katika kuhakikisha wananchi wanapata matibabu sahihi, Mkoa umepokea mashine mbali mbali za uchunguzi wa magonjwa ya binadamu na kuzipeleka kwenye vituo vinavyotoa huduma za Afya ya Msingi. Hadi Juni 30, 2024 Mkoa umepokea mashine 27 za Heamatolojia kwa ajili ya FBP, mashine 26 za kupima kemia ya Mwili (Biochemistry) na Mashine 25 za kupima maambukizi ya njia ya mkojo.

Katika harakati za kutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma, Mkoa una jumla ya mashine 9 za Genexpert, hadubin 64 na mashine 2 za Truenat zenye uwezo wa kupima maabukizi ya vimelea vya TB.

Kwenye Mapambano ya kutokomeza maambukizi ya virusi vya ukimwi Mkoa una Mashine moja ya kupima wingi wa virusi vya

UKIMWI kutoka kwa watu wenye maambukizi ya VVU. Aidha Mkoa una Jumla ya mashine 8 za X – Ray za kidijitali (Digital X – ray mashine) ambazo zimeshapelekwa katika Halmashauri zote na CT- Scan mashine moja ambayo ipo katika hospitali ya rufaa ya Mkoa Songea (HOMSO). Vifaa hivi vyote vimegharimu **Shilingi 6,178,901,063.87**

**E. Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Basket**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mkoa wa Ruvuma umepokea fedha kutoka Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Busket Fund*) kiasi cha **Shilingi 3,507,362,484.00** kwa robo zote nne, na hadi Juni 2024 **Shilingi 3,177,625,646.22** zilitumika sawa na asilimia **90.5** ya fedha pokelewa na kubakiwa na salio la **Shilingi 329,736,837.78**

**F. Ujenzi wa Miundombinu ya Afya Katika Mkoa**

Kwa kipindi cha mwaka 2023/24 Mkoa umepokea jumla ya fedha **Shilingi. 9,093,750,000** kwa ajili kuimarisha na kuboresha miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya, ikiwa fedha kutoka Serikali Kuu Shilingi. **8,800,000,000.00** DHIBITI MALARIA (PSI) **Shilingi 293,750,000.00.** Miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba shilingi **800,000,000.00**

- Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga shilingi **800,000,000.00**
- Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Songea Shilingi **800,000,000.00**
- Umaliziaji wa Zahanati ya Ifinga Halmashuari ya Wilaya ya Madaba shilingi **50,000,000.00**
- Ukarabati wa hospitali ya Mbinga Mji kwa gharama ya **Tshs. 900,000,000.00**
- Ununuzi wa vifaa tiba vya Zahanati kwenye Halmashauri zote nane **Tshs. 800,000,000.00**
- Ununuzi wa vifaa tiba katika Vituo vya Afya kwenye Halmashauri zote nane **Tshs. 3,900,000,000.00**
- Ujenzi wa Zahanati moja katika kijiji cha Chawisi Tunduru kwa gharama ya **Tshs. 293,750,000.00**
- Ukamilishaji wa zahanati 16 kwa gharama ya **Tshs. 800,000,000.00**
- Mkoa pia umepokeea Magari **12** kati ya hayo magari ya kubebea wagonjwa "Ambulance" tano (**5)** na magari ya usimamizi shirikishi sita **(6)** na gari la Utawala Hospitali ya Mkoa Songea moja (**1)**

Kwa mwaka wa fedha 2024/25 Mkoa umepokea Shilingi **2,125,000,000.00** ikiwa ni fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ya afya na ununuzi wa vifaa tiba katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Mbinga na Madaba.

## 2.19 Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

### A. Utangulizi

Sekta ya elimu mkoani inafanya kazi kwa ushirikiano na Halmashauri, Idara ya Uthibiti Ubora wa shule, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, vyuo vya Ualimu, Mamlaka ya vyuo vya ufundi (Veta), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Maktaba ya Mkoa.

Aidha Mkoa kupitia Halmashauri unasimamia na kuratibu utoaji wa Elimu Msingi na Sekondari ambayo inaanzia Elimu ya Awali, shule za Msingi na shule za sekondari (O- level na A-level) Elimu ya Ufundi Stadi na Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

### B. Idadi ya Taasisi zinazotoa Elimu katika Mkoa

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi **860**, kati ya hizo shule za Serikali ni **815** na zisizo za Serikali ni **45**, Shule za sekondari ni **247** zikiwemo **187** za Serikali na **60** ni shule za binafsi. Mkoa umekuwa na ongezeko la idadi ya shule za msingi

**16** kutoka idadi ya shule **841** zilizokuwepo mwaka 2023 hadi shule **860** mwaka 2024 sawa na asilimia **1.8**. Shule za sekondari zimeongezeka **14** kutoka idadi ya shule **233** mwaka 2023 hadi kufikia shule **247** mwaka 2024 sawa na ongezeko la shule 14**.** Aidha Mkoa una vyuo vya Maendeleo ya wananchi **9,** vyuo vya ufundi stadi (VETA) **5,** vyuo vya ualimu **3** na Chuo Kikuu **1.** Aidha, Mkoa unaendelea na ujenzi wa chuo cha ufundi kwa watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea

**C. Hali ya uandikishaji elimu ya Awali na darasa la kwanza**

- **Uandikishaji wa wanafunzi Elimu ya Awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2024.**

Uandikishaji umeongezeka na kuimarika ambapo kuna ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya Awali kutoka wanafunzi **42,140** mwaka 2023 hadi kufikia idadi ya wanafunzi **49,396** mwaka 2024 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia **14.** Aidha, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka kutoka wanafunzi **44,857** mwaka 2023 hadi kufikia idadi ya wanafunzi **52,632** mwaka 2024 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia **16.** Mafanikio haya yametokana na mpango wa utoaji wa elimu bila malipo ulioanza kutekelezwa tangu Serikali ya awamu ya tano na sasa unaendelea kutekelezwa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

- **Idadi ya wanafunzi darasa la Awali-VII mwaka 2024**

Kwa mujibu wa takwimu za *Annual School Census* (ASC), Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Machi, 2024 una idadi ya wanafunzi wa darasa la Awali hadi la VII **387,526** Kati yao wavulana **194,666** na wasichana **192,860.**

- **Hali ya Uripoti wa wanafunzi kidato cha Kwanza mwaka 2024**

Kwa mwaka 2024 wanafunzi waliopangwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule za sekondari za Serikali kutoka ndani na nje ya Mkoa ni **31,990**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 walioripoti ni wanafunzi **28,113** sawa na asilimia **88**.

- **Idadi ya Wanafunzi wa Sekondari**

Hadi kufikia Machi, 2024 Mkoa una wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita **87,353** kati ya hao wavulana ni **41,532** na wasichana ni **45,825** Idadi ya wanafunzi wa Sekondari imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutokana na utekelezaji wa sera ya Elimu bure (bila Malipo), kuboresha usimamizi wa ufundishaji katika shule za msingi unaopelekea kupandisha ufaulu.

- **Ikama ya walimu wa shule za msingi na sekondari hadi Machi, 2024**

Hadi kufikia Machi, 2024 mahitaji ya walimu wa shule za msingi ni **10,029** waliopo ni **6,214** hivyo upungufu ni walimu **3,815** sawa na asilimia **38.** Kwa upande wa walimu wa sekondari mahitaji ni **4,395** waliopo ni **3,269**, hivyo upungufu ni walimu **1,126** sawa na asilimia **25**

## D. Hali ya Ufaulu wa Mitihani ya Kitaifa

- **Matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) mwaka 2023**

Jumla ya watahiniwa **46,324** walifanya mtihani wa Taifa wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2023 ambapo **21,532** ni wavulana na **24,792** ni wasichana. Watahiniwa **31,992** wakiwa wavulana **14,272** na wasichana **17,720** wamefaulu Mtihani ambayo ni sawa na asilimia **69.06.** Ufaulu wa mkoa kwa mwaka 2023 umepanda kwa asilimia **0.94** kutoka asilimia **68.12** mwaka 2022**.**

- **Matokeo ya Upimaji Kitaifa Darasa la nne (SFNA) mwaka 2023**

Jumla ya watahiniwa **49,991** walifanya Upimaji wa Kitaifa wa darasa la nne ambapo **24,533** ni wavulana na **25458** ni wasichana. Watahiniwa **37,999** wakiwa wavulana **17,603** na wasichana **20,396** wamefaulu Mtihani sawa na asilimia **76.01.** Mkoa kwa mwaka 2023 umepanda kwa asilimia **0.01** kutoka asilimia **76** mwaka 2022**.**

- **Matokeo ya upimaji wa kidato cha pili- FTNA 2023**

Kimkoa kati ya wanafunzi wenye matokeo **18,786** wanafunzi **15,433** sawa na asilimia **82.2** wamefaulu na wanafunzi **3,353** wamefeli hivyo watarudia kidato cha pili kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Mitihani. Kwa matokeo haya, ufaulu wa mkoa kwa

mwaka 2023 umeshuka kwa asilimia **0.5** kutoka asilimia **82.7** mwaka 2022**.**

- **Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (CSEE) 2023**

Kimkoa kati ya wanafunzi **14,343** waliofanya mtihani, wanafunzi **12,918** sawa na asilimia **91.2** wamefaulu na wanafunzi **1,425** wamefeli kwa kupata daraja sifuri. Ufaulu wa mkoa mwaka 2023 umeshuka kwa asilimia **1.5** kutoka asilimia **92.7** mwaka 2022 hii ni kutokana kushuka kwa viwango vya ufaulu katika Halmashauri za Madaba na Mbinga TC. Ufaulu wa wanafunzi wanaopata daraja la I – III ni asilimia **32.7**. Ufaulu huu bado upo chini ukilinganisha na vigezo vya KPI vilivyowekwa ambapo inatakiwa ufaulu uwe ni asilimia **50**. Idadi kubwa ya wanafunzi wanaofaulu wanapata daraja la IV ukilinganisha na darala la I – III.

- **Ufaulu wa kidato cha Sita mwaka (ACSEE) 2023**

Mkoa umeendelea kufanya jitihada za kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika matokeo ya kidato cha Sita. Tangu Mwaka 2021 mkoa umepandisha ufaulu hadi kufikia wastani wa ufaulu wa 100. Idadi ya wanafunzi waliopata daraja la IV imepungua kutoka **6** mwaka 2022 hadi 4 mwaka 2023.

**E. Samani na Miundombinu**

- **Hali ya madawati katika shule za Msingi**

Hadi kufikia Machi, 2024 mkoa una mahitaji ya madawati **126,459** yaliyopo ni **102,060** na upungufu ni **24,399** Aidha, mkoa kwa

kushirikiana na wilaya zake umeendelea na jitihada mbalimbali ili kuweza kuondoa upungufu uliopo.

- **Hali ya majengo katika shule za Msingi**

Hadi kufikia Machi, 2024 mkoa una mahitaji ya vyumba vya madarasa **9,935**; vilivyopo ni **6,294** na upungufu ni **3,641**. mahitaji ya nyumba za walimu **9,038**; zilizopo ni **2730** na upungufu ni **6248** Kwa upande wa matundu ya vyoo mkoa una mahitaji ya matundu **17,039** yaliyopo ni **9,666** na upungufu ni **7,373**.

- **Samani katika shule za sekondari**

Hadi kufikia Machi, 2024 hali ya meza na viti mahitaji ni **89,112** zilivyopo ni **80,513**, upungufu ni **8,599.**

- **Hali ya Miundombinu ya shule za sekondari**

Miundombinu ya shule za sekondari imekuwa ikijengwa ili kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia. Hadi kufikia Machi, 2024. Mkoa una mahitaji ya vyumba vya madarasa **2,270**; vilivyopo ni **2,341** na upungufu hakuna. Mahitaji ya nyumba za walimu ni **3,374**; zilizopo ni **714** na pungufu ni **2,690.** Kwa upande wa matundu ya vyoo mahitaji ni **3,809** yaliyopo **2,474** na upungufu ni matundu **1,352.** Mahitaji ya mabweni ni **576** yaliyopo **306** upungufu **270,** mahitaji ya vyumba vya maabara ni **645,** vilivyopo **484** upungufu **171.**

**F. Utekelezaji wa Programu ya Elimu Bila Malipo**

Sera ya utoaji wa Elimu Bila Malipo inaendelea kutekelezwa ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Juni, 2024 Mkoa umepokea kiasi cha Shilingi **14,550,415,776.00** ambazo zimesaidia katika uendeshaji wa shule na kuboresha na kuimarisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi na sekondari. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri unaendelea kufuatilia na kutekeleza kwa ufanisi utoaji wa elimu bila malipo ili fedha ya Serikali inayowekezwa iweze kutoa matokeo chanya katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ikiwemo kuimarisha taaluma na elimu kwa ujumla na hivyo kujenga jamii yenye uelewa na kujiletea maendeleo.

**G. Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo na miradi inayotekelezwa**

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu ni matokeo ya kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi kufuatia utekelezaj wa Sera ya elimu bila malipo. Miradi inayotekelezwa ni kama inavyooneshwa hapa chini:

- **Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 Mkoa wa Ruvuma ulipokea fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali kama inavyoonesha hapa chini: -

- Tshs. **8,039,624,574.00** Kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari za kata **10** ambapo shule **9** zimekamilika. Aidha, shule hizi zimesajiliwa na zilipokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2024. Shule **1** (Dr. Damas Ndumbaro) iliyopo Kata ya Tanga baadhi ya majengo yapo katika hatua ya upauaji. Hii ilitokana na changamoto ya mfumo wa NEST na changamoto ya mvua za masika iliyopelekea eneo la ujenzi kutofikika kwa urahisi.
- Tshs**.512,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni **4** ikiwa ni upanuzi wa shule nne za kidato cha tano na sita ambapo ujenzi katika shule zote umekamilika.
- **Tshs. 49,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **49** ya vyoo ambapo maboma yote yamekamilika.
- **Tshs. 550,000,000.00** kwa ajili ya Ukarabati wa maboma **44** ya madarasa ambapo ujenzi umekamilika na madarasa yanatumika.
- **Tshs. 210,000,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa maboma **7** ya maabara ambapo ujenzi umekamilika.

- **Upanuzi wa Shule za Sekondari Kidato cha 5 na 6 kupitia Mradi wa BARRICK**

Mkoa ulipokea jumla ya Tshs. **1,165,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba **13** vya madarasa, mabweni **5** na vyoo matundu **20** katika shule **3** za Sekondari za Maposeni, Namabengo na Nandembo. Mradi huu umekamilika na madarasa, mabweni na matundu ya vyoo yanatumika.

- **Ujenzi wa Miundombinu ya vyumba vya madarasa, mabweni na matundu ya vyoo kupitia Serikali Kuu**

Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs **4,447,300,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya upanuzi wa shule nane (8). Ujenzi unahusisha vyumba **55** vya madarasa, mabweni **24** na matundu ya vyoo **89**. Ujenzi wa madarasa umekamilika. Aidha, ujenzi wa mabweni upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Mkoa pia umepokea jumla ya **Tshs. 2,931,895,119** kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya elimu kwa ajili ya kidato cha kwanza kwa mchanganuo ufuatao; ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya vyumba **100** vya madarasa kwa gharama ya **Tshs 2,539,895,119,** ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya matundu **274** ya vyoo kwa gharama ya **Tshs. 459,600,000** na ukamilishaji wa bwalo katika Sekondari ya Dr. Samia Suluhu Hassan **Tshs. 350,000,000.** Ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo umekamilika isipokuwa ukamilishaji wa bwalo la sekondari ya Dr. Samia upo katika hatua za umaliziaji

- **Ujenzi wa matundu ya vyoo kupitia mradi wa SWASH**

Mwaka 2023/2024 mkoa umepokea kiasi cha Tsh. **833,341,953.58** kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo **330** katika shule **22** katika halmashauri **6.** Ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji isipokuwa kwa Halmashauri ya Nyasa ujenzi upo katika hatua za kupandisha ukuta.

- **Ujenzi wa mabweni kupitia ufadhili wa TEA**

Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. **142,934,332.00** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja katika sekondari ya Darajambili. Ujenzi upo katika hatua ya lenta. Aidha kiasi cha Tshs **118,117,000.00** kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya maabara katika sekondari ya Nyasa. Mradi upo katika hatua ya umaliziaji.

- **Ujenzi wa Miundombinu ya madarasa, mabweni na matundu ya vyoo kupitia Mradi wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R)**

Kwa mwaka fedha 2023/2024 Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs **664,800,000.00** kupitia mradi wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni na matundu ya vyoo katika Halmashauri ya Nyasa, Mbinga DC na Songea MC. Ujenzi unahusisha madarasa **6**, mabweni **4** na matundu ya vyoo **4**. Ujenzi wa miradi hii umekamilika.

- **Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya Elimu Msingi kupitia Programu ya BOOST**

Mkoa umetekeleza mradi wa ujenzi wa shule mpya za Msingi **12**, na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule za Msingi **44**. Miundombinu hii inatekelezwa kupitia Mradi wa BOOST kwa gharama ya Tshs. **7,291,300,000.00.** Ujenzi wa shule zote 12 unaojumuisha shule za awali umekamilika na zimeanza kutumika.

- **Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Walimu**

Mkoa umejenga na kukarabati Vituo vya walimu **12** katika Halmashauri zote 8 za Mkoa kwa gharama ya Tshs. **264,000,000.00**. Vituo vyote vimekamilika na vinatumika.

Aidha kwa kipindi cha mwisho wa mwaka 2023/2024 mwezi Juni 2024, Mkoa umepokea fedha za ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo: -

- **Ujenzi wa Miundombinu ya madarasa, mabweni na matundu ya vyoo kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Mkoa umepokea jumla ya Tshs **3,435,200,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **20**, mabweni **22** na matundu ya vyoo **82**. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuongeza miundombinu katika shule zilizopandishwa hadhi kuwa za kidato cha tano na sita na kuongeza miundombinu kwa shule zilizopangiwa wanafunzi wengi. Miradi hii inatekelezwa katika Halmashauri za Namtumbo, Songea vijijini, Songea Manispaa na Tunduru.

- **Ujenzi wa nyumba za walimu kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Mkoa umepokea jumla ya Tshs **950,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **10** za walimu mbili kwa moja (2 in 1) katika shule za sekondari zilizojengwa kupitia mradi wa SEQUIP awamu ya pili. Ujenzi huu unatekelezwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma.

- **Ujenzi wa shule mpya za sekondari kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) awamu ya tatu**

Mkoa umepokea fedha kiasi cha Tshs. **5,044,975,443.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya **9** za sekondari za Kata ikiwa ni utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP awamu ya tatu. Ujenzi huu unatekelezwa katika majimbo yote 9 ya uchaguzi ndani ya Mkoa wa Ruvuma

- **Ujenzi wa shule mpya za sekondari za Mkondo wa Amali kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Hadi sasa Mkoa umepokea fedha kiasi cha Tshs. **3,842,211,308.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za mkondo wa Amali. Fedha hizi zimeingizwa katika shule zilizopo katika Halmashauri ya Mbinga Vijijini, Tunduru, Mbinga Mji, Madaba na Songea Manispaa.

- **Ujenzi wa miundombinu mbalimbali na shule mpya ya msingi kupitia Mradi wa BOOST**

Mkoa umepokea jumla ya Tshs **3,662,000,000.00** kutoka mradi wa kuboresha ujifunzaji na fursa sawa kwa elimu ya awali na msingi (BOOST) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **95**, matundu ya vyoo **216,** ukarabati wa shule za msingi kongwe **5**, ujenzi wa shule mpya **1** ya mkondo mmoja pamoja na usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi ya Mkoa hadi shule. Ujenzi huu unatekelezwa katika shule za msingi **39** zilizoteuliwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali za ujenzi kama vile ununuzi wa vifaa na uchimbaji wa misingi baada ya mifumo kufunguliwa, hivyo kila halmashauri inaendelea na utekelezaji.

**H. Changamoto katika ujenzi wa miundombinu.**

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi;

a. Wazabuni na mafundi wanaotumika katika ujenzi hawana mitaji badala yake kutegemea malipo ndipo waendelee na ujenzi.
b. Mfumo wa ulipaji kuchukua muda mrefu hali inayochelewesha mradi kuendelea.
c. Uhaba wa mafundi ujenzi katika maeneo ya miradi katika Halmashauri.

d. Kuchelewa kwa mchakato ya wazabuni katika maeneo ya miradi kwenye Halmashauri.

**l. Elimu maalum, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi**

Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ambayo ni Elimu Endelevu inatekelezwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma. Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inayojumuisha Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA), Mpango wa Elimu ya Sekondari kupitia Ujifunzaji huria (Open Learning) unaojumuisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa mtihani wa kujitegemea (PC).

Elimu ya Watu Wazima inahusisha utoaji wa stadi za Kisomo (KKK) kwa watu wazima na Kisomo cha kujiendeleza kwa kupiga vita Umasikini, Maradhi na Ujinga ili kumudu mazingira na kujiletea maendeleo kupitia Elimu ya Ufundi Stadi na shughuli za kijamii na za uzalishaji mali (shughuli za kiuchumi).

Hadi kufikia Agosti, 2024 kuna vituo **109** katika shule za msingi vinavyotekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA). Utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya sekondari katika vituo **125** vinavyoandaa wanafunzi wa mtihani wa kujitegemea (PC) na utekelezaji wa elimu ya ufundi stadi katika vituo vya ufundi stadi **24**.

Utekelezaji wa elimu maalum unafanyika katika shule zote za msingi na sekondari.  Kwa sasa kuna vituo **302** katika shule zilizobainisha watoto wenye mahitaji maalum. Ubainishaji kwa ajili ya usajili wa wanafunzi wenye mahitaji maalum hufanyika kila mwaka kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa mwaka wa masomo unaofuata.

**J. Taarifa za michezo**

Mkoa wa Ruvuma Kuanzia mwaka 2021 - 2024 mkoa umekuwa na mafanikio katika masuala ya michezo kwani mkoa umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka katika michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA kama jedwali Na.55 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 51: Nafasi katika mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA**

| MWAKA | AINA YA MASHINDANO | NAFASI KITAIFA |
|---|---|---|
| 2021 | Umitashumta | 26 |
| | Umisseta | 24 |
| 2022 | Umitashumta | 24 |
| | Umisseta | 22 |
| 2023 | Umitashumta | 22 |
| | Umisseta | 9 |
| 2024 | Umitashumta | 18 |
| | Umisseta | 14 |

Mkoa umeendelea kuhimiza Halmashauri zote kuanzisha vitalu vya ufundishaji michezo ili kuendeleza vipaji kwa wanafunzi. Pamoja na juhudi za Mkoa katika kuendeleza vipaji kwa wanafunzi, Serikali imetupendelea kwa kutupa vituo vitatu maalum

vya michezo tofauti na mikoa mingine yenye vituo viwili. Vituo hivyo ni Mahanje sekondari, Maposeni na Songea Boys. Lengo la shule hizo maalum za michezo ni kuhakikisha wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi na kufaulu masomo yao wanapelekwa katika shule hizo ili kuendelezwa vipaji vyao. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI iligawa mipira 56 kwa mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya mashindano ya Samia Taifa Cup, pamoja na hiyo mkoa ulipokea mira 1,000 kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa ajili ya uendelezaji wa vipaji kwa vijana wanafunzi

- **Hatua za kuboresha michezo**

i. Kila Halmashauri zimeagizwa kuwa na vitalu ambavyo vitawaandaa wanamichezo kuepuka maandalizi ya zimamoto.
ii. Shule ya sekondari ya Mahanje ya Halmashauri ya Madaba kuwa shule inayopokea wanafunzi wenye vipaji mbalimbali vya michezo kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma ili kukuza vipaji vyao.
iii. Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za kuchangia na kuendeleza michezo shuleni katika Mkoa wa Ruvuma

**K. Changamoto katika sekta ya elimu**

i. Wazazi kuhamia mashambani mbali na shule na kuwaacha wanafunzi peke yao hivyo kusababisha baadhi yao kuwa watoro na kuacha masomo.

ii. Baadhi ya wazazi kutokuchangia chakula cha mchana shuleni kwa ajili ya watoto wao

iii. Kutokuwa na shule za kutosha za bweni na kuwepo kwa mabweni na hosteli zisizokidhi mahitaji

iv. Upungufu wa miundombinu na samani

v. Mdondoko mkubwa wa wanafunzi kati ya wanaoandikishwa darasa la kwanza na kidato cha kwanza ukilinganisha na wanaosajiliwa kufanya mitihani ya Taifa.

**Jedwali Na. 52: Mdondoko wa wanafunzi**

| Elimu ya Msingi darasa la Kwanza hadi la Saba | | | | | | | | Elimu ya Sekondari Kidato cha Kwanza hadi cha Nne | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walioandikishwa drs I mwaka 2017 | | | Waliosajiliwa darasa la VII 2023 | | | Waliondondoka | % ya mdondoko | Walioandikishwa kidato cha I mwaka 2020 | | | Waliosajiliwa kidato cha IV 2023 | | | Waliondondoka | % ya mdondoko |
| Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml | | | Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml | | |
| 27228 | 28288 | 55516 | 23077 | 25652 | 48729 | 6787 | 12.23 | 11852 | 13549 | 25115 | 6391 | 7952 | 14343 | 10772 | 42.89 |

**L. Mikakati ya kuongeza ufaulu kwa mwaka 2024**

Ili kuinua ubora wa elimu katika Mkoa wa Ruvuma, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wameelekezwa kuhakikisha yafuatayo yanatekelezwa; -

(i) Serikali za mitaa/vijiji na vitongoji wanasimamia uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuanza darasa la awali na la kwanza katika kipindi cha Septemba hadi Disemba ili ifikapo mwezi Januari watoto waanze masomo kwa pamoja.

(ii) Walimu wa madarasa ya Awali, la kwanza na la pili lazima wawe na maarifa ya kutosha kufundisha madarasa hayo. Walimu wasiokuwa na uwezo wajengewe uwezo kupitia walimu mahiri na MEWAKA.

(iii) Mkoa na halmashauri zihakikishe zinawajengea uwezo wa upimaji katika madarasa ya Awali, la kwanza na la pili ili kubaini wasiojua KKK na kuchukua hatua mapema za kuwasaidia

(iv) Wazazi na uongozi wa shule wahakikishe wanatoa chakula kwa wanafunzi

(v) Wazazi kwa kushirikiana na uongozi wa kata wahakikishe kuwa wanafunzi wote waliofaulu wanaripoti na kuandikishwa mapema na wanamaliza mzunguko wa masomo kufikia kidato cha nne,

(vi) Uongozi wa kata kwa kushirikiana na uongozi wa shule wahakikishe wanafunzi wanaofeli kidato cha pili wanarejea shuleni na kuendelea na masomo katika shule zao.

(vii) Uongozi wa shule uhakikishe kuwa unabaini wanafunzi watoro wote na kuwasilisha taarifa kwenye uongozi wa kata na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

(viii) Kuimarisha ufundishaji wa wanafunzi wa darasa la tatu na kidato cha kwanza ili kuwajengea umahiri katika masomo yao hasa kiingereza na hisabati.

(ix) Kuwa na utaratibu wa kutoa motisha kwa walimu wanaofanya vizuri na kwa wale wanaofanya vibaya.

(x) Kila shule iwe na mradi utakaowezesha shule kuongeza kipato.

(xi) Kufanya ufuatiliaji wa kina na wa mara kwa mara shuleni ili kuona changamoto zinazowakabili walimu katika kutekeleza majukumu yao pamoja na kutatua changamoto hizo na kudhibiti utoro wa walimu.

(xii) Halmashauri ziweke uratibu wa kuwatumia walimu waliohitimu vyuo vikuu kwa masomo ambayo hayana walimu mfano walimu wa Sayansi na Hisabati

(xiii) Wakurugenzi kutenga bajeti/fungu la uendeshaji wa mitihani ya upimaji (MOCK) hasa kwa madarasa ya mitihani

(xiv) Kufanya vikao vya kisheria na dharura ili kuimarisha ushirikishwaji katika masuala yanayotokea shuleni. Hii itasaidia kupunguza migogoro shuleni

(xv) Kila Halmashauri ifanye uchambuzi na tathmini kwa kila mtihani utakao fanyika ili kupima ufundishaji wa walimu.

(xvi) Kuhakikisha wanafunzi wanafanya mitihani na mazoezi ya kutosha ili kuwezesha wanafunzi kujenga kujiamini.

(xvii) Kuimarisha kamati za uthibiti ubora wa ndani kwa kila shule.

(xviii) Kufanya vikao vya kisekta kwa kila robo mwaka kujadili changamoto zinazoikabili sekta na kutatua baadhi za changamoto zinazowakabili walimu kwa ujumla.

(xix) Wakurugenzi wafuatilie na watekeleze ushauri unaotolewa na wathibiti ubora juu ya shule zao kwa wakati.

(xx) Kila shule ya msingi na sekondari zihakikishe zinaandaa viwanja vya michezo na kusimamia michezo kwa mujibu wa ratiba.

## 2.20 Sekta ya Maji

### 2.20.1 Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA)

#### A. Utangulizi

Mkoa wa Ruvuma unakadiriwa kuwa na jumla ya watu 1,848,794 (Sensa, 2022). Watu 1,479,035 sawa na 80% wanakadiriwa kuishi maeneo ya vijijini.

#### B. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijiini

Asimilia 70.69 ya watu wanaoishi vijijini ambao ni sawa na watu 973,833 ndio wanapata huduma ya maji safi na salama. Lengo la Mkoa ni kufikia asilimia 85 kwa wakazi wote washio vijijini na asilimia 95 kwa wakazi washio Mjini ifikapo mwaka 2025 kwa

mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025. Jedwali **Na. 53** linaonesha hali ya huduma ya Maji kwa kila Halmashauri

**Jedwali Na. 53: Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kila Halmashauri**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya wakazi | Idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji | Idadi ya vituo | Idadi ya vituo Vinavyofanya kazi | Asilimia ya upatikanaji Maji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea | 178,201 | 130,783 | 2, 916 | 2,650 | 73.3 |
| 2 | Madaba | 65,215 | 47,490 | 1,481 | 1,395 | 72.8 |
| 3 | Tunduru | 362,394 | 253,899 | 1,312 | 1,141 | 70.6 |
| 4 | Mbinga DC | 285,582 | 202,763 | 1451 | 1414 | 71 |
| 5 | Mbinga TC | 98,064 | 74,528 | 563 | 485 | 76 |
| 6 | Namtumbo | 225,466 | 160,081 | 1,719 | 1,587 | 71 |
| 7 | Nyasa | 191,193 | 104,289 | 2617 | 2506 | 60.1 |
| **Jumla** | | **1,406,115** | **973,833** | **9,143** | **11,178** | **70.5** |

***Chanzo:*** *Ofisi za RUWASA Wilaya kufikia 30 Juni**, 2024***

- **Mahitaji ya Maji kwa Mkoa**

Mahitaji ya maji katika Mkoa wa Ruvuma yanakadiriwa kufikia lita za ujazo 33,523.5 kwa siku kwa wastani wa lita 25 kwa mtu. Upatikanaji wa huduma ya maji katika Mkoa kwa mwaka 2024 ni lita za ujazo 58,790.8 ambazo zinahudumia jumla ya watu 973,833 waishio vijijini. Mahitaji ya huduma ya Maji kwa kila Halmashauri ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na. 54.

**Jedwali Na. 54: Mahitaji na Huduma ya Majisafi na Salama Vijijini 2024**

| Na. | Halmashauri | Mahitaji ya Maji (M3/SIKU) | Uzalishaji wa Maji ($M^3$/SIKU) |
|---|---|---|---|
| 1 | Songea | 3,269.625 | 28,080 |
| 2 | Madaba | 1,187.250 | 9,384 |
| 3 | Tunduru | 9,059 | 6,347 |
| 4 | Mbinga DC | 7,139.55 | 5,963.8 |
| 5 | Mbinga TC | 2,451.6 | 2,192 |
| 6 | Namtumbo | 5,636.7 | 4,012 |
| 7 | Nyasa | 4,779.8 | 2,812 |
| **Jumla** | | **33,523.525** | **58,790.8** |

***Chanzo:*** *Ofisi za RUWASA Wilaya katika Mkoa wa Ruvuma kufikia 30 Juni,* ***2024***

## C. Mpango na Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini kwa Mwaka wa Fedha 2023/24

Katika bajeti ya Mwaka wa fedha 2023/24, Mkoa wa Ruvuma umetengewa jumla **TSh 22,405,174,224.97** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Hadi kufikia 30 Juni, 2024 Mkoa umepokea jumla ya **Tsh. 14,649,981,811.34 (65.8%)**. Mchanganuo wa bajeti na mapokezi ya fedha kwa kila Wilaya ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na. 55

**Jedwali Na. 55: Mpango na bajeti ya Miradi ya maji vijijini kwa kila Wilaya.**

| Na | Wilaya | Bajeti 2023/2024 | Fedha Pokelewa Hadi 30 Juni,2024 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga | 6,795,964,812.02 | 4,427,570,254.53 |
| 2 | Namtumbo | 2,810,986,031.39 | 1,910,885,016.07 |
| 3 | Nyasa | 2,459,067,532.65 | 769,940,074.51 |
| 4 | Songea | 4,678,691,793.36 | 2,873,619,924.34 |
| 5 | Tunduru | 5,500,594,055.71 | 4,667,966,541.89 |
| | | **22,245,304,225.13** | **14,649,981,811.34** |

Mkoa kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 imepokea fedha kiasi cha **TSh. 7,632,995,220.58** kwa ajili ya kulipa madai ya wakandarasi na madai yote yamelipwa kwa wakandarasi husika.

**D. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi hadi 30 Juni, 2024**

- **Miradi iliyokamilika hadi Juni, 2024**

Hadi kufika 30 Juni, 2024 Jumla ya miradi 18 yenye jumla ya **TSh. 20,115,564,233.94** ilikuwa imekamilika kwa asilimia 99 na inatoa huduma kwa wananchi zaidi ya 68,000 na Vijiji 23 vinapata huduma ya maji. Orodha ya miradi iliyokamilika ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na. 56

**Jedwali Na. 56: Orodha ya miradi iliyokamilika**

| Na | Halmashauri | Jina la Mradi | Gharama ya Mradi |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Ruvuma Chini | 1,315,905,699.80 |
| 2 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Mbangamao | 1,810,439,739.89 |
| 3 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Utiri | 428,434,691.91 |
| 4 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Kitanda | 473,101,856.40 |
| 5 | Mbinga TC | Mradi wa maji Mkwaya | 375,139,800.00 |
| 6 | Mbinga TC | Mradi wa maji Luwaita | 273,701,057.24 |
| 7 | Mbinga TC | Mradi wa maji Tanga | 817,492,457.71 |
| 8 | Mbinga DC | Mradi wa Maji Kihuruku na Luhagara | 1,163,502,774.00 |
| 9 | Mbinga DC | Mradi wa Maji Mabuni | 157,188,980.00 |
| 10 | Mbinga DC | Mradi wa maji Ruanda | 396,001,772.00 |
| 11 | Mbinga DC | Mradi wa maji Matiri | 1,671,665,426.67 |
| 12 | Tunduru DC | Mradi wa maji semeni na muhuwesi | 485,946,240.00 |
| 13 | Songea DC | Mradi wa Maji Peramiho A | 336,625,870.00 |
| 14 | Songea DC | Mradi wa Maji Lyangweni | 548,658,000.00 |
| 15 | Madaba | Mradi wa Maji Mbangamawe | 453,6475,600.00 |
| 16 | Namtumbo | Mradi wa Maji Litora Kumbara | 2,230,172,084.32 |
| 17 | Namtumbo | Mradi wa Maji Likusanguse | 527,780,284.00 |
| 18 | Nyasa | Mradi wa Maji ngombo Phase I | 2,567,331,900.00 |
| | **JUMLA YA GHARAMA ZA MIRADI ILIYOKAMILIKA** | | **20,115,564,233.94** |

***Chanzo:*** *Ofisi za RUWASA Wilaya kufikia 30 Juni**, 2024***

- **Miradi inayoendelea hadi 30 Juni, 2024**

Hadi kufikia 30 Juni, 2024, Mkoa wa Ruvuma ulikuwa una jumla ya miradi 31 inayoendelea kutekelezwa, yenye Jumla ya **TSh. 65,875,384,905.31** ambapo hadi 30 Juni, 2024 **TSh. 21,393,424,794.09,** kati ya **TSh. 65,875,384,905.31** zilikuwa zimelipwa. Orodha ya Miradi inayoendelea hadi 30 Juni, 2024 ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na.57.

**Jedwali Na. 57: Orodha ya Miradi inayoendelea hadi 30 Juni, 2024**

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea DC | Mradi wa Maji wa vijiji vya Kizuka,Lipaya na Lipokela | 3,402,065,438.14 | 2,107,812,068.00 | 2,107,812,068.00 | **Kijiji cha Lipokera**<br>Ujenzi wa chanzo-98%, Ujenzi wa sump tanki-100%, -Ujenzi wa nyumba ya Mtambo-100%,<br>Ujenzi wa tanki la lita 100,000-98%, -Ununuzi wa pampu na ufungaji-85%, -Ufungaji wa laini ya umeme-100%, Ujenzi wa vituo 18-90%, Uchimbaji wa mtaro na kulaza bomba 20-60% na<br>Ununuzi wa bomba 20km-80%<br>**Wastani wa utekelezaji-90.1%**<br><br>**Kijiji cha Kizuka**<br>Ujenzi wa nyumba ya Mtambo-100%,-Ujenzi wa tanki la juu lita 150,000-85%,Ununuzi wa pampu na ufungaji-85%,Ufungaji wa laini ya umeme-100%, Ujenzi wa vituo 11-90%,Uchimbaji wa mtaro na kulaza bomba 11-80%, Ununuzi wa bomba 11km-100%<br>**Wastani wa utekelezaji-88.6%** |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | **Kijiji cha Lipaya** Ujenzi wa chanzo-100%, Ujenzi wa tanki lenye lita 100,000-100%,Ujenzi wa vituo 17-100%, Ununuzi wa bomba 23km-100%, Uchimbaji na ulazaji wa bomba 23km-98%. **Wastani wa utekelezaji 99%** |
| 2 | | Mradi wa Maji Liweta | 635,634,451.00 | 124,364,314.00 | 124,364,314.00 | Ujenzi wa nyumba ya Mtambo-95%, -Ujenzi wa tanki la juu lita 100,000-20%, Ujenzi wa vituo 10-98%, **Wastani wa utekelezaji-42%** |
| 3 | Madaba | Mradi wa maji Gumbiro | 987,902,670.00 | 76,185,400.00 | 76,185,400.00 | Ujenzi wa tanki la juu mita sita lenye lita 75,000-95%, Ujenzi wa vituo 10-90%, **Wastani wa utekelezaji 49%** |
| 4 | | Mradi wa Maji Ndelenyuma na Lutukira | 1,614,363,301.00 | 768,110,151.38 | 768,110,151.38 | Ujenzi wa chanzo-100%, Ujenzi wa sump tanki-100%, Ujenzi wa nyumba ya Mtambo-100%, Ujenzi wa tanki la juu lita 100,000-90%, Ununuzi wa pampu na ufungaji-90%, Ufungaji wa laini ya umeme-100%, Ujenzi wa vituo 15-90%, Uchimbaji wa mtaro na kulaza bomba 23.7-80%,Ununuzi wa bomba 23.7km-27.4%. **Wastani wa utekelezaji-83%** |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | | Mradi wa Maji Mtangimbole | 5,565,324,305.08 | 1,484,798,645.76 | 1,484,798,645.76 | Ujenzi wa tanki la juu lenye lita 150,000-85%, Ujenzi wa tanki la chini lita 200,000-85%, Ujenzi wa vituo 40-0%, Ununuzi wa bomba 49km-12.2%,Uchimbaji na ulazaji wa bomba 49km-30% **Wastani wa utekelezaji 40.5%** |
| 6 | | Mradi wa Maji Ngadinda | 1,468,929,252.00 | 270,404,844.00 | 270,404,844.00 | Ujenzi wa Sump tank- 90%, Ujenzi wa Nyumba ya Mtambo -70%, Ujenzi wa tanki la juu lenye lita 200,000- 40%, **Wastani wa Utekelezaji – 40%** |
| 7 | | Upanuzi wa mradi wa Maji Lilondo | 251,358,496.00 | 215,385,681.00 | 215,385,681.00 | Ujenzi wa chanzo-10%, Uchimbaji na ulazaji wa bomba 12.6km-80%.**Wastani wa utekelezaji-50%** |
| 8 | Namtumbo DC | Mradi wa Maji Luhimbalilo Naikesi | 3,168,334,997.72 | 2,596,487,868.42 | 2,596,487,868.42 | Ujenzi wa chanzo cha Maji 100%, Ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji Lita 200,000-95% na Lita 100,000-95%, .Ujenzi wa vituo 53 vya Kuchotea Maji-85%, Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba (bomba Kuu na Bomba la usambazaji) km-98%, Ujenzi wa ofis ya chombo cha watumiaji Maji-0%. Utekelezaji wa mradi ni 86 % na ujenzi wa mradi unaendelea. |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | | Mradi wa Maji Mgombasi | 2,734,991,792.00 | 415,473,492.40 | 415,473,492.40 | Ujenzi wa chanzo cha Maji 100%, Ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji Lita 300,000-90%, Ujenzi wa vituo 30 vya Kuchotea Maji-85%, Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba (bomba Kuu na Bomba la usambazaji) km-65%. Utekelezaji wa mradi ni 78% , ujenzi wa mradi unaendelea |
| 10 | | Mradi wa Maji Msisima/Mnalawi | 1,115,824,600.00 | 147,373,690.00 | 147,373,690.00 | Ujenzi wa chanzo cha Maji 75%, Ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji (Sump) Lita 50,000-0%, Ujenzi wa nyumba ya pump (Pump House) 0%, Ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji Lita 200,000-45%, Ujenzi wa vituo 16 vya Kuchotea Maji-0%, Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba (bomba Kuu na Bomba la usambazaji) km-0%, Ujenzi wa Ofisi ya chombo cha watumiaji Maji -0%. Utekelezaji wa mradi umefikia 35% na ujenzi wa mradi unaendelea |
| 11 | | Mradi wa Maji Mchomoro | 2,267,593,020.60 | 320,138,953.00 | 320,138,953.00 | Ujenzi wa chanzo cha Maji 40%, ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji (Sump) Lita 75,000-0%, Ujenzi wa nyumba ya pump (Pump House) 0%, Ujenzi wa tenki la kuhifadhi Maji Lita 300,000-20%, Ujenzi wa vituo 25 |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | vya Kuchotea Maji-0%, Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba (bomba Kuu na Bomba la usambazaji) 41.5km-0%, Ujenzi wa Ofisi ya Chombo cha watumiaji Maji-0%. Utekelezaji upo 20% |
| 12 | **Tunduru DC** | Ujenzi wa Mradi wa Maji Ndaje - Mbesa **PHASE II** | 1,500,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | Uchimbaji na ufungaji wa bomba umefikia 22km kati ya 24m. Utekelezaji umefikia asilimia 50. |
| 13 | | Mradi Maji Masuguru-Mchoteka | 2,416,574,071.52 | 795,279,030.43 | 795,279,030.43 | Ujenzi wa intake ya kuelea umekamilika,Ufungaji wa pampu na solar panel 125 umekamilika,Ujenzi wa pampu house umefanyika,Ujenzi wa tenki la 500m3 umefanyika, Uchimbaji na ufungaji wa bomba umefanyika 11km kati ya km24,vituo vimejengwa 15 kati ya vituo 24,Vijiji viwili(masuguru na mchekeni) vinapata huduma ya maji kati ya vijiji 7 bado vijiji 5(Mchoteka,Mkolola,Kitani,Mnemasi,Likweso).Utekelezaji umefikia asilimia 77 |
| 14 | | Mradi wa maji Ligoma, Makoteni, na | 1,451,962,121.38 | 621,151,351.61 | 621,151,351.61 | Ujenzi wa matenki 3 umekamilika,Ukarabati wa tenki moja umekamilika,Ujenzi wa vituo 28 umekamilika ufungaji wa pampu tatu |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Imani , majimaji na chalinze | | | | umefanyika,Ujenzi wa pampu house tatu umefanyika,Uchimbaji na ufungaji wa mabomba 38km umefanyika na vijiji 3(Ligoma,Makoteni,Imani) vinapata huduma ya maji bado vijiji viwili kuingiza umeme(majimaji na chalinze).Utekelezaji umefikia asilimia 95. |
| 15 | | Mradi wa Maji Misechele&Liwanga | 3,020,150,910.00 | 453,022,636.60 | 453,022,636.60 | Ujenzi wa intake umefanyika, ujenzi wa pampu house umefanyika, Ujenzi wa Sumpwell 75m3 umefanyika ,Ujenzi wa tenki 300m3 umefanyika,Uchimbaji na ufungaji wa bomba umefanyika 9km,Ujenzi wa ofisi ya CBWSO imefikia hatua ya umaliziaji. Utekelezaji umefikia asilimia 77 |
| 16 | | Mradi wa Maji Msinji | 1,069,014,450.00 | 160,352,167.50 | 160,352,167.50 | Ujenzi wa miundombinu bado haujaanza mkandarasi bado hajalipwa advance payment.. |
| 17 | | Mradi wa Maji Tuwemacho | 1,054,232,603.55 | 328,752,441.76 | 328,752,441.76 | Ujenzi wa intake unaendelea,Ujenzi wa tenk unaendelea.Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 70. |
| 18 | | Mradi wa Maji Hulia | 1,206,605,519.28 | 180,990,827.89 | 180,990,827.89 | Ujenzi wa intake umefanyika ,Ujenzi wa tenki la 135m3 umefanyika,Ujenzi wa Office ya CBWSO inaendelea na ujenzi,Uchimbaji |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | na ufungaji wa bomba umefanyika 1010m kati ya 7014m<br>Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 50. |
| 19 | NYASA DC | Mradi wa Maji Lituhi | 6,595,019,722.69 | 3,091,485,406.00 | 3,091,485,406.00 | Ujenzi wa Intake umekamilika kwa 95%<br>Ujenzi wa tanki 1 lenye ujazo 500M3 umekamilika kwa 95%<br>Bomba kuu na la usambazaji 42.7km sawa na 64%<br>Ujenzi wa vituo 24 vilivyo utekelezaji umefikia 95%<br>Ujenzi wa ofisi ya CBWSO (0%)<br>**Wastani wa utekelzaji ni asilimia 70** |
| 20 | | Mradi wa Maji Liuli | 4,718,087,447.85 | 1,881,595,665.03 | 1,881,595,665.03 | Ujenzi wa Intake umekamilika kwa 98%<br>Ulazaji wa bomba kuu 12.276km imekamilika kwa 95%<br>Ujenzi wa matanki 3 yenye ujazo 300M3 lipo kijiji cha Hongi, 135M3 lipo kijij cha Mkalachi na 100M3 lipo kijiji cha Liuli umekamilika kwa 95%<br>Ulazaji wa bomba la usambazaji umekamilika kwa 95%<br>Ujenzi wa vituo 19 vya kuchotea maji (DPs) umekamilika kwa 95% |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Ujenzi wa ofisi ya CBWSO (55%)<br>Wastani wa utekelzaji ni asilimia 95<br>Na mradi upo hatua za mwisho za ukamilishaji |
| 21 | | Mradi wa Ngumbo PHASE I&II | 4,598,000,400.00 | 2,059,725,545.72 | 2,059,725,545.72 | Ulazaji wa bomba la usambazaji umefanyika 27.986 kati ya 29.516 sawa 94%,Ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji kati ya 30 sawa na asilimia 33%<br>Ujenzi wa ofisi ya CBWSO (0%)<br>**Wastani wa utekelezaji ni asilimia 69. Utekelezaji unaendelea.** |
| 22 | | Mradi wa Maji Nangombo - Kilosa | 4,134,064,577.50 | 620,109,689.00 | 620,109,689.00 | Ujenzi wa Intake Haujaanza sawa na 0%<br>Ulazaji wa bomba kuu umekamilika kwa 44%<br>Ujenzi tanki 1 lenye ujazo 1000M3 Haujaanza sawa 0%<br>Ulazaji bomba la usambazaji Haujaanza sawa na 0%<br>Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji (DPs Haujaanza sawa na 0%<br>**Utekelezaji kwa ujumla: 8%** |
| 23 | | Mradi wa Maji | 1,022,715,230.38 | 522,272,882.00 | 522,272,882.00 | Ujenzi wa Intake umekamilika kwa 95% |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Malungu | | | | Ulazaj wa bomba kuu na usambazaji umekamilika kwa 90%<br>Ujenzi wa anki 1 lenye ujazo 100M3 lipo kijiji cha malungu limekamilika kwa 85%<br>Ujenzi wa vituo 11 vya kuchotea maji (DPs umekamilika kwa 85%<br>**Utekelezaji kwa ujumla: 85%** |
| 24 | | Mradi wa Maji Puulu Songambele | 1,839,631,098.40 | 0 | 0 | Ujenzi wa Intake unaendelea sawa na 60%,Ujenzi wa tanki 1 lenye ujazo 200M3 umeanza hatua ya msingi sawa na 5%<br>Uchimbaji wa mtaro umefanyika km 3.2<br>Ukarabati wa tanki 1 la lita 100,000. Utekelezaji 0%,<br>**Utekelezaji kwa ujumla: 12%** |
| 25 | | Mradi wa Maji Mtupale | 353,441,287.78 | 262,232,941.21 | 262,232,941.21 | Kuendelea na kazi ya uchimbaji wa mtaro kwa bomba kuu na la usambazaji kwa ajili ya ulazaji wa bomba.<br>**Wastani wa utekelezaji ni asilimia 30** |
| 26 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Myangayanga | 228,432,680.00 | 100,000,000.00 | 100,000,000.00 | Uchimbaji mtaro, ulazaji wa bomba, ufukiaji umbali wa km.5 kutoka chanzo hadi kwenye tanki la kuhifadhia maji -100%, Ujenzi wa intake umekamilika-100%, Ukarabati wa tank la kuhifadhia maji-100%, |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Ujenzi wa vituo 14-100%. **Utekelezaji Jumla ni asilimia 70** |
| 27 | Mbinga DC | Mradi wa Maji Maguu | 742,369,771.50 | 235,481,146.14 | 235,481,146.14 | Tenki limejengwa la Lita 150,000-80%, Uchimbaji wa Mtaro na ulazaji wa Bomba za njia kuu ya kutoka chanzo hadi tenki umbali wa km1.3-100%, ujenzi wa Vituo vya kutchotea maji-100%, Mkandarasi anasubiri bomba zinunuliwe na RUWASA ili alaze. **Utekelezaji jumla ni asilimia 60** |
| 28 | | Mradi wa Maji Ndongosi | 660,000,000.00 | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 | Ujenzi wa tenki -100%, Uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba-100%, ujenzi wa vituo-100%, Ujenzi wa chanzo-20%. **Utekelezaji ni asilimia 90** |
| 29 | | Mradi wa Maji Kitura | 1,472,413,443.14 | 367,385,867.24 | 367,385,867.24 | Uchimbaji mtaro km 20 na ulazaji wa bomba km.8 –54.9%, Ujenzi wa chanzo uko 90%, Ujenzi wa tenki la lita 150,000-80%, Ujenzi wa tenki la Lita 75,000 –80%, Ujenzi wa tenki la lita 100,000-60%,ujenzi wa BPT -80% **Utekelezaji ni asilimia 60** |
| 30 | | Mradi wa Maji Kambarage | 2,884,478,730.00 | 432,671,810.00 | 432,671,810.00 | Ujenzi wa chanzo uko 96%.Mitaro imechimbwa umbali wa km.29.5 na bomba zinaendelea kulazwa -78%, Ujenzi wa tenki |

| Na | H/SHAURI | JINA LA MRADI | GHARAMA YA MRADI | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | -20%. **Utekelezaji jumla ni asilimia 40** |
| 31 | | Mradi wa Maji Amanimakolo | 1,695,868,516.80 | 254,380,278.00 | 254,380,278.00 | Tenki limefunikwa na kupigwa plasta -90%, Bomba zimenunuliwa na ulazaji unaendelea wastani wa km 4-20%. **Utekelezaji Jumla ni asilimia 40** |
| **Miradi imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya fedha kuchelewa kutolewa kwa wakati** | | | | | | |

*Chanzo: Ofisi za RUWASA Wilaya katika Mkoa wa Ruvuma kufikia 30 Juni **2024***

Miradi hii 31 ikikamilika itakuwa inahudumia zaidi ya wananchi **264,742**, vijiji **78** na kuongeza asilimia ya upatikanaji wa huduma ya maji toka asilimia 70.5 ya sasa hadi asilimia 80.3

**E. Changamoto**

Sekta ya Maji katika Mkoa wetu inakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:-

i. Uharibifu wa mazingira unachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu vyanzo vya maji na kupelekea kuwa na upungufu wa maji katika vyanzo vingi vya maji hasa wakati wa kiangazi,

ii. Kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya wakandarasi na wazabuni na hivyo kusababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati.

iii. Kuchelewa michakato ya upatikanaji wa Misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT Exemption) kwa miradi inayohitaji msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani hivyo kuchelewesha utekelezaji.

iv. Changamoto ya vitendea kazi hasa Ofisi na vyombo vya usafiri hususani magari kwa ajili ya usimamizi wa miradi kwenye Ofisi za Meneja wa Wilaya

### F. Utatuzi wa changamoto

Mkoa umeendelea kukabiliana changamoto hizo kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kuelimisha wananchi kuacha shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ya vyanzo vya maji,

i. Kuendelea kukumbushia Wizara ya Maji kupitia Mkurugenzi Mkuu RUWASA kutuma fedha za miradi kwa wakati,

ii. Kuzingatia mahitaji na matakwa ya mfumo wa kuombea msamaha wa kodi la ongezeko la thamani TRA ili kuwezesha upatikanaji wa Misamaha ya kodi kwa wakati,

iii. Kuendelea kukumbushia Wizara ya Maji kupitia Mkurugenzi Mkuu RUWASA juu ya ununuzi wa vitendea kazi hasa magari na ujenzi wa ofisi za mameneja wa Wilaya na Mkoa.

## 2.20.2 Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (SOUWASA)

### A. Utangulizi

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) chini ya Wizara ya Maji inatekeleza azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi wote Majisafi na salama ili kufikia uchumi wa kati wa juu ifikapo mwaka 2025. SOUWASA inaendelea kutekeleza miradi na kazi mbalimbali kwa kuzingatia mipango na maazimio ya maendeleo ya ndani na nje ya nchi ikiwemo Sera ya Taifa ya Majisafi ya Mwaka

2002 (NAWAPO, 2002); Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji Na 11 ya Mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na 5 ya mwaka 2019 pamoja na kanuni zinazoelekeza utekelezaji wa sheria hizo, Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2025); Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2016 – 2030); na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

- **Utekelezaji wa shughuli za Taasisi**

Manispaa ya Songea ina wakazi wapatao **286,285** kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa iliyofanyika mwaka 2022. Manispaa inakadiriwa kuwa na wakazi **306,676** katika mwaka 2024. Wakazi **260,733** wanapata huduma ya maji sawa na asilimia **90.5**. Mahitaji ya maji ni wastani wa lita milioni **20.593** kwa siku kwa mwaka 2024 katika maeneo yote ya Manispaa.Uzalishaji wa maji ghafi ni wastani wa mita za ujazo **8,370** kwa siku. Wastani wa upatikanaji wa huduma ya Majisafi ni saa **23.15** kwa siku. Mamlaka inatekeleza miradi ya maji mijini ili kiwango cha utoaji huduma kifikie asilimia **95** ifikapo mwaka 2025 kama ilani ya chama tawala inavyoelekeza.

- **Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya miradi nane yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania **149,554,326,165.19** iliidhinishwa kutekelezwa ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi za

kitanzania **145,773,015,609.69** kiliidhinishwa kwa ajili ya Mradi wa kimkakati wa miji 28 katika Manispaa ya Songea na kiasi cha Shilingi za Kitanzania **3,781,310,555.50** kilitolewa na Wizara ya Maji kwa Mamlaka. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 58: Mchanganuo wa Miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2023/24**

| Na | Jina la Mradi | Shughuli zilizofanyika | Fedha zilizoidhinishwa (TZS) | Fedha zilizotolewa (TZS) | Fedha zilizotumika (TZS) | Hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa Maji Safi Katika Mji wa Tunduru | • Ununuzi wa bomba nza usambazaji maji na viungio km 22.1<br>• Uchimbaji mtaro na ulazaji wa bomba.<br>• Ununuzi wa dira za maji 1000. | 596,972,005.50 | 140,660,965.00 | 140,660,965.00 | 100% | Mradi umekamilika |
| 2. | Mradi wa Maboresho ya Uzalishaji Maji Katika Mji wa Tunduru | • Uchimbaji wa kisima kirefu cha maji<br>• Marekebisho ya nyumba ya pampu<br>• Marekebisho ya tenki la kuhifadhi maji za ujazo 225<br>• Ununuzi wa bomba za kusukuma maji km 6<br>• Ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba ya pampu, visima na tenki | 355,080,000.00 | 53,262,000.00 | 53,262,000.00 | 60% | Mradi Unaendelea |

| Na | Jina la Mradi | Shughuli zilizofanyika | Fedha zilizoidhinishwa (TZS) | Fedha zilizotolewa (TZS) | Fedha zilizotumika (TZS) | Hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| 3. | Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa Maji Safi Eneo la Mwengemshindo Katika Manispaa ya Songea | • Ununuzi wa bomba za usambazi maji na viungio km 26.5<br>• Uchimbaji wa mtaro na kuunga bomba km 26.5 | 547,521,500.00 | 547,521,500.00 | 547,521,500.00 | 100% | Mradi umekamilika |
| 4. | Ujenzi wa Mradi wa Maji Eneo la Viwanda Lilambo Katika Manispaa ya Songea | • Manunuzi ya vifaa vya ujenzi<br>• Ujenzi wa nyumba ya mtambo(Pump house)<br>• Kufunga mfumo wa umeme kutoka Tanesco<br>• Ujenzi wa Tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 150000<br>• Uchimbaji wa kisima | 415,980,885.10 | 326,072,362.50 | 326,072,362.50 | 100% | Mradi umekamilika |

| Na | Jina la Mradi | Shughuli zilizofanyika | Fedha zilizoidhinishwa (TZS) | Fedha zilizotolewa (TZS) | Fedha zilizotumika (TZS) | Hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kirefu chenye maji. | | | | | |
| 5 | Mradi wa Kufunga Mfumo wa Umeme wa jua Katika Mji wa Tunduru | • Ufungaji wa mfumo wa umeme katika visima vya uzalishaji maji<br>• Ujenzi wa fensi kuzunguka eneo la visima | 367,764,814.60 | 154,074,953.73 | 154,074,953.73 | 100% | Mradi Umekamilika |
| 6 | Mradi wa upanuzi wa mtandao wa Majisafi katika eneo la Luwawasi Katika Manispaa ya Songea | • Ununuzi wa bomba za usambazi maji na viungio km 20.1<br>• Uchimbaji wa mtaro na kuunga bomba km 20.1 | 329,127,960.30 | 203,223,311.30 | 128,185,135 | 5% | Mradi Unaendelea |
| 7 | Ujenzi wa Mradi wa Maji Eneo la Subira Katika Manispaa ya Songea | • Ujenzi wa nyumba 2 za pampu<br>• Kufunga mfumo wa umeme kutoka TANESCO<br>• Ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji | 1,168,863,390.00 | 350,659,017.00 | 350,659,017.00 | 40% | Mradi Unaendelea |

| Na | Jina la Mradi | Shughuli zilizofanyika | Fedha zilizoidhinishwa (TZS) | Fedha zilizotolewa (TZS) | Fedha zilizotumika (TZS) | Hatua ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 200,000<br>• Ununuzi wa bomba ,uchimbaji wa mitaro na ulazaji bomba km 42.5 | | | | | |
| 8 | Mradi wa kimkakati wa miji 28 katika Mji wa Songea | • Ujenzi wa matenki matatu ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita 9,000,000<br>• Ujenzi wa kidaka maji katika mto njuga<br>• Ujenzi wa mtambo wa kutibu ma kuchuja maji | 145,773,015,609.69 | 21,865,952,341.45 | 21,865,952,341.45 | 3% | Mradi Unaendelea |
| **Jumla** | | | **149,554,326,165.19** | **23,641,426,450.98** | **23,566,388,274.68** | | |

**Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali**

**Jedwali Na. 59:** **Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali**

| Na. | Makisio | Makusanyo Halisi | Asilimia ya Makusango | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 4,821,858,660.00 | 4,362,739,878.86 | 90% | Makusanyo yanayotokana na maduhuli ya huduma ya Majisafi na uondoaji wa Majitaka. |
| 2. | 349,245,482.22 | 444,502,083.20 | 127% | Makusanyo yanayotokana na vyanzo vingine |
| | **5,171,104,142.22** | **4,807,241,962.06** | | |

- **Changamoto**

i. Miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na fedha kutokufika kwa wakati

ii. Chanzo cha maji cha bwawa kilichoainishwa katika mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa miji 28 kutokidhi mahitaji ya manispaa ya Songea hivyo kulazimu Mamlaka kutumia chanzo mbadala kilichopelekea kuchelewa kuanza kwa Mradi huo

- **Utatuzi wa Changamoto**

i. Mamlaka imekuwa ikiwasiliana na kuikumbusha Wizara ya maji kuhusu kutolewa kwa fedha za miradi ili ikamilike kwa wakati.

ii. Mamlaka kwa kushirikiana na Bonde la mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Wizara ya Maji na Wananchi imepata chanzo cha maji cha mto Njuga katika eneo la Kijiji cha Kikunja kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

- **Mafanikio**

Upatikanaji maji umeongezeka kutoka asilimia **85** mwezi Juni,2023 mpaka **90.**5 mwezi Juni,2024 kwa mji wa Songea.

## 2.21 Maendeleo ya Jamii.

### A. Utangulizi

Sekta ya Maendeleo ya jamii imekuwa ikiishirikisha jamii katika kutekeleza shughuli mbalimbali zenye lengo la kuboresha maisha ya wananchi katika nyanja za uchumi, kijamii pamoja na maendeleo ya jinsia. Baadhi ya shughuli ambazo hufanyika ni pamoja na:-

i. Kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa nyumba bora ambapo asilimia 70 ya wananchi wanaishi katika makazi bora.

ii. Ushirikishwaji wa wananchi katika upangaji wa mipango na utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika maeneo yanayowazunguka.
iii. Utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wananchi na uimarishaji wa vikundi mbalimbali vya kiuchumi ambao hufanyika kupitia Halmashauri.

**B. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Utoaji wa Mikopo ya 10% inayotokana na Mapato ya Ndani ya Halmashauri; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 mikopo haikutolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu hii ni kutokana na fedha nyingi kutorejeshwa kwa wakati. Kati ya fedha Tsh 6,324,993,424.33 zilizokopeshwa Mkoa umefanikiwa kukusanya Tsh 3,709,755,029.66 na kubakiwa na Tsh 2,873,064,509.02 ambazo bado hazijarejeshwa. Jitihada za kuwapeleka wanadaiwa polisi na mahakamani zinaendelea kufanyika ili mikopo yote iweze kurejeshwa na kutoa fursa kwa watu wengine kuweza kupata mikopo. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 Mkoa wa Ruvuma unatarajia kutoa mikopo ya 10% inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri Jumla **Tsh. 2,625,220,200.00** kwa mchanganuo

ufuatao; Wanawake **Tsh. 1,050,088,080.00**, Vijana **1,050,088,080.00** na Watu wenye Ulemavu **525,044,040.00**.

## C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III)

- **Utangulizi**

Katika Mkoa wa Ruvuma Mpango wa kunusuru kaya masikini ulianza kutekelezwa rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru tarehe 04/11/2014 na baadae kutekelezwa kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016.

Mpango wa kunurusu kaya za Walengwa awamu ya tatu upo katika kipindi cha pili (2020 – 2025) cha utekelezaji ambapo kwa Mkoa wa Ruvuma unatekelezwa kwenye Halmashauri zote nane (8), na katika vijiji/Mitaa **685.**

Lengo kuu la Mpango wa Kunusuru Kaya za Walengwa Sehemu ya Pili ni kuziwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu kama chakula, huduma za Afya na Elimu kwa lengo la kujenga, kuendeleza na kulinda rasilimali watu kwenye kaya za walengwa hususani watoto.

- **Idadi ya Walengwa wa utekelezaji wa Mpango wa kunusuru kaya za masikini Mkoani Ruvuma.**

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Juni, 2024 jumla ya kaya **65,089** zinaendelea kunufaika na Mpango huu. Aidha, kwa sasa Mpango huu upo katika sehemu ya pili ya utekelezaji na unahusisha vijiji/mitaa **685** kutoka katika Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma. Aidha, katika kipindi hiki kuna kaya ambazo zimehitimu katika Mpango kwa Mkoa wa Ruvuma Jumla ya Kaya **18,912** zimehitimu, baada ya kuboresha kipato cha kaya na kupata mahitaji ya msingi.

- **Uhawilishaji Fedha**

Uhawilishaji fedha unahusisha utoaji wa ruzuku kwa kaya za walengwa, hususan zenye watoto ili ziweze kupata lishe bora na mahitaji muhimu ya shule na kupata huduma za afya. Aina hii ya ruzuku inaitwa ruzuku yenye masharti ambayo mlengwa anatakiwa kuyatimiza. Uhawilishaji fedha pia unafanyika kwa kutoa ruzuku ya shilingi **12,000** kwa mwezi kwa kila kaya ili kaya maskini ziweze kuongeza kipato kupitia uwekaji akiba na kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Kuanzia Julai, 2023 hadi, Machi 2024, Mkoa na Halmashauri umepokea jumla ya shilingi **19,583,886,550.2** kwa ajili ya uhawilishaji kwa mgawanyo ufuatao: Malipo ya walengwa

shilingi **18,443,731,993.5** Usimamizi na ufuatiliaji ngazi kwa Halmashauri shilingi **811,767,480.00** usimamizi na ufuatiliaji ngazi ya kijiji shilingi **239,700,000**. Aidha, Sekretarieti ya Mkoa imepokea shilingi **88,687,076.07** kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini zinazotekelezwa katika Halmashauri. Jedwali Na.64 linaonyesha mchanganuo wa fedha zilizopokelewa ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri.

- **Utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu (Targeted Infrastructure - TI)**

Katika kipindi cha mwaka 2020 - 2023 Halmashauri ya wilaya Songea, Madaba na Tunduru zimepokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundo mbinu ambapo kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi Desemba 2023 jumla ya Tsh. **1,521,318,958.21** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Miundombinu kama vile Soko, Nyumba ya Mganga, ujenzi wa madarasa na Zahanati.

## Jedwali Na. 60: Mchanganuo wa Miradi ya Miundombinu

| Kata | Kijiji | Mradi Unaotekelezwa | Kiasi Cha Fedha Zilizotolewa | Idadi Ya Walengwa Wanaoshiriki | Hatua (Hali)Ya Utekelezaji Kwa Sasa |
|---|---|---|---|---|---|
| Peramiho | Peramiho A | Ujenzi Wa Soko, Choo Matundu 6, Ghuba Na Vizimba | 185,801,157.85 | Jamii Nzima | 100% |
| Maposeni | Mdunduwalo | Ujenzi Wa Nyumba Mbili Za Mganga (Two In One), Kisima kirefu cha Maji, kichomea taka na Gata za kuvunia maji ya mvua Zahanati Ya Mdunduwalo | 163,573,256.5 | Jamii Nzima | 100% |
| Mpitimbi | Mpitimbi 'B' | Ujenzi Wa Nyumba Moja Ya Mganga | 56,741,360.00 | 49 | 100% |
| Parangu | Parangu | Ujenzi Wa Stend, Maduka Na Uzio | 339,161,371.43 | 0 | 60% |
| Peramiho | Lundusi | Ujenzi Wa Stend Na Vibanda Vya Biashara | 434,657,802.68 | 0 | 60% |
| Madaba | Lituta | Ujenzi Wa Soko,Vyoo Na Vizimba | 171,176,339.29 | 0 | 85% |
| Tunduru | Mkapunda | Ujenzi Wa Zahanati | 92,410,714.29 | 0 | 70% |
| | Chingulungulu | Ujenzi Wa Madarasa Matatu (3) | 77,796,956.17 | 0 | 100% |
| **Jumla Kuu** | | | **1,521,318,958.21** | | |

## 2.22 Sekta ya Utawala

### A. Taarifa ya Hali ya Watumishi Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma mpaka kufikia Juni, 2024 ulikuwa na jumla ya watumishi **14,361** kati ya watumishi **23,346** wanaohitajika na Ofisi ya Mkuu wa mkoa na Halmashauri zote nane (8). Aidha, Mkoa una upungufu wa watumishi **8,985** kama mchanganuo unavyoonyesha kwenye jedwali Na.61

**Jedwali Na. 61: idadi ya watumishi waliopo na upungufu**

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Watumishi | | | Asilimia ya Watumishi Waliopo |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hitajika | Waliopo | Upungufu | |
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 340 | 178 | 162 | 52% |
| 2 | Tunduru DC | 3,988 | 2,300 | 1,688 | 57% |
| 3 | Namtumbo DC | 3,745 | 1,914 | 1,831 | 51% |
| 4 | Songea MC | 3,522 | 2,603 | 920 | 74% |
| 5 | Songea DC | 2,012 | 1,409 | 603 | 70% |
| 6 | Madaba DC | 1,213 | 678 | 535 | 56% |
| 7 | Mbinga TC | 2,146 | 1,462 | 684 | 68% |
| 8 | Mbinga DC | 4,226 | 2,325 | 1,901 | 55% |
| 9 | Nyasa DC | 2,253 | 1,492 | 661 | 69% |
| | **Jumla kuu** | **23,346** | **14,361** | **8,985** | **62%** |

### B. Watumishi waliopandishwa Madaraja

Mkoa wa Ruvuma, umeidhinishiwa kupandisha madaraja jumla ya watumishi **7,050** kwa ikama ya mwaka 2023/2024, kati ya

hao watumishi **5,170** wameshapandishwa madaraja na kubadilishiwa mishahara. Aidha watumishi **1,880** hawajapandishwa kutokana na sababu ya kukosa sifa za kimuundo. Taratibu za kupandisha madaraja watumishi wanaostahili zinaendelea kufanyika. Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja imeonyeshwa kwenye jedwali Na.62

**Jedwali Na. 62: Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja**

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Watumishi | Idadi Ya Watumishi | Idadi Ya Watumishi |
|---|---|---|---|---|
| | | Waliohidhinishwa Kupandishwa vyeo | Waliopandishwa Madaraja Na Kubadilishwa Mishahara | Ambao Bado Hawajabadilishiwa Mishahara |
| 1 | Ofisi ya mkuu wa Mkoa | 66 | 48 | 18 |
| 2 | Tunduru DC | 991 | 584 | 407 |
| 3 | Namtumbo DC | 1173 | 1032 | 141 |
| 4 | Songea MC | 1474 | 755 | 719 |
| 5 | Songea DC | 636 | 409 | 227 |
| 6 | Madaba DC | 285 | 236 | 49 |
| 7 | Mbinga TC | 707 | 568 | 139 |
| 8 | Mbinga DC | 982 | 881 | 101 |
| 9 | Nyasa DC | 736 | 657 | 79 |
| | **JUMLA** | **7,050** | **5,170** | **1,880** |

## C. Ajira Mpya

**K**wa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuletewa jumla ya Watumishi **460** kwa kada za elimu, afya, utawala na miundombinu kutoka Serikali Kuu, Jedwali 63 linaonyesha mchanganuo wa watumishi hao.

**Jedwali Na. 63: Idadi ya watumishi walioajiriwa kwa mwaka 2023/2024**

| Na | Jina la Taasisi | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 12 |
| 2 | H/W Tunduru | 29 |
| 3 | H/W Namtumbo | 143 |
| 4 | Songea MC | 57 |
| 5 | Songea DC | 31 |
| 6 | Madaba DC | 89 |
| 7 | Mbinga TC | 41 |
| 8 | Mbinga DC | 25 |
| 9 | Nyasa | 33 |
| **Jumla** | | **460** |

### 2.22.1 Utekelezaji wa Demokrasia

Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na demokrasia, umeendelea kusimamia uwepo wa vikao vya kisheria katika ngazi zote. Ngazi ya Mkoa vikao vya menejimenti vimekuwa vikifanyika kila wiki kikao 1 ambapo kwa mwezi vinafanyika vikao 4. Vikao vya KAMUS vimefanyika 3 kati ya vikao 4 viliyotakiwa kufanyika. Vikao vya watumishi katika kila sekisheni vinafanyika kila mwezi.Kikao 1 cha baraza la wafanyakazi kimefanyika kati ya vikao 2 vilivyotakiwa kisheria. Aidha, ngazi ya Wilaya vikao vimekuwa vikifanyika kwa kufuata taratibu ikiwa na lengo la kuhakikisha changamoto zote za watumishi zinafanyiwa kazi kwa wakati na kuleta ufanisi katika utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa umma.

### 2.22.2 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
### Taarifa ya Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Kodi

### A. Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Ruvuma unazo Wilaya tano yaani Wilaya ya Songea, Mbinga, Tunduru, Namtumbo na Nyasa. Pia unacho kituo cha huduma kwa Mlipakodi kinacho patikana Wilaya ya Madaba.

Kwa upande mwingine, Mkoa unavyo vituo viwili vya forodha yaani kituo cha Mkenda Nakawale na Mbambabay.

### B. Makusanyo Julai, 2023- Juni, 2024

Kwa kipindi cha Julai**, 2023** hadi Juni**, 2024;** Mamlaka ya Mapato mkoa wa Ruvuma ilipangiwa lengo la kukusanya **TSHS. 17,430,066.646.00** Ilifanikiwa kukusanya **TSHS. 20,328,874,383.54** sawa na asilimia **117%,** mchanganuo wa lengo na makusanyo kwa kila mwezi umeonyeshwa kwenye jedwali Na.64.

**Jedwali Na. 64: Makusanyo Julai, 2023- Juni, 2024**

| Mwezi | Mwaka | Lengo la Mwezi | Makusanyo Mwezi | Utendaji |
|---|---|---|---|---|
| Julai | 2023 | 1,322,344,899.00 | 1,079,308,537.07 | **82%** |
| August | 2023 | 1,261,788,574.00 | 1,507,280,993.95 | **119%** |
| Septemba | 2023 | 1,471,225,314.00 | 2,335,012,733.36 | **159%** |
| Oktoba | 2023 | 1,369,988,452.00 | 1,645,259,340.66 | **120%** |
| Novemba | 2023 | 1,313,773,720.00 | 1,540,433,795.22 | **117%** |
| Desemba | 2023 | 1,887,780,457.00 | 2,268,030,249.85 | **120%** |
| Januari | 2024 | 1,350,320,208.00 | 1,432,462,570.13 | **106%** |
| Februari | 2024 | 1,301,741,214.00 | 1,501,852,020.67 | **115%** |
| Machi | 2024 | 1,553,652,881.00 | 1,831,412,515.50 | **118%** |
| Aprili | 2024 | 1,321,259,674.00 | 1,571,505,892.51 | **119%** |
| Mei | 2024 | 1,350,788,444.00 | 1,351,391,101.54 | **100.4%** |
| Juni | 2024 | 1,925,402,809.00 | 2,328,874,383.54 | **121%** |
| **Jumla** | | **17,430,066,646.00** | **20,392,824,134.00** | **117%** |

## C. Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Mkoa

Serikali kupitia Uongozi wa juu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania iliweza kutenga fedha na kufanya ukarabati Mkubwa wa jengo la Ofisi ya Mkoa. Kwani hapo awali jengo lilikuwa chakavu na hali mbaya. Jengo limekamilika na linatumika.

Kukamilika kwa jengo hili kumewezesha kuwa na nafasi ya kutosha kwa watumishi pamoja na walipakodi ambao hufika kupata huduma.

Tunaishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya **Mh. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan** kwa kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati huu ambao umeboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**D. Changamoto za Utekelezaji wa Majukumu Yahusuyo Makusanyo ya Kodi**

**(i)** Matumizi hafifu ya Matumizi ya Mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD);

**(ii)** Baadhi ya Taasisi za Serikali kutowasilisha kodi ya zuio (Withholding Tax on goods and services);

**(iii)** Baadhi ya wafanya Biashara kutowasilisha ritani mbalimbali kwa wakati;

**(iv)** Baadhi ya wafanya Biashara kutolipa kodi kwa wakati;

**(v)** Baadhi ya wafanya Biashara kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya masuala yahusuyo kodi;

**(vi)** Biashara ya Magendo kwa kutumia njia zisizo rasmi.

**E. Mikakati na Malengo**

**(i)** Kuendelea kutoa elimu kwa wafanya Biashara na wadau wengine ndani ya Mkoa wa Ruvuma

**(ii)** Kuwakumbusha walipakodi kuwasilisha ritani na kufanya malipo kwa wakati

**(iii)** Kutoa elimu kwa taasisi za Serikali zinazo husika na uwasilishaji wa kodi ya zuio.

**(iv)** Kuwahimiza walipakodi kulipa malimbiklizo ya kodi za nyuma kwa kuingia nao Mikataba ya namna ya kulipa madeni yao.

**(v)** Kusimamia utoaji wa vibali vya leseni (Tax Clearance pamoja na Stika za Magari)

**(vi)** Kuboresha utoaji wa huduma kwa kutoa mafunzo Maalum kwa wafanyakazi.

**(vii).** Kusimamia matumizi ya EFD, kwa kuwaweka maafisa katika maeneo ya starehe na maeneo mengine muhimu kwa ajili ya kusimamia utoaji wa Risiti. Pia kufanya mazoezi ya Kukagua mizigo ili kuhimiza wajibu wa kudai na kutoa risiti kwa mauzo au huduma zitolewazo.

**(vii).** Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Stempu za kielektroniki kwa kutembelea maeneo ya mauzo ya vimiminika kuhakiki uhalali wa stempu maeneo hayo kama, Baa, Majumba ya Starehe, Maduka ya vinywaji ya jumla na rejareja;

**(viii).** Kutembelea maeneo mbalimbali kama, Songea vijijini, Songea wilayani ili kuongeza wigo wa walipakodi;

**(ix).** Kusimamia ukaguzi wa bidhaa zote zinazoingia nchini, kwa kufuata utaratibu kwa mujibu wa sheria za forodha na ushuru, ikiwa pamoja na kuthaminisha thamani ya mizigo hiyo;

**(x).** Kusimamia ubadilishaji umiliki wa vyombo vyote vya moto kutoka kwa wanufaika wa misamaha kwenda kwa wasio wanufaika wa misamaha;

**(xi).** Kufanya doria katika sehemu mbalimbali ndani ya mkoa ili kudhibiti mianya yote ya bidhaa kuingizwa kwa njia ya magendo;

**(xii).** Kutambua idadi ya majengo na mabango kwa kushirikiana na watendaji wa mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa kukusanya kodi za pango Pamoja na ushuru wa mabango na

**(ix).** Kushirikiana na washikadau wa Mamlaka ya Mapato kama TCCIA na JWT, kuwakusanya wamiliki wa biashara ili wahudhurie semina stahiki za kodi.

## F. Hitimisho

Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla inamshukuru Mh. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuweka mazingira rafiki ambayo yamewezesha kukua kwa Biashara na kuongezeka kwa makusanyo ya kodi.

Pia tuna shukuru uongozi wa Mkoa chini ya Mkuu wa Mkoa pamoja na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kwa ushauri na

Maelekezo ya Mara kwa mara ambayo yametuwezesha kuendelea kufanya vizuri katika makusanyo yatokanayo na kodi.

Mwisho tunawashuru viongozi wa wafanya Biashara pamoja na wafanya Biashara wa mkoa wa Ruvuma kwa kuendelea kuwa na ushirikiano katika masuala yahusuyo ulipaji wa kodi.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

### 2.22.3 Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 2023/24.

Mkoa wa Ruvuma katika mwaka 2023/24 uliidhinishiwa kukusanya **Tshs 29,167,014,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Hadi kufikia Juni, 2024 kiasi cha **Tshs 30,514,972,395.92** zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo ikiwa ni sawa na asilimia **104.62** ya lengo la makusanyo. Jedwali Na. 65 linaonesha malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

**Jedwali Na. 65: Malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kufikia Juni, 2024.**

| Taasisi | Lengo la Makusanyo 2023/24 | Makusanyo kufikia Juni, 2024 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Mbinga TC | 2,476,487,000.00 | 2,455,808,805.36 | 99.17 |
| Mbinga DC | 6,900,000,000.00 | 7,539,011,686.98 | 109.26 |
| Songea MC | 6,069,654,000.00 | 5,639,578,041.85 | 92.91 |
| Tunduru DC | 5,470,503,000.00 | 6,420,523,668.39 | 117.37 |
| Namtumbo DC | 2,747,631,000.00 | 2,833,323,992.14 | 103.12 |
| Songea DC | 2,468,957,000.00 | 2,631,803,853.02 | 106.60 |
| Nyasa DC | 1,744,005,000.00 | 1,820,627,593.00 | 104.39 |
| Madaba DC | 1,289,777,000.00 | 1,174,294,755.18 | 91.05 |
| **Jumla** | 29,167,014,000.00 | 30,514,972,395.92 | **104.62** |

### 2.22.4 Ujenzi wa Miundombinu Mbalimbali ya Sekretarieti ya Mkoa

Katika mwaka wa fedha **2023/24**, Sekretarieti ya Mkoa ilitekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za viongozi zikiwemo; Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Mkoa, Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Songea na Mbinga, Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Sehemu, ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ujenzi wa Ofisi ya Afisa Tarafa Sasawala. Katika utekelezaji wa kazi zote hizo jumla ya kiasi cha fedha za Kitanzania Tsh **817,000,000.00** zilipokelewa na kutumika. Mchanganuo wa fedha kwa kila mradi ni kama ifuatavyo;

i. **Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Mkoa**

Kiasi cha fedha cha Tsh **110,000,000.00** kimetumika katika ujenzi wa Makazi ya Mkuu wa Mkoa

ii. **Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Wilaya Mbinga na Songea**

Kiasi cha fedha cha Tsh **465,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Songea na Mbinga.

iii. **Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala Msaidizi**

Kiasi cha fedha cha Tsh **72,000,000.00** kimetumika kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Songea.

iv. **Ujenzi wa Ofisi ya Afisa Tarafa Sasawala**

Kiasi cha fedha cha Tsh **110,000,000.00** kimetumika katika ujenzi wa Ofisi ya Afisa Tarafa Sasawala.

v. **Ukarabati wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa**

Kiasi cha fedha cha Tsh **60,000,000.00** kimetumika katika ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa sehemu ya ukumbi wa mikutano ambako ukarabati unaendelea.

### 2.22.5 Vitendea Kazi vya Ofisi

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika mwaka wa fedha 2023/24 imepokea magari matatu ya Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na gari moja la Ufuatiliaji na Tathmini ngazi ya Mkoa.

### 2.22.6 Hitimisho

Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa makundi yote ikiwemo wazee wa Mkoa wa Ruvuma, Vijana na wanawake, watumishi wa umma, Sekta binafsi, Mashirika ya umma na ya binafsi, taasisi za kidini na viongozi wa ngazi zote wa chama na Serikali wanaendelea vyema na shughuli zao za kiuchumi pamoja na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Mara nyingine, kwa moyo wa dhati nikukaribishe Mkoani Ruvuma.